Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Nane - Tarehe 28 Aprili, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA FEDHA:**

Hati ya Uhamishaji Fedha Na.2 ya Mwaka 2004/2005 *(Statement of Reallocation Warrant No.2 of 2004/2005).*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa Maalum ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

**MHE. PRO. HENRY R. MGOMBELO- MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDO MBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Miundo Mbinu, kwa Mwaka 2004.

**SPIKA:** Ahsante. Nimearifiwa kwamba Hati ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala itawasilishwa mezani kesho, siyo leo. Kwa hiyo, tunairuka tunaendelea na *Order Paper.*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 103

**Vazi la Spika**

**MHE. SALOME J. MBATIA** aliuliza:-

Kwa kuwa Vazi Rasmi la Mheshimiwa Spika ni zuri na nadhifu:-

(a) Je, nakshi ambazo zimepamba vazi hilo yakiwemo mazao mbalimbali kama mahindi, korosho na kadhalika zinaashiria nini?

(b) Je, vazi hilo lilibuniwa na nani?

(c) Je, Mabunge yote duniani hususan katika nchi za Jumuiya ya Madola yana vazi rasmi la Spika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Vazi Rasmi la Mheshimiwa Spika, limewekwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 119(2). Kwa mujibu wa Kanuni hiyo, Vazi Rasmi la Spika, litakuwa ni joho lenye kuonyesha rangi za Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa na baadhi ya mazao makuu nchini.

Aidha, kwa namna lilivyoshonwa vazi hilo kwa hakika ni zuri na nadhifu, kama alivyokiri Mheshimiwa muuliza swali.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakshi ambazo zimepamba vazi hilo ni pamoja na mazao mbalimbali yakiwemo mahindi, korosho na kadhalika. Mazao hayo ni baadhi tu ya mazao makuu nchini yakiashiria kilimo kuwa ndiyo sekta kiongozi katika uchumi wa nchi yetu.

(b) Vazi hilo Rasmi la Mheshimiwa Spika, lilibuniwa na Kamati Maalum ya Waheshimiwa Wabunge, ambayo iliteuliwa mwaka 1994 kwa madhumuni mahsusi ya kubuni Vazi la Spika. Kamati hiyo pia ilishirikisha Wataalam wa Idara ya Sanaa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

(c) Mheshimiwa Spika, si Mabunge yote duniani au katika Jumuiya ya Madola yaliyo na Vazi Rasmi la Spika. Yapo Mabunge mengine ambayo hayana Vazi Rasmi la Spika. Inategemea uamuzi wa Bunge lenyewe na nchi inayohusika.

**SPIKA:** Vazi la Spika ni la Spika jamani, mwachie mwenyewe. *(Kicheko)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Nashukuru kuona katika vazi zuri la Mheshimiwa Spika, lina nembo ya korosho na wakati huo huo naona korosho kama haipewi heshima yake. Je, sasa hivi ndilo lingezidi kuwa na hadhi nzuri zao hili la korosho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Halitokani na swali la msingi lakini unaweza kujibu Waziri kama unayo majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mimi nafikiri imepewa heshima zaidi korosho kuwekwa kwenye vazi la Spika badala ya kutopewa heshima na kwa kweli katika nchi hii Serikali inatilia maanani sana uimarishaji wa zao la korosho na hasa kwa kuzingatia ni miongoni mwa mazao makuu yanayoipatia fedha Serikali. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuimarisha mikakati ya kuboresha zao hili ili liendelee kuwa miongoni mwa mazao makuu ya uchumi wa nchi hii.

Na. 104

**Kushindwa Kuwalipa Watendaji wa Vijiji**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilipojibu Swali Na. 11 katika Kikao cha Pili cha Mkutano wa 18 wa Bunge hapo tarehe 2/2/2005 ilikiri kushindwa kutekeleza kikamilifu ahadi yake ya kubeba mzigo wa kuwaajiri Watendaji wote wa Vijiji vyote nchini kuanzia Januari, 2004; na kwa kuwa, kutokana na kauli hiyo kumezuka mtafaruku mkubwa katika maeneo ambayo Watendaji hao hawakuwa wamelipwa na vilevile wale waliolipwa, wamelipwa mishahara ya miezi michache au kiasi cha shs.256,000/=.

(a) Je, Serikali inatamka nini kuhusu ukiukwaji huo mkubwa wa haki kati ya mwajiri na mwajiriwa na kwamba, hali hiyo haiashirii hatari kwa Serikali kushtakiwa na waajiriwa hao?

(b) Kama ilivyofanyika kwa walimu katika Mkutano wa bajeti 2004/2005. Je, kwa nini isitenge fedha za dharura kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kuhudumia hao Watendaji wa Vijiji 2150 ambao hawajalipwa kabisa ili kuondoa manung'uniko juu ya Watendaji 7,000 waliolipwa kati ya zaidi ya Watendaji 9,000?

(c) Je, Serikali inatamka nini kuhusu malimbikizo ya mishahara ya watumishi hao kuanzia mwaka 2004 hadi watakapolipwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimeombwa nilijibu kwa makini, basi naomba univumilie litakuwa refu kidogo.

(a) Mheshimiwa Spika, tarehe 2/2/2005 nililieleza Bunge lako Tukufu azma ya Serikali ya kuajiri Watendaji wa Vijiji vilivyosajiliwa 9,808 wenye sifa kwa lengo la kuimarisha Serikali za Vijiji kuanzia Januari, 2004. Aidha, nililieleza Bunge lako Tukufu juu ya kukwama kwa zoezi hilo kwa sababu kubwa tatu zifuatazo:-

* Uhaba mkubwa wa watu wenye sifa zilizoainishwa;

* Utaratibu mrefu wa kutangaza nafasi;

* Ushauri kutoka ngazi mbalimbali za uongozi likiwemo Bunge kwamba kuwaondoa Watendaji wa Vijiji waliopo wasio na sifa zilizoainishwa kungesababisha manung'uniko makubwa kutoka kwa Watendaji hao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizi tarehe 9/2/2004 Serikali ililazimika kutoa tamko la kubadili utaratibu wa ajira za Watendaji wa Vijiji uliokuwa umetolewa na badala yake Serikali ikaamua kuendelea na Watendaji wa Vijiji waliokuwepo. Utaratibu wa awali wa ajira ulikuwa unaipatia Serikali nafasi ya kufanya zoezi hili kwa awamu kwa kuwa haikutegemewa kwamba watu wenye sifa zilizoainishwa wangeweza wote 9,808 kupatikana kwa wakati mmoja. Baada ya tamko la Serikali la tarehe 9/2/2004 Serikali ililazimika sasa kushughulikia Watendaji wa Vijiji waliokuwepo ambao ni wengi tofauti na matarajio yake ya awali. Hivyo Serikali ililazimika kuajiri Watendaji hao kwa awamu kulingana na uwezo wa Bajeti ya Serikali kama ilivyopitisha na Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka wa Fedha 2003/2004 kuanzia mwezi Mei 2004 Watendaji wa Vijiji 3,940 waliajiriwa na fedha iliyotengwa ni shs. bilioni 5.7 kwa ajili ya mishahara yao ya miezi ya Mei na Juni, 2004 pamoja na mafunzo.

(ii) Mwaka wa Fedha 2004/2005 kuanzia mwezi Julai, 2004 Watendaji wa Vijiji 3,421 ndiyo walioingizwa katika ajira na fedha iliyotengwa na Bunge lako Tukufu baada ya kupitishwa ni shs. bilioni 5 kwa ajili ya mishahara yao ya miezi ya Julai, 2004 hadi Juni 2005. Kwa bahati mbaya fedha hiyo haikutosha pamoja na mafunzo. Fedha ya mafunzo yao imetokana na msaada toka *JICA*. Jumla ya shs. bilioni 5 pia zimetumika kugharamia mishahara ya Watendaji wa awamu ya kwanza kwa miezi ya Julai hadi Juni, 2005. Hii inafanya jumla ya Watendaji wa Vijiji wanaolipwa mishahara toka Serikalini kuwa 7,361 kati ya Watendaji wa Vijiji 9,808.

(iii) Mwaka wa Fedha 2005/2006 Watendaji wa Vijiji waliobakia 2, 191 na Watendaji wa Mitaa 1,746 wataanza kulipwa mishahara na Serikali sambamba na wenzao wa awamu ya

Kwanza na Pili kuanzia Julai, 2005 baada ya fedha za mishahara yao kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa katika mazingira haya Watendaji wa Vijiji watakaoanza kupata mishahara yao kuanzia mwezi Julai, 2005 watakuwa na manung'uniko. Ili kupunguza manung'uniko haya Ofisi yangu iliziagiza Halmashauri zote nchini zichukue jukumu la kuziba pengo hilo kwa kuwalipa Watendaji hawa fedha wakati Serikali inakamilisha taratibu za mishahara yao kupitia Serikali kwa kipindi cha Mei 2004 - Juni, 2005 kwa kuzingatia kwamba Watendaji hawa ni watumishi wao tangu awali.. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Halmashauri nyingi zimetekeleza maagizo haya na hivyo kupunguza malalamiko kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi hizi za Serikali hatutegemei kwamba wapo Watendaji wa Vijiji watakaotaka kuishtaki Serikali yao baada ya kuwaandalia mfumo wa uhakika wa ajira kama huu. Kuhusu baadhi ya Watendaji kulipwa mishahara yao kwa miezi michache Ofisi yangu inatambua tatizo hilo, lakini linashughulikiwa kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali na Mitaa, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma pamoja na Hazina

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa na nia nzuri ya kutekeleza azma yake kama ilivyoahidi lakini tatizo limekuwa ni ufinyu wa bajeti. Waheshimiwa Wabunge nanyi ni mashahidi. Mmejitahidi sana kuishauri Serikali wakati wa kuchangia hotuba zangu za Bajeti ifanye kila liwezekanalo kutimiza azma yake lakini haikuwezekana. Aidha, uwezekano wa Serikali kutumia fedha dharura nao vile vile umeshindikana kutokana na fedha ndogo iliyopo ikilinganishwa na mahitaji ya Mfuko huo wa dharura.

(c) Mheshimiwa Spika, suala la ajira ya Watendaji wa Vijiji linaambatana na mambo muhimu miwili; kwanza ni upatikanaji wa fedha na pili ni kutolewa kwa mafunzo kwa Watendaji hao

. Kwa kutambua mambo hayo Serikali ilizielekeza Halmashauri zote kuhakikisha ajira za Watendaji hawa zinapata kibali kutoka Ofisi yangu kabla ya barua za ajira kutolewa. Kwa bahati mbaya jambo hili halikuzingatiwa kwa kiasi kikubwa na ndiyo maana kumekuwa na tatizo hili ambalo sasa linajitokeza.

Hata hivyo, naomba kuliarifu Bunga lako Tukufu kwamba bado Serikali imedhamiria kumaliza tatizo hili katika Bajeti ya mwaka ujao. Hivyo, endapo yapo malimbikizo ya malipo hayo ambayo yamedaiwa katika swali la Mheshimiwa Mbunge, basi tutaendelea kuyashughulikia kati ya Halmashauri hizo na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali na Mitaa.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nimefurahi kwa majibu mazuri na ya kina ya Mheshimiwa Naibu Waziri na nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa ni kweli kwamba Watendaji hawa wamekwishakupewa barua na katika Jimbo langu kuna Kata nyingine ambapo Watendaji hawakupewa kabisa mishahara. Pia

vilevile katika Kata nyingine wamepewa mishahara Watendaji wawili na wengine hawakupata wote. Sasa katika hali ya namna hii Serikali inawahakikishiaje ili wasije wakaleta vurugu hasa katika kipindi cha uchaguzi ambapo hawa ndiyo Watendaji ili hawa wawe na uhakika wa kupata haki zao?

La pili, kwa kuwa Halmashauri zetu hazina fedha na Serikali imeagiza kwamba Halmashauri zitapata fedha na hizo fedha zitatoka wapi? Maana si kweli kwamba Halmashauri zimelipa, Halmashauri nyingi hazijalipa. Serikali inatamka nini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza ni kweli katika zoezi hili na kwa namna mgao ulivyofanyika ziko baadhi ya Kata ambazo zimejikuta hazina Ma-*VEO* katika baadhi ya vijiji vyake na hii ilitokana na sababu moja kubwa kwamba wakati tumepeleka maelekezo kwa Halmashauri zetu baadhi ya Halmashauri zili-*respond* haraka sana na kwa hiyo zoezi lao kwa maana ya Halmashauri hizo likawa jepesi. Wengine walichelewa mno mpaka dakika za mwisho tukalazimika kwa hiyo kugawa Ma-*VEO* hawa katika makundi machache machache ili kuweza kukidhi angalau mahitaji yanayohitajika. Kwa mfano, kwa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto wao wanao Watendaji wa Vijiji 166, lakini tulilazimika kuchukua 126 tu ili kuweza kuachia nafasi kwa Halmashauri nyingine. Kwa hiyo, ni tatizo lipo na tunalijua lakini tunaendelea kwa kweli kulitazama tuone namna tutakavyolikamilisha katika bajeti inayofuata.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kabisa kwamba tunatambua kwamba Halmashauri nyingine zina matatizo, tuseme nyingi zina matatizo makubwa ya kifedha. Lakini maadam Halmashauri kama nilivyosema yeye anasema si nyingi, na mimi nasema kwa taarifa tulizonazo ziko idadi ya kutosha kuweza kuthibitisha wameweza kushughulikia zoezi hili vizuri sana. Kwa hiyo, mimi niziombe Halmashauri zote zilizobaki Watendaji hawa walikuwa ni waajiriwa wao, Serikali ilichofanya ni kuwatua mzigo huo kwa kuwasaidia. Sasa tusaidiane zisikwepe jambo hili zibebe mzigo ni miezi michache tu baada ya hapo wanaingia katika utaratibu wa kawaida wa Serikali Kuu.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na katika mawasilisho ya Bajeti ya Wizara ya TAMISEMI mwaka jana waliwasilisha fedha za kutosha za kuwalipa Watendaji hao. Je, ni kitu gani kilitokea baada ya hapo kwamba sasa Watendaji hawa wagawanywe kwenye awamu. Serikali inatuambia kwamba ilifanya kosa la kimahesabu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sitaki kubishana na Mheshimiwa Mbunge. Lakini naomba nirudie tu nilichosema kwamba fedha zilizotengwa ambazo zilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka jana zilikuwa ni bilioni 5/= kiasi hicho cha fedha hakikuweza kutosheleza kutoa ajira kwa Watendaji wote wa Vijiji, tuweze tu kuajiri Watendaji wapatao 3,600 hivi. Huo ndiyo ukweli na ndivyo takwimu zilivyo. Vinginevyo hatuna sababu nyingine yoyote ya kuacha kuajiri wote wakati tunajua vijana hawa tungependa wapate mishahara yao ili wafanye kazi kwa

ari zaidi. Ndiyo maana hata mwaka wa kwanza mlitoa bilioni 5.7 kwa sababu hiyo hiyo. Safari hii ndiyo tunatarajia zoezi hilo litaweza kumalizika.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali ndogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inakiri kabisa kwamba uwezo wa Halmashauri ni mdogo sana; na kwa kuwa katika Jimbo langu la Siha wako Watendaji ambao kila wakati wanakuja nyumbani kwangu na ofisini wakidai haki zao hizo. Je, Serikali Kuu kwa Halmashauri zile ambazo hazina uwezo itakubali kulipa *arreas* zao kwa sababu amesema kwamba wapo ambao hawajalipwa toka huko nyuma na uwezo ni mdogo itakuwa tayari kulipa arreas zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Hai ina Watendaji 85 na katika hao tulioweza kuwaajiri ni Watendaji 34 wengine bado ndiyo hao tunasema tutawaajiri katika awamu inayofuata. Hao ambao hatukuwaajiri ndiyo hao ambao tunasema tatizo lao ndiyo tunategemea litamalizika kupitia Bajeti ya mwaka huu baada ya Bunge kukubali kupitisha Bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la *arreas* katika mazingira haya ambayo ninayaeleza ni ngumu sana. Mimi nafikiri Waheshimiwa Wabunge wote tukubali tu mzigo ni mkubwa tunajitahidi kuutua na ndiyo maana tumesema ajira hizo zitakwenda na mambo mawili ni kuwepo kwa fedha lakini vilevile mafunzo. Hao wote ambao wamebaki 2,191 hata kama wanazo barua ili mradi fedha hazipo na hawajapita kwenye mafunzo itakuwa tunajidanganya kusema kwamba tuwatafutie *arrears* kwa sababu mzigo huo hautabebeka na Serikali hii katika mazingira tuliyonayo. Naomba tupige moyo konde tuwasaidie hao vijana kuwaeleza ukweli ili bajeti ijayo waweze na wao kuingizwa katika utaratibu.

**Na. 105**

**Barabara ya Nyigo - Mgololo**

**MHE. BENITO M. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Nyigo - Mgololo inayopita katika vijiji vya Ihawaga, Mtulingala, Nyamande, Kitandililo, Usaula, Kiyowera Makungu - *SPM Mgololo* ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi; na kwa kuwa barabara hiyo inahudumia Kiwanda cha *SPM - Mgololo* kwa kupeleka mafuta na kuchukua karatasi toka Kiwandani hapo na kuzisambaza nchini; na kwa kuwa barabara hiyo inakwenda sambamba na Reli ya *TAZARA* hivyo kuwa na umuhimu wa pekee hasa ikiwa kutatokea dharura yoyote katika reli:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha maalum kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo kama inavyofanya kwa *TANZAM highway* na nyinginezo?

(b) Kwa kuwa barabara hiyo imeanzia Nyigo - Wilayani Mufindi, halafu ikaingia Mtulingala kuingia Wilaya ya Njombe, baada ya hapo ikaingia tena Isaula - Wilayani Mufindi hadi *SPM - Mgololo*; je, ni Halmashauri gani inayowajibika kuitengeneza?

(c) Kwa kuwa barabara hiyo muhimu sana ina urefu wa Km.65. Je, ni lini Mfuko wa barabara kupitia TAMISEMI utazihudumia barabara hizo moja kwa moja badala ya kupitia mgao wa Halmashauri za Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito M. Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara ya Nyigo - Mgololo inayounganisha vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu pamoja na Mheshimiwa Mbunge kuwa utaratibu unaotumika kwa Halmashauri kupatiwa fedha za Mfuko wa Barabara ni kama ifuatavyo:-

(i) Halmashauri inapaswa kuandaa Mpango wa Matengenezo ya Barabara *(Road Maintenance Master Plan).*

(ii) Mpango huo lazima upitishwe na Baraza la Madiwani (Halmashauri)

(iii) Baada ya kupitishwa na Halmashauri mpango huo huwasilishwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

(iv) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hujumuisha mipango ya barabara *(Consolidate)* kwa Halmashauri zote.

(v) Mpango uliojumuishwa *(Consolidated)* hupelekwa kwenye Bodi ya Mfuko wa Barabara *(Road Fund Board)* kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali katika suala hili ni kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kufuata utaratibu huu wala sio vinginevyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hiyo inapita katika vijiji vilivyopo Wilayani Mufindi na Njombe, inapaswa kuhudumiwa na Halmashauri zote mbili kwa umbali tofuati uliomo katika Halmashauri hizo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Matengenezo ya Barabara wa Serikali za Mitaa kwa kuzingatia kipaumbele;

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kawaida Mfuko wa Barabara wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa huwa hautengi fedha moja kwa moja kwa ajili ya barabara maalum. Kwa vile Halmashauri husika bado inaona umuhimu wa barabara hiyo kiuchumi na kijamii naomba kushauri kwa dhati kuwa waendelee kutoa kipaumbele katika barabara hii kupitia Mfuko wa Barabara, na kama hapana budi waandae andiko maalum *(Write up)* ya kuomba fedha kwa wadau mbalimbali ikiwemo Serikali Kuu kupitia Mkoa wao wa Iringa.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu na hasa ikizingatiwa kwamba sasa hivi Mwekezaji katika Kiwanda cha *SPM* amepatikana na ameleta vifaa vingi; na kwa kuwa amekuwa akilalamika mara nyingi sana kuhusu barabara hii; na kwa kuwa Bodi ya Mkoa wa Iringa kwa muda mrefu imekuwa ikiiomba Serikali ichukue barabara hii iwe barabara Mkoa. Katika kipindi cha miaka 10 nikiwa kama Mbunge ombi hili limekuwa nikiliomba sana. Kwa nini Serikali imekuwa haikubali kuichukua barabara hii ikizingatiwa kwamba miaka yote ya nyuma imekuwa ni barabara ya Mkoa? *(Makofi)*

(b) Hata utaratibu wa kuunganisha .....

**SPIKA:** Hebu punguza utangulizi uliza swali moja kwa moja.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** (b) kwa kuwa

**SPIKA:** Ahaa uliza swali. Je...........! *(Kicheko)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** (b) Je, ni hatua gani ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri ataisaidia Wilaya ya Mufindi ili iweze kukutana na Wilaya ya Njombe ili kufanya utaratibu kwamba fedha za Wilaya ya Njombe pia ziweze kusaidia matengenezo ya barabara hii?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali lile la kwanza. Maombi ya barabara ambazo zinatakiwa ziingie kuwa katika *highway code* zimepokelewa na Wizara ya Ujenzi kutoka kila Mkoa na zipo katika *highway code* ambayo inaletwa Bungeni. Hapo itakapoletwa Bungeni na kujadiliwa na kupitishwa ndiyo zile barabara za Wilaya zinazoombewa kuwa za Mkoa zitakuwa za Mkoa na zingine za Mkoa zitaombwa zitoke kupunguza. Lakini kwa sasa hivi haiwezekani kubadilisha tu barabara bila kupitishwa kwenye sheria. Kwa hiyo, maombi hayo tunayo na tunayafanyia kazi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijajibu hilo pengine nimwombe tu Mheshimiwa Benito Malangalila ahakikishe basi kwamba maombi ya barabara hii yapo katika Ofisi ya Ujenzi maana vinginevyo ataendelea kuuliza swali hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Benito Malangalila anataka nimsaidie namna ya kumwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na Njombe kuweza kukutana pamoja na kutazama namna nzuri zaidi ya kufanya kazi kwa kutumia resources walizonazo au fedha walizonazo kuhudumia barabara hii.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama hili ni mgogoro mkubwa. Wilaya ya Njombe, Wilaya ya Mufindi zote ziko katika Mkoa wa Iringa. Halmashauri zote hizi mbili hukutana kwenye

*Road Board,* kwenye *RCC.* Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba wanacho chombo ambacho kinaweza kabisa kikawasaidia kutatua tatizo hili kama kweli lipo. Lakini katika mazingira ya kawaida ninayoyajua mimi wanachohitaji hapa ni Halmashauri zote mbili kuingiza mipango ya barabara hiyo kila upande katika kilomita zinazostahili. Vinginevyo nadhani halina tatizo hata kidogo.

**Na. 106**

**Kuwaendeleza Kitaaluma Maafisa Afya Wasaidizi**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la kuwaendeleza kitaaluma Maafisa wa Afya Wasaidizi ni muhimu sana; na kwa kuwa, Serikali ilitamka Bungeni kwamba, lengo la kufunga vyuo vinavyotoa mafunzo ya wataalamu hao ni kuwaendeleza Maafisa Afya Wasaidizi walioko kazini wafikie ngazi ya kuwa Maafisa Afya:-

(a) Je, Serikali ilikuwa na sababu gani za msingi za kuwafukuza Vyuoni Maafisa Afya Wasaidizi waliochaguliwa mwaka 2004 kujiunga na Vyuo vya Afya ili kujiendeleza kitaaluma kwa ngazi ya Stashahada?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba, Maafisa hao walifanya mitihani na walipofaulu Serikali iliwapelekea barua za wito wa kujiunga na Vyuo vya Afya Mpwapwa, Muhimbili na Tanga?

(c) Kwa kuwa Maafisa hao wamesomea kazi hiyo kwa muda wa miaka miwili katika Vyuo vya Afya na kupata vyeti vya Afya ya Mazingira.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, vyeti walivyonavyo vinatosha kabisa kuwa na sifa ya kujiunga na Vyuo vya Afya na kupata Stashahada badala ya kuwafukuza Vyuoni kwa kuwa hawana vyeti vya kidato cha nne ambapo hapo awali Serikali haikutoa vyeti hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Maafisa Afya Wasaidizi wamekuwa wakitoa huduma za kinga katika ngazi mbalimbali za Mikoa na Wilaya. Kama walivyo wafanyakazi wengine katika Sekta ya Afya, watumishi hawa hujiendeleza kitaaluma kuwa Maafisa Afya yaani Stashahada baada ya kufanya mtihani wa kujiendeleza. Kwa wakati huu Wizara inayo Vyuo vitatu (3) nchini vya Maafisa Afya ambavyo ni Mpwapwa, Muhimbili na Tanga. Vyuo hivi vyote kitaaluma vipo chini ya Chuo

Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili *(MUCHS).* Hivyo uchaguzi wa watumishi hawa kujiunga na mafunzo ya kujiendeleza hufanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imetoa mwongozo wa kiwango cha chini cha elimu cha mtumishi wa umma kuwa ni elimu ya sekondari ya kidato cha nne, yalifanyika majadiliano kati ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili na Uongozi wa Wizara ya Afya ambapo muafaka ulifikiwa kwamba katika Vyuo vya Muhimbili na Tanga wachukuliwe wenye kiwango cha elimu ya kidato cha nne na wale wote ambao hawana kiwango hicho cha elimu ambao idadi yao ni 42 kati ya wanafunzi 112 wapelekwe Chuo cha Mpwapwa na utaratibu ufanyike ili waweze kupata elimu ya kiwango cha sekondari wakiwa Chuoni hapo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali ndogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na majibu ambayo yanawapa matumaini Maafisa wa Afya hapa nchini. Nina swali ndogo la nyongeza. Kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba na Mheshimiwa Naibu Waziri yeye amekiri kwamba Mabwana Afya hawa wanafanya kazi katika Idara ya Afya ya Kinga.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba sasa iko haja ya kuimarisha Idara ya Afya ya Kinga ili kupambana na magonjwa ya kuambukiza kama vile malaria, kipindu pindu, homa ya matumbo kwa kuwapatia Mabwana Afya hawa vitendea kazi kama vile baiskeli, pikipiki na magari. Je, atakubaliana nami hilo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninakiri kwamba kinga ni bora kuliko tiba na jambo hili limepewa kipaumbele kikubwa sana chini ya utendaji wa Wizara ya afya.

Mheshimiwa Spika, tuna idara maalum ya kinga katika Wizara ya Afya ambayo pamoja na mambo mengine jukumu lake ni kuhakikisha kwamba kinga inatiliwa mkazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mabwana Afya kupatiwa vifaa utaratibu uliopo sasa ni kwamba Mabwanaafya wako chini ya Halmashauri za Wilaya. Idara ya Afya, Halmashauri za Wilaya inatakiwa kuhakikisha ili Mabwana Afya waweze kufanya kazi yao kwa usahihi ni vyema wahakikishe kwamba wanaweka Bajeti ya kuwapatia vifaa ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Na. 107

**Kukataza Uvutaji wa Sigara Kwenye Maeneo Fulani**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limetunga Sheria Na. 3 ya Mwaka 2003 kuhusu Bidhaa za Tumbaku *(Tobacco Products Act, 2003 (No. 3/2003);* na kwa kuwa, katika sehemu ya nne ya kifungu cha 12 cha sheria hiyo kinazuia uvutaji wa sigara katika maeneo fulani:-

(a) Je, sheria hiyo imeanza kutumika lini na inatoa majukumu kwa vyombo na watu gani kusimamia utekelezaji wake?

(b) Je, ni maeneo gani hasa yanakatazwa kvutia sigara na ni adhabu gani zimewekwa kwa wakosaji?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bunge na. 2 ya mwaka 2003 kuhusu Udhibiti wa Matumizi ya Tumbaku na Mazao yake ilianza kutumika Julai, Mosi, 2003 kwa Tangazo la Serikali Na. 159/2003.

Sheria hii ina madhumuni yafuatayo:-

* Kulinda watu wote walio chini ya umri wa miaka 18 na wale wote wasiovuta sigara dhidi ya vishawishi vya matumizi ya bidhaa za tumbaku.

* Kuwalinda wasiovuta sigara dhidi ya moshi wa sigara;
* Kutoa taarifa za kutosha kuhusu athari za matumizi ya tumbaku;

* Kuhakikisha kwamba bidhaa za tumbaku zinazingatia viwango vya utengenezaji;

* Kujenga mazingira ya kuwa na jamii isiyovuta sigara kwa watu wa aina zote.

Utekelezaji wa sheria hii unasimamiwa na Kamati ya Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku iliyoundwa na Waziri wa Afya.

(b) Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12 cha Sheria ya Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku, kinazuia kuvuta sigara au kutumia bidhaa yoyote ya Tumbaku katika maeneo yote ya umma kama ifuatavyo:

* Vituo vya kutolea huduma za afya na tiba;
* Maktaba;
* Sehemu ya kuabudia;
* Kwenye vyombo vya usafiri vya angani, ardhini na majini;
* Majengo yanayotumiwa kwa mikutano, mihadhara, michezo, burudani, masoko, maduka na sehemu zote zenye mikusanyiko ya watu;
* Wale wote watakaokiuka sheria hii wanaweza kupigwa faini ya shilingi laki tano au kifungo cha miaka 3 jela au adhabu zote mbili yaani kifungo na faini.

(c) Mheshimiwa Spika, sheria hii iko kimya juu ya masuala ya fidia kwa walioathirika na bidhaa za Tumbaku. Hata hivyo endapo mtu ataathirika kiafya na anaamini kuwa athari

alizopata zinatokana na kuvutishwa moshi wa tumbaku katika maeneo yaliyokatazwa anaweza kufungua kesi ya madai ya fidia kwa kuzingatia taratibu za kesi za madai zilizopo kisheria.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Je, katika eneo la Bunge hili ni sehemu gani imetengwa kwa Wabunge wanaopenda kuvuta sigara? *(Makofi/Kicheko)*

Pili, sigara zinazoingizwa kutoka nje zinazingatia kwa kiasi gani masharti ya uvutaji sigara kama inavyozingatia Kampuni ya Sigara *(TCC)* hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilisema maeneo ambayo yamekatazwa watu kuvuta sigara. Sikuwa nimezungumzia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hivyo ninachotaka kusema hapa ni kwamba kila eneo lenye mkusanyiko wa watu litakuwa haliruhusiwi kuvuta sigara iwe nje ya Bunge au ndani ya Bunge. Lakini kama mtu ni mvutaji na anahitaji kufanya hivyo kwa sasa kwa sababu Bunge halijatenga eneo maalum ni vyema akahakikisha anafanya hivyo pale ambapo hakuna watu wengine ambao wataathirika na moshi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la masharti aliyowekewa sigara zinazotoka nje ya nchi. Nataka niseme kwam ba utaratibu wa *quality control* upo ndiyo maana sheria hii inazungumzia viwango kwa hivyo bila shaka sigara zinazotoka nje ya nchi vile vile zinatakiwa zikidhi viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria. Nafahamu *TBS* wanafanya kazi hiyo na vile vile hii Kamati iliyoundwa ya Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku itawajibika kwa kazi hiyo.

**SPIKA:** Jibu la nyongeza ni kwamba ukumbi wa Bunge na Maofisi yote ya Bunge yamekatazwa kuvuta sigara na ziko mashine ambazo moshi ukizifikia tu zinapiga kengele jengo zima la Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Makampuni makubwa ya Kimataifa yanayotengeneza sigara duniani yamefika mahali yanakosa masoko nchini kwao kwa sababu ya sheria kubwa, kali na ngumu zilizowekwa na Serikali mbalimbali duniani. Na kwa kuwa sasa yale Makampuni yamehamia nchi hizi za kwetu na hasa hapa Tanzania na wanawatumia vijana wadogo, wasichana, wavulana katika matangazo yao ya *billboard* na kuwafanya vijana wengi sana nchi hii kuanza kupenda na kuwa na hamu ya kuvuta sigara.

Je, Serikali itakubaliana na mimi sasa kwamba wakati umefika wa kupiga marufuku kabisa matangazo yote ya sigara na *billboard* zinazotokea katika nchi hii ili kunusuru nchi hii na vijana wetu katika uvutaji wa sigara? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, sheria tuliyokuwa nayo sasa hivi haikatazi matangazo ya biashara ya sigara. Isipokuwa yameweka utaratibu ambao ni lazima

utekelezwe nao ni kuonyesha katika lile tangazo wanaloliweka lazima wawe wameandika kwa maandishi makubwa athari zinazosababishwa na matumizi ya sigara.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda niongezee kwa kusema kwamba wazo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri na tutalizingatia. *(Makofi)*

Na. 108

**Elimu ya Awali**

**MHE. MARIA D. WATONDOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Elimu ya Awali inatakiwa itolewe katika kila Shule ya Msingi nchini; na kwa kuwa, elimu hiyo inampatia msingi mzuri mtoto anayetakiwa kuanza darasa la kwanza:-

(a) Je, katika Mkoa wa Lindi, ni Shule za Msingi ngapi zenye madarasa ya Elimu ya Awali?

(b) Kwa kuwa shule nyingi za msingi zina upungufu wa Walimu. Je, kwa nini Walimu waongezewe mzigo wa kufundisha Elimu ya Awali badala ya kada ya Walimu wa kutoa elimu hiyo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Lindi kuna Shule za Msingi 202, kati ya 398, zenye madarasa ya Elimu ya Awali kama ifuatavyo:-

| WILAYA | IDADI YA SHULE | ZENYE MADARASA YA AWALI |
|---|---|---|
| Kilwa | 86 | 46 |
| Lindi (M) | 104 | 70 |
| Liwale | 45 | 22 |
| Nachingwea | 82 | 13 |
| Ruangwa | 68 | 37 |
| **Jumla** | **398** | **202** |

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kuanzia mwaka 2005 imerekebisha na kuiboresha mihtasari ya Elimu ya Ualimu inayotumika kwa vyuo vyote ili kuhakikisha kila anayeingia chuoni yaani kila Mwalimu mtarajali katika ngazi ya cheti pamoja na masomo mengine anapata masomo ya Malezi ya Elimu ya Awali na mbinu za kufundisha Elimu ya Msingi na ya Awali kwa lengo la kuwa na Walimu wa kutosha wa kufundisha Elimu ya Msingi na ya Awali kwa pamoja.

Kupitia utekelezaji wa MMEM mafunzo haya yameanza na wanachuo 10,000 mwaka huu wa 2005 na 9,000 mwaka 2006 na yataendelea kulingana na mahitaji ya Walimu wa ngazi hiyo. Aidha, Walimu wengine waliopo kazini watapewa mafunzo hayo kwa njia ya mafunzo kazini.

Hatua hizo zitasaidia sana kupunguza mzigo kwa Walimu wanaofundisha madarasa ya awali. Kwa kuwa Elimu ya Awali ni sehemu ya Elimu ya Msingi, hakuna sababu ya kuwa na kada tofauti ya Walimu wa kufundisha elimu hiyo.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nimeshtushwa kuona katika takwimu zake Wilaya ya Lindi Vijijini haionekani kama ina Shule za Msingi wala Shule za Awali. Je, Shule za Msingi za Wilaya ya Lindi Vijijini ni ngapi na shule ngapi zina Shule za Awali?

Pili, kwa kuwa ameeleza kwamba mafunzo haya yameanza mwaka 2005 kwa kuandaa walimu 10,000 ambao watakuwa pia na taaluma ya Elimu ya Awali. Je, kwa hivi sasa vituo hivi ambavyo madarasa haya ambayo yako katika shule hizi yanafundishwa na walimu wa kada zipi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba radhi katika jibu nililotoa takwimu za Lindi Vijijini hazikuwemo. Nitampatia majibu kwa ajili ya Wilaya hiyo. Naomba radhi kwamba kumekuwa na *omission* katika kuandaa jibu hili.

Kuhusu suala la pili, kwamba hivi sasa ni Walimu wepi wanaofundisha Elimu ya Awali. Ni Walimu wale wale walio katika Shule za Msingi.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika ni hapa kwetu tu ambapo Elimu ya Msingi inaanza na mtoto wa umri wa miaka 7. Katika nchi nikisema hapa kwetu ninamaanisha ni hapa kwetu Tanzania. Afrika na katika nchi zinazoendelea, wenzetu huko Ulaya na Amerika ya Kaskazini Elimu ya Msingi huanza na mtoto wa miaka 5. Kwa hiyo, hawa Walimu waliopewa mafunzo ili wakafundishe katika Shule za Msingi wanao uwezo wa kuweza kufundisha Elimu ya Awali.

Tunachofanya sasa ni kuwaona vizuri zaidi namna ya ku-*handle* watoto wa umri wa chini ya miaka 7 ambao walikuwa hawana uzoefu wa kuwafundisha katika miaka ya nyuma. Ndiyo maana sasa kila Mwalimu anayepewa mafunzo ya kufundisha Elimu ya Msingi, itakuwa ni pamoja na kufundisha watoto walio katika madarasa ya Elimu ya Awali wa miaka 5 na 6.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Kwa kuwa Elimu ya Awali inahitaji mtoto awe ameandaliwa na kwa kuwa watoto wengi ambao hawajafikisha miaka 5 vijijini hawaendi kwenye vituo vya Chekechea. Je, Wizara ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba itashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii

kuhakikisha kwamba hawa watoto kabla hawajaenda Shule ya Awali wametoka kwenye vituo vya Chekechea?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, ni kawaida ndani ya Serikali kuna ushirikiano kati ya Wizara na Wizara. Lakini nilipenda nimfahamishe kwamba wale Chekechea nadhani hawako katika Wizara aliyoitaja ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Jinsia. Bado wako kwenye Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Nafikiri wote huwa tunadhani hivyo lakini bado wako kwenye Wizara hiyo. Nadhani hili jambo litakapotazamwa upya katika muundo wa Serikali huenda ndipo watahamishiwa kwenye Wizara anayozungumza. Lakini ni kweli panahitaji ushirikiano na ni kweli inapendeza sana na inafaa sana kama mtoto kabla ya kuingia katika Elimu ya Awali awe amepitia katika mafunzo ya shule ya watoto wadogo katika Chekechea. Jambo hili inabidi litazamwe kwa pamoja wakati muundo wa Serikali unatazamwa upya.

Na. 109

**Ujenzi wa Shule za Sekondari Geita**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kuendeleza Elimu ya Sekondari Wilaya ya Geita imepanga na kuamua kufungua shule nyingi ikilinganishwa na wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na kwa kuwa, mwaka huu jumla ya wanafunzi 8,678 wanategemea kumaliza Elimu ya Msingi na utaratibu wa Serikali ni kwamba asilimia 35 ya wanafunzi wote ndio wanaotegemewa kujiunga na Sekondari kwa maana ya wanafunzi 3,037 watakaochaguliwa na kwa kuwa Wilaya hiyo haikuwa na Shule za Sekondari kabisa na wananchi wamejitolea kujenga shule hizo kwa nguvu zao wenyewe:-

(a) Je, Serikali itawasaidiaje wananchi wa Geita ambao wanategemea kufungua Shule za Sekondari zaidi ya 12 kwa mwaka huu?

(b) Kwa kuwa, wananchi wamejitolea kujenga shule na Serikali ikawapatia madarasa 34 Wilaya zile ambazo wananchi wake hawakujitolea lakini wamepewa fedha nyingi. Je, Serikali haioni kuwa imezibagua Wilaya nyingine?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inachangia kwenye nguvu za wananchi kwa kutoa ruzuku ya maendeleo ya shilingi 7,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa darasa na shilingi 9,000,000/= kwa ujenzi wa nyumba ya Mwalimu. Wilaya ya Geita imeshapewa shilingi 238,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 34. Aidha, jumla ya shilingi 117,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 13 za walimu, zitakazojengwa kwenye shule za wananchi zilizopo zilizokuwa zimesajiliwa hadi Desemba, 2004. Kwa mgao huo wa madarasa 34, Wilaya ya Geita itaweza

kufikia lengo la Kitaifa la asilimia 35 ya wanafunzi wa darasa la saba kuingia Kidato cha Kwanza.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa ruzuku ya ujenzi wa madarasa na nyumba za Walimu kuchangia kwenye nguvu za wananchi. Lengo la Serikali Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya la mwaka wa kwanza wa MMES ni kupeleka asilimia 35 ya wanafunzi wa darasa la saba wa 2004 kuingia Kidato cha Kwanza mwaka 2005. Kwa hiyo, mgawanyo wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa kwa kila Wilaya umezingatia lengo hilo. Kwa msingi huo hakuna Wilaya iliyobaguliwa na Serikali katika kutoa ruzuku ya Maendeleo. Kwa sababu mgao umefanywa kwa kutumia vigezo vya usawa.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya ya Geita imetimiza Ilani ya Uchaguzi kwa kujenga shule kila Kata kwa Kata 33. Mwaka jana 2004 ilifungua shule saba (7), mwaka huu 2005 imeshafungua jumla ya shule 17.

Je, Serikali inasemaje juu ya kupeleka Walimu katika shule hizo ambazo sasa hivi hazina Walimu?

Pili, kwa kuwa shule hizo sasa hivi zina Walimu Wanafunzi ambao wamemaliza Kidato cha Sita na bado wanajitolea. Je, Serikali inasemaje juu ya kuajiri wale vijana wakawa wanapelekwa awamu kwa awamu kwenda chuoni ili waweze kuendeleza elimu katika Wilaya ya Geita? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza Serikali inasemaje kuhusu Walimu baada ya Wilaya ya Geita kufungua shule mpya 17. Kwanza napenda kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Wizara yangu niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Wilaya ya Geita kwa kuanzisha Shule za Sekondari 17 katika mwaka mmoja. Miaka michache iliyopita ilikuwa ni jambo lisilotegemewa kabisa katika Wilaya ya Geita. *(Makofi)*

Kuhusu sasa Walimu na hili nafikiri linahusu nchi nzima. Ni wazi kabisa kwamba kwa mfumko mkubwa uliotokea mwaka huu wa kufungua Shule za Sekondari tutakuwa na kipindi cha upungufu mkubwa wa Walimu kwa sababu hata kiutawala Wizara haijawahi kuwa na jukumu la kuajiri na kuwapata Walimu wengi kiasi hiki kutokana na *speed* inayotokana na mpango huu wa maendeleo wa Elimu ya Sekondari. Kwa hiyo, naomba kuchukua nafasi hii kutoa ushauri ufuatao. Kwamba ndani ya kila Wilaya katika Shule za Msingi tunao Walimu wenye *diploma.* Walimu wale wenye *diploma* za Ualimu wanao uwezo wa kuanza kufundisha katika Kidato cha Kwanza na cha Pili. Kwa hiyo, nashauri na naidhinisha kwamba pale ambapo imefunguliwa Shule ya Sekondari wapangwe walimu walio na *diploma,* walio ndani ya Wilaya ili mafunzo ya Elimu ya Sekondari yaanze kuendelea wakati Wizara tunafanya mpango wa mchakato wa kuajiri Walimu wa Shule hizo za Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Walimu ambao wameajiriwa hawana vyeti lakini wana elimu ya Kidato cha Sita. Wizara inao mpango wa Walimu hao kuwaajiri ili waingizwe katika mpango wa Wizara baadaye wapelekwe kwenye mafunzo ya Ualimu. Kwa hiyo, tunaomba Maafisa Elimu wa Wilaya wawaorodheshe Walimu hao ambao tayari ni *Ex-Form Six* lakini wawe na sifa za kufaulu angalau katika daraja la III kwenda juu ili tuweze kuwaajiri katika programu hiyo maalum ya kuziba pengo wakati hatujawa na Walimu wa kutosha na waingizwe katika ratiba ya kupelekwa kusomea Ualimu wa *diploma* kwa kadri nafasi zinavyopatikana. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa huko nyuma kuna Mikoa na Wilaya ambazo zimejengewa Shule za Sekondari na Serikali kabla na baada ya uhuru. Na kwa kuwa kwa sasa hivi ziko Wilaya kama vile Geita tunajenga sisi wenyewe kwa nguvu zetu sisi wenyewe na kuna tatizo la Walimu. Je, Serikali sasa katika mpango wa kuajiri Walimu ambao kuna taarifa kwamba wanataka kuajiri Walimu 4,000 itafikiria kwanza shule hizi za Kata zinazojengwa na wananchi wenyewe kwanza ili tuweze kwenda pamoja na walioanza siku nyingi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimkumbushe kwamba shule hizi zinazojengwa na wananchi nazo ni za Serikali. Yaani ni shule za Serikali zinazojengwa na wananchi.

Kwa hiyo, katika upangaji wa Walimu Serikali inawajibika kwa usawa kabisa kwa shule zile ambazo zilijengwa na Serikali au zilikuwa za Madhehebu zikakabidhiwa kwa Serikali uwajibikaji katika suala la Walimu ni kwa usawa kabisa. Napenda nikiri kwamba mpaka sasa hali hiyo haijitokezi kwa sababu tunapopanga Walimu katika shule nyingi zilizojengwa na wananchi Walimu wanakwepa kwenda. Unampanga Mwalimu aende kwenye shule lakini wanaulizia kuna nyumba ya Mwalimu, kuna umeme, kuna maji katika nyumba hiyo. Wakijua hakuna wanapiga chenga. Wengine wanakwenda Dar es Salaam tu wanafanya *moonlighting* ama wanakwenda kuajiriwa kwenye shule zisizo za Serikali.

Kwa hiyo, napenda nilifahamishe Bunge hili na hasa Waheshimiwa Wabunge kwamba ili tufanikiwe kwa ukamilifu katika kupanga Walimu kwa usawa tujitahidi kujenga nyumba za Walimu sambamba na madarasa tunayoyajenga kwa ajili ya shule zetu.

Serikali ndiyo maana katika Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari imepanga kutoa ruzuku ya maendeleo kwa ujenzi wa nyumba 1,000 za Walimu kila mwaka kwa miaka mitatu mfululizo. Ninachotoa wito ni usimamiaji ili tuweze kuifanya kazi hii kwa ufanisi. Ukiwa una nyumba iliyo nzuri, ina maji, ina umeme elewa dhahiri hicho ni kivutio kikubwa cha kumpata Mwalimu ambaye atakaa pale na kufanya mahali pake pa kudumu. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Waziri kuhusiana na suala la Walimu na Shule za Sekondari zinazojengwa, suala la wanafunzi kuingia kwenye Kidato cha Kwanza limepanuka sana nchi

nzima. Hata leo kwenye taarifa ya habari nimesikia viongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro wakiomba wanafunzi wengi zaidi wazidi kuingizwa katika Shule za Sekondari. Sasa swali ni kwamba kwa hali ya Mwanza kuna maeneo mengi ambako tumejenga Shule za Sekondari kwa kuweka nafasi kuanzia mikondo miwili miwili kwenye kila shule. Lakini kufuatana na msongamano tungependa mikondo iwe minne minne au zaidi.

Mheshimiwaa Spika, je, Wizara inaweza kusaidiaje tuweze kufikia lengo hilo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika mpango huu wa MMES ruzuku ya maendeleo iliyotolewa siyo kwa ajili ya shule mpya zinazojengwa na wananchi ni ya madarasa mawili na ndiyo maana programu ile iliyopangwa ni ya kufungua shule hizi zikiwa na mikondo miwili. Lakini kama ipo shule ambayo kutokana na ruzuku ya maendeleo ya kujengea madarasa mawili nguvu za wananchi zimechangia kwa kiwango kikubwa na wamejenga madarasa manne au matano kila tunapopewa taarifa hiyo tunaruhusu shule ifunguliwe ya mikondo minne.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda niseme wazi kabisa kama kuna shule yoyote ambayo madarasa yapo kibali kinatolewa kuweza kufungua iwe ya mikondo minne kuanzia sasa. *(Makofi)*

Na. 110

**Magari Yanayofaa Katika Kupambana na Ujambazi**

**MHE. MOSSY S. MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa majambazi wanatumia magari yaendayo kwa kasi aina ya *Landcruiser* na askari wetu bado wanatumia magari madogo katika *patrol*:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha magari ya askari hao ili yakidhi ushindani katika kupambana na majambazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa majambazi yamekuwa yakitumia mbinu mbalimbali za hali ya juu kufanikisha ujambazi wao ikiwa ni pamoja na kutumia magari yaendayo kasi kama *Landcruiser.*

Kwa muda mrefu Polisi wamekuwa wakipambana na majambazi hayo kwa shida kwa kuwa magari mengi yanayotumika kwa *patrol* ni machakavu na hayana mwendo wa kasi kama yale yanayotumiwa na majambazi. Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali imeazimia kuwapa mafunzo ya kisasa na vitendea kazi bora zaidi askari wake katika kukabiliana na ujambazi ikiwa ni pamoja na kutoa magari yaendayo kasi.

Mheshimiwa Spika, juhudi zinazofanywa na Wizara yangu hivi sasa ni kuimarisha usafiri katika ngazi ya Mkoa na Wilaya. Kwa mwaka huu wa fedha yaani kati ya sasa mpaka mwezi Juni, 2005 magari 215 aina ya *Landrover* yatanunuliwa kwa ajili ya Makamanda wa Polisi wa Wilaya *(OCDs), OC* - Saidizi na vikosi vya *FFU.* Aidha, jitihada za kununua magari yaendayo kasi zimeanza pia. Kwa kuanzia, Serikali hivi karibuni imenunua magari aina ya *Land cruiser* kwa Makamanda wa Polisi wa Mikoa yote 26 hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hii Serikali pia imenunua na kusambaza katika Mikoa yote vifaa vya kisasa vya mawasiliano.

Aidha, Serikali itaendelea kununua magari yaendayo kasi kwa Mikoa na Wilaya hatua kwa hatua hadi Mikoa na Wilaya zote zitakapokuwa zimepata magari hayo. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wavute subira.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa jibu la Mheshimiwa Waziri limezungumza kwamba watanunua magari kwa ajili ya Ma-*OCDs* na kwa askari wengine katika maeneo hasa ya Wilayani. Lakini ukizingatia hali ilivyo katika Tarafa na baadhi ya vituo vya polisi katika maeneo vina matatizo makubwa sana ya usafiri hata wengine wanakosa hata baiskeli hawana. Je, wana mkakati gani nao wa kuwapatia vyombo vya usafiri hasa maeneo yale ambayo ni ya hatari kama kule Kalalani ambapo kuna ujambazi wa watu wanaowakung'uta watu njiani wanapokwenda kuchimba madini na maeneo mengine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera Mbunge wa Korogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika swali langu la msingi kwamba matatizo ya usafiri yanalikabili Jeshi la Polisi, katika ngazi mbalimbali. Kuanzia ngazi ya mkoa mpaka ngazi za chini kabisa. Kwa hiyo, sasa hivi tumeanza kwa kutatua katika ngazi ya Mikoa na ngazi ya Wilaya. Sasa baada ya hapo katika Bajeti zetu zijazo tutaanza kuzingatia vile vile matatizo katika ngazi za chini hasa katika vituo vya tarafa na vituo ambavyo viko mbali sana kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Hata hivyo kwa sababu Ma-*OCD* watapata magari mapya, yale wanayotumia sasa ambayo ni machakavu tutatenga fedha yatatengenezwa yawe imara na yataanza kutelemshwa chini ili wale wasaidizi wao wa chini kwenye tarafa na kadhalika na wenyewe wapate vyombo vya usafiri. *(Makofi)*

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hapa Tanzania sasa hivi majambazi wameona ujambazi ni ajira *(professional)* na kwa kuwa kila tunavyofanya mbinu wanaona hazifai wao ni zaidi.Je, Serikali iko tayari kuleta Muswada wa Sheria hapa Bungeni, ili majambazi wakishakamatwa wapigwe risasi hadharani, *(firing squad)* ili wengine wanaotaka kujifunza kazi hiyo na ujinga huo waache na taifa letu litulie liendelee na kazi ya kulijenga taifa zuri zaidi? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meja Mstaafu Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sasa hivi ujambazi siyo Tanzania tu kwa kweli sasa ni tatizo la dunia nzima ujambazi umeongezeka na wanatumia mbinu za hali juu na wenyewe wanatumia sayansi na teknolojia hii hii, jinsi inavyopanda na wenyewe wanaitumia hiyo hiyo na kwamba na sisi katika vyombo vya dola tunachojaribu kufanya na sisi ni kuongeza utalaam wa askari wetu kupambana nao, kwa maana ya vitendea kazi, vifaa vya mawasiliano na kadhalika ili kuweza kupambana na mbinu mpya za hawa majambazi.

Sasa kuhusu suala la tulete sheria ndani ya Bunge hili ili kila jambazi apigwe risasi, kuna baadhi ya nchi nasikia kule Nigeria ujambazi ulizidi sana waliwahi kujaribu hiyo njia, basi wakaona ili kukomesha wizi watunge sheria hii sasa ya *firing squad.* Sasa inasemekana walipotunga sheria ile walipoanza kutekeleza, ujambazi ukazidi mara mbili. Kwa hiyo, pengine dawa si sheria anayosema Mheshimiwa Mbunge, dawa ni kutazama chanzo cha ujambazi katika jamii yetu na ujambazi mwingi kabisa chanzo chake ukitafuta uko katika uchumi. Nadhani tukiboresha uchumi wale ambao hawana kazi wakapata ajira na tukaimarisha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama tunaweza tukapunguza tatizo hili kuliko kujaribu hii sheria ya *firing squared. (Makofi/Kicheko)*

Na. 111

**Fedha na Vifaa Vinavyotolewa Kama Msaada kwa Tanzania**

**MHE. GWASSA A. SEBABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania imejaliwa kuwa na marafiki wengi mbalimbali ambao wanapenda maendeleo yetu ya Kiuchumi. Kisiasa, Kiutamaduni na Kijamii na kwa kuwa, kutokana na ukweli huo, nchi nyingi marafiki duniani zimekuwa zikitoa misaada ya fedha na vifaa kwa ajili ya kuisaidia Tanzania kutekeleza mipango yake ya maendeleo na hatimaye kuondoa umaskini:-

(a) Mheshimiwa Spika, je, ni nchi zipi kwa majina ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika kutoa misaada ya fedha na ni fedha kiasi gani kwa kila mwaka tangu mwaka 1996 hadi sasa na ziligawanywaje Kimkoa na Kiwilaya?

(b) Je, ni nchi zipi kwa majina zilitoa misaada na ni mangapi na ya yamegawanywa vipi Kimkoa na Kiwilaya?

(c) Je, ni vigezo gani vilivyotumika katika kugawa vifaa na fedha zilizotolewa kama msaada kwa Mikoa na Wilaya?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mbunge wa Ngara, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Tanzania imekuwa ikipokea misaada mbalimbali kutoka kwa nchi marafiki kote duniani. Misaada hii imekuwa ikigharamia shughuli mbalimbali za maendeleo hapa nchini. Shughuli hizi ikijumuisha miradi huwa zinatekelezwa na Wizara/Mikoa/Wilaya husika. Misaada hiyo huelekezwa moja kwa moja kwenye Wizara/Mkoa/Wilaya inayotekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, miradi inayotekelezwa na Wizara huwa ni ya Kitaifa na hivyo fedha zake huonyeshwa katika Bajeti ya Wizara husika. Miradi inayotekelezwa na Mkoa/Wilaya, fedha zake hupelekwa moja kwa moja kwa watekelezaji wa mradi husika yaani Mkoa au Wilaya. Misaada ya fedha ambayo hupitia Mfuko wa Serikali *(Exchequer)* mara nyingi imekuwa ya kusaidia Bajeti ya Serikali na hupelekwa kwenye Wizara/Mkoa/Wilaya kulingana na Bajeti zao kama zilivyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha msaada wa vifaa kwa kawaida huwa umeonyeshwa katika ujumla wa thamani wa mradi husika. Hata hivyo kama nchi rafiki imetoa msaada wa vifaa peke yake, basi msaada huo huthamanishwa kwa fedha na hupelekwa/kuelekezwa kwenye Wizara/Mkoa/Wilaya kwa utaratibu ule ule yaani nilioueleza hapo awali. Hivyo, takwimu zilizopo hazitofautishi misaada ya kifedha na vifaa bali zinaonyesha ujumla wa misaada katika fedha *(Monetary Value)*.

Mheshimiwa Spika, ni vyema ieleweke kuwa kumekuwepo na ugumu wa kupata takwimu za misaada ya wahisani inayopokelewa moja kwa moja na wahisani hao. Hata hivyo, Serikali imeshaanza kuchukua hatua madhubuti ikishirikiana na wafadhili kuhusu ukusanyaji wa takwimu za misaada ya aina hii. Mfano, mwaka 2001 Wizara ya Fedha ilitoa Waraka kwa wafadhili wote, Wizara, Mikoa, Wilaya na mameneja wa miradi yote ukionyesha jinsi ya kutoa taarifa za takwimu za fedha zinazokwenda moja kwa moja kwenye miradi/Mkoa/Wilaya bila kupitia Mfuko wa Serikali Kuu. Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Angus Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, (a) & (b)kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa na Wizara ya Fedha, ikishirikiana na wafadhili tangu mwaka wa fedha 1996/97 hadi Desemba, 2004, Tanzania imepokea misaada inayofikia jumla ya shs. 2,519.148 bilioni kutoka kwa nchi 19 marafiki. Nchi hizo ni Australia, Ubelgiji, Canada, Denmark, Uingereza, Finland, Ufaransa, Ujerumani, Ireland, Italia, Japan, Uholanzi, Norway, Poland, China, Hispania, Sweden, Switzerland na Marekani. *(Makofi)*

( c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kueleza hapo mwanzo vigezo vinavyotumika kugawa misaada hii ni kwa mujibu wa sera za Bajeti ya Serikali kwa jinsi ilivyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Aidha, mpango wa kuondoa umaskini *(PRS)* na mpango wa muda wa kati wa matumizi *(MTEF)* ndio dira ya uandaaji wa miradi inayogharamiwa na fedha za nje na zile za ndani.

Mheshimiwa Spika, ili kuokoa muda kwa mujibu wa Kanuni za kujibu maswali Bungeni, nitagawa kiambatisho kwa Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kinachoonyesha nchi mfadhili, mwaka na thamani ya ufadhili tangu mwaka 1996 hadi Desemba, 2004. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini hata hivyo naomba uniruhusu kuuliza maswali mawili.

(a) Kwa kuwa inajulikana wazi kwamba Mikoa ya Magharibi, Mikoa ya Kusini, imesahaulika sana katika maendeleo yake. Je, si vizuri sasa misaada ya namna hii ikaelekezwa maeneo hayo kwa sababu inawezekana inavyokuja, inakuja haina masharti maalum? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa Mikoa hiyo niliyoitaja ukiwemo mkoa wa Kagera na Wilaya ya Ngara, haina wawekezaji na ni kwa sababu ya kutokuwa na miundo mbinu ambayo inaweza kuwavutia wawekezaji kuweza kuelekea katika maeneo hayo. Je, Serikali ina makusudi gani kuweza kuhakikisha kwamba Mikoa hii inaendelea sambamba na Mikoa ya Mashariki, Mikoa ya Kaskazini na Mikoa ya Kusini milimani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Gwassa Sebabili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Suala la mgao wa fedha za bajeti miongoni mwa Mikoa tulilijadili hapa wakati wa Bajeti ya mwezi Juni, Julai, Agosti mwaka jana. Tulionyesha kwamba kuanzia mwaka huu wa bajeti mwaka unaoishia mwezi Juni mwaka huu, tumekuwa tukitumia formula ambayo ilipendekezwa na wataalam kuonyesha jinsi Mikoa mbalimbali na Wilaya mbalimbali zinavyoweza kupendelewa katika mgao wa bajeti. Kwa hiyo, tumaini langu ni kwamba formula hii tukiendelea kuiboresha na tukiendelea kutumia njia nyingine za misaada ambayo kwa kawaida huenda moja kwa moja Vijijini kama ile ya *TASAF* ambayo tumekuwa tukiizungumza hapa kwenye semina wiki hii, nina matumaini makubwa kabisa kwamba tofauti zilizoko baini ya Mikoa katika mgao wa bajeti zitatoweka. *(Makofi)*

Na. 112

**Udhibiti wa Wizi Katika Mabenki**

**MHE. MARIAM S. MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kazi mojawapo ya vyombo vya fedha kama vile Benki ni pamoja na kutunza fedha za akiba za wateja wake na kuwapa huduma wateja hao wanapohitaji kuchukua fedha zao kutoka katika Benki husika na kwa kuwa, akiba za wateja ni siri kati ya Benki na mteja wake hasa wakati wa kuweka na kuchukua fedha na mteja asingependa aonekane na mtu mwingine wakati wa zoezi hilo la kuweka na kuchukua fedha linapofanyika kwa kuhofia kuporwa fedha zake kwani hakuna uhakika kuwa watu wote wanaoingia Benki ni wema au ni wahalifu wanaotaka kujua siri za wateja wanaofika Benki kuchukua fedha zao:-

(a) Je, ni lini Serikali itaviagiza vyombo vya fedha (Benki) kutengeneza vyumba vya siri mahali pa mteja kuweka au kuchukuliwa fedha zake?

(b) Je, kuna utata gani katika kutekeleza jambo hilo?

(c) Je, Serikali imeviandaa vyombo vya fedha katika kuwalipa mishahara watumishi wa Serikali hasa walimu kupitia Benki ili walimu wengi wasije kulala mijini wakisubiria mishahara yao kutokana na kuwepo kwa watumishi wengi wanaolipwa mishahara kupitia Benki?

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mbunge Viti Maalum, napenda kuoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa biashara ya Mabenki iliwekwa huru mwaka 1991 ilipopitishwa Sheria ya Usimamizi wa Mabenki na Vyombo vya Fedha ya mwaka 1991 *(The Banking and Financial Institutions Act, 1991)* na hivyo biashara hiyo kuendeshwa kwa ufanisi, usalama na ushindani katika soko huria bila kuingiliwa na Serikali. Aidha, kifungu 36 (i) cha Sheria hiyo kinawataka Wafanyakazi wa Mabenki kutunza siri za wateja zinazohusiana na amana zao pamoja na taarifa za shughuli za kibenki.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu kama chombo cha Serikali kinachosimamia shughuli zote za Mabenki, kinahakikisha kuwa Benki na Taasisi za fedha, kabla ya kuanza shughuli za kibenki mahali popote pana usalama wa kutosha kwa wateja wake wanapokuwa ndani ya Benki.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wafadhili tangu mwaka 2001 ilianzisha mradi wa kutathmini mwenendo na mapungufu ya vyombo vya fedha *(Financial Sector Aassessment Study)* ili kubaini kasoro zilizopo na kuvisaidia viweze kufanya kazi vizuri. Mradi huo umesaidia kurekebisha kasoro katika endeshaji wa Mabenki.

Aidha Benki Kuu imetoa miongozo mbalimbali kwa Mabenki na vyombo vya fedha ikiwa ni pamoja na unaozitaka Benki kufanya malipo kupitia katika mtandao wa malipo unaojulikana kama *Tanzania Inter Bank Setting System (TISS)* kwa lengo la kuongeza kasi ya Mabenki kufanya malipo kwa teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mbunge Viti maalum, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa wateja wanaoweka au kuchukua fedha nyingi benki na taasisi za fedha zina utaratibu wa kutumia vyumba maalum ambavyo vimetengwa kwa ajili ya huduma hiyo. Aidha katika siku za hivi karibuni Benki nyingi zimeanzishwa mtandao aina ya *ATM* unaowawezesha wateja kuchukua fedha wakiwa nje ya majengo ya Benki, lakini wakiwa katika vyumba maalum vinavyolindwa na askari wenye silaha kwa saa 24. Wateja hao wanaweza kuchukua fedha zao kwa usalama kwa kujiwekea wakati wa siri wa kwenda Benki. Mtindo huu umewafurahisha wateja wengi na unatumika sana pale ulipokwisha anza. Aidha baadhi ya Benki zimeanza kutumia pia utaratibu wa kadi maalum kulipia huduma na hivyo kuondoa ulazima wa kubeba fedha nyingi toka Benki. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wananchi wanashauriwa kuongeza matumizi ya hundi au kadi maalum za malipo badala ya fedha taslimu katika kufanya malipo. Aidha Serikali inahimiza wananchi wakiwemo walimu, kuanzisha vyama vyao vya kuweka na kukopa au Benki jamii kwa shughuli zao ndogo ndogo za kibenki ili waondokane na usumbufu na hatari ya wanyang'anyi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imeingia mkataba na *National Micro Finance Bank (NMB)* kufanya malipo kwa watumishi wake wote bila kujali kuwa wana akaunti katika Benki hiyo au katika Mabenki mengine. Pale ambapo watumishi wake wana akaunti nje ya Benki hiyo ya *National Micro Finance Bank* huwalipa kupitia Benki hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu matatizo ya hapa na pale kuhusu mishahara kulipwa kupitia Mabenki, likiwepo la mazoea ya kutaka walipwe dirishani hapo hapo kazini. Matatizo hasa ni ucheleweshо wa baadhi ya Wizara na Halmashauri kuchelewa kupeleka hundi au orodha za malipo *NMB* na *NMB* yenyewe kukosa nafasi kwenye baadhi ya matawi na kusababisha msongamano wa walipwaji. Suala hili litafikiriwa upya baada ya mkataba wa *NMB* kumalizika.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

(i) Mheshimiwa Waziri, mwenyewe kathibitisha kwamba bado kuna msongamano mkubwa wa Watumishi na hasa walimu wakati wa kuchukua mishahara. Je, ni kwa nini sasa Benki hizi hasa *NMB* isiongeze hata madirisha ya muda ili kuwezesha watumishi hawa kuchukua fedha zao kwa muda mfupi badala ya kutumia saa 8 mpaka saa 9 kwa siku moja?

(ii) Mheshimiwa Spika, naomba ili kuthibitisha majibu yake Mheshimiwa Waziri, atembelee hasa kipindi cha mishahara katika benki yetu ya *NMB* ya Dodoma ajionee mwenyewe ni jinsi gani watumishi hawa wanavyopata shida wakati wa kuchukua mishahara yao. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali (a) na (b) ya Mheshimiwa Mfaki, kama ifuatavyo:-

Sina haja ya kutembelea Benki hiyo, nafahamu kabisa kwamba kuna matatizo na nimesema kwenye jibu la msingi. Matatizo yenyewe yametokana na Benki ya *NMB* kutokuwa na vyumba vikubwa vya kuhudumia wageni katika matawi yao. Matawi yao ni finyu na vyumba vyake ni finyu. Pale Dar es Salaam imebidi wahamie matawi mengine, hata hapa Dodoma penyewe wamehama kwenye tawi la awali wakahamia kwenye jengo la CCM hapa Mjini. Kwa hiyo, wao wenyewe wanafahamu kwamba hawana nafasi. Nafikiri tatizo kubwa wala siyo *NMB* yenyewe kama nilivyosema tatizo kubwa ni wale wanaoandaa mishahara ya walimu yaani Wizara na Halmashauri husika, kuchelewesha orodha ya walipwaji kwa namna ambayo wiki ya kwanza ya mwezi ufuatao ndipo wanakwenda tarehe 1 au wiki moja kujaribu kufuata fedha zao. Mimi ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kwamba kila tarehe 8 ya kila mwezi Wizara ya Fedha, inapanga fedha za Idara zote na Halmashauri zote na yeyote anayelipwa na Serikali kila tarehe 8 au 9. Ikifika katikati ya kila mwezi *NMB* huwa wameshapokea hundi za kupeleka sasa kwenye Halmashauri na watumishi wanaolipwa kupitia kwao.

Tatizo ni kwamba *NMB* kwenye matawi hawezi kulipa mpaka Halmashauri husika iseme kwa mwezi huu hawa ndiyo watakaolipwa na fedha zao ni hizi na makato yao ni haya ndiyo walipe. Sasa baada ya kuchelewa watakapoingia walimu wote mathlani wa Dodoma Vijijini au Dodoma Mjini siku moja mahali pamoja ndiyo msongamano huo hutokea. Kwa hiyo, sina haja ya kutembelea nafahamu sana. Lakini narudia kwamba kama tatizo ni *NMB* wamezidiwa na *NMB* ina wenyewe ni juu yao kuangalia namna watakavyoweza kuhudumia wateja wao. Lakini mimi kama Serikali kwa kutegemea maamuzi yatakayofanywa naweza nikayatangaza hata kwenye Bajeti ijayo, sijaamua, nafikiria uwezekano wa kutoa *contract* hizi kwa *tender* ili Benki nyingi zenye matawi Vijijini ziweze kushinda *tender* hizo na kupewa ili tuwe na Benki nyingi zinazoweza kupewa fedha hizi watu wasambae kwenye matawi mbalimbali badala ya mahali pamoja. Lakini kama *NMB* wakionyesha umahiri zaidi kati ya sasa na Bajeti ijayo au mkataba wao utakapokwisha tuko tayari kuendelea nao.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea. Swali linalofuata kwa bahati mbaya, lilipelekwa Wizara isiyohusika. Masuala ya *IFAD* yako Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, muuliza swali ameomba kwamba lijibiwe siku nyingine na Waziri mhusika na mambo ya *IFAD.* Tutalitafutia nafasi siku nyingine. Tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Ujenzi.

Na. 114

**Barabara ya Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi na Ile ya Newala - Makonga - Kitangari - Mkwiti - Mtama**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipokuwa ikijibu swali Na. 197 hapo tarehe 09/07/2003 ilinieleza kwamba, barabara ya Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi yenye urefu wa kilomita 211 pamoja na ile ya Newala - Makonga - Kitangari hadi Mkwiti- Mtama haziwezi kuwekewa lami na badala yake zitafanyiwa matengenezo ya kawaida na majibu ambayo hayakuridhisha.

(a) Je, Serikali inaota sababu gani za msingi za kutoziwekea lami Barabara hizo na itakuwa tayari kupitia upya na kwa ufasaha swali langu la msingi ili kuelewa tatizo lilipo ambalo limenilazimu kuomba barabara hizo ziwekewe lami?

(b) Je, Serikali haioni kwamba wakulima wa Mkoa wa Mtwara wanapokosa barabara za lami kwa ajili ya kusafirishia mazao yao wanaelewa kwamba Serikali yao haiwatendei haki?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara za Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi (km 211) na Newala (Amkeni) - Kitangari - Mkwiti - Kinolombedo hadi Mtama (km. 78) ni barabara za Mkoa *(Regional Roads)* zinazohudumiwa na wakala wa Barabara *(TANROADS).* Wizara yangu

kupitia wakala wa Barabara *(TANROADS)* huzifanyia matengenezo ya kawaida; matengenezo ya dharura na matengenezo ya sehemu korofi za barabara hizi kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Fund).*

Hali ya barabara ya Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi kwa sasa, ukiondoa sehemu korofi kwenye Milima ya Nyambamba na Namaleche, ni nzuri kwa wastani na inapitika wakati wote bila matatizo. Katika mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, Wizara yangu kupitia wakala wa barabara *(TANROADS)* imepanga kuifanyia matengenezo barabara hii kwa gharama ya shilingi milioni 651.3.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2005 tayari kilomita 91 za barabara hii zimefanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya Shilingi milioni 46.071 pamoja na matengenezo ya muda maalum kilomita 6 ambayo yamekamilika kwa gharama ya shilingi milioni 89.661. Aidha, mkandarasi wa kufanya matengenezo ya muda maalum sehemu zenye lami kilomita 5.4 Milima ya Nyambamba na Namaleche kwa gharama ya shilingi milioni 391.184 amekwisha patikana na hivi sasa anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi kwa kutumia shilingi milioni 104 katika awamu ya kwanza.

Vile vile, maandalizi ya kuanza kazi ya matengenezo ya muda maalum kwa kuweka lami eneo la Masasi Mjini kilometa 3.5 yanaendelea na yatagharimu shilingi milioni 270 katika awamu ya kwanza. Kwa upande wa barabara ya Newala (Amkeni - Kitangari - Mkwiti-Kinolombedo hadi Mtama, hali ya barabara hii katika baadhi ya sehemu ni mbaya na hupitika kwa taabu katika maeneo korofi ya lengo, Kitangari na Mangombya. Hata hivyo hatua zimeanza kuchukuliwa kwa kuifanyia matengenezo barabara ili iweze kupitika wakati wote.

Aidha, barabara hiyo ilifanyiwa matengenezo ya dharura eneo la Makonga kilomita 5 katika mwaka wa fedha 2003/2004 kwa gharama ya shilingi milioni 37.084. Hivyo tatizo la magari kukwama eneo hilo kwa sababu ya mchanga limekwisha. Maeneo mengine yenye tatizo kama hilo yataendelea kufanyiwa kazi kadri fedha zitavyopatikana. Kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi wetu ni vigumu kwa sasa kuweza kujenga barabara ya Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi (km. 211) na ile ya Newala - Kitangari - Mkwiti - Mtama (km. 78) kwa kiwango cha lami kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge. Gharama za kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami inakadiriwa kuwa kiasi kisichopungua shilingi bilioni 86.7 ambazo kwa sasa hatuna, kwani kipaumbele hivi sasa ni kujenga barabara kuu kwanza kwa kiwango cha lami.

(b) Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ya Newala - Kitangari - Mtama ina hali mbaya. Lakini kama nilivyokwishaelezea katika sehemu (a) tayari hatua zimekwisha anza kuchukuliwa kuifanyia matengenezo barabara ya Newala - Kitangari - Mtama ili iweze kupitika wakati wote wa mwaka.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri. Nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Mtwara barabara alizozitaja nazifahamu na ni kweli kuna maeneo korofi.

(a) Kwa kuwa kitendo cha kutokuweka lami ni kuwapunguzia maendeleo wananchi wa Mtwara. Je, Waziri haoni kwamba ni kuwabagua wananchi hao kwa kutokuweka lami wakati nchi hii inaweka lami mpaka kwenye Makao Makuu ya Kata? *(Makofi)*

(b) Tatizo nililolisema ni barabara mbovu ambazo hazina hadhi katika Mkoa wa Mtwara ni pamoja na barabara ya Kibiti - Lindi. Mwanzoni mwa wiki mwezi huu wananchi wamekwama wiki mbili. Je, hawa watalipiwa fidia au Serikali inawatambua? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kutokuweka lami kwenye barabara za Mkoa Tanzania nzima *(Regional Roads)* si kuwabagua Watanzania wanaoishi sehemu hizo. Ni sera ya Wizara ya Ujenzi, kwamba kwa sasa hivi tuweze kuunganisha miji yote kwa kutumia barabara kuu kujenga barabara hizo kwa lami ifikapo mwaka 2012 ili Makao Makuu ya Mikoa yote iwe imeunganishwa kwa Barabara Kuu zenye lami. Kwa hiyo, siyo sera sasa hivi ya kutengeneza Barabara za Mkoa. Kama ni bahati nzuri tu kwamba Barabara Kuu inapita kwenye kata basi itapata lami. Lakini siyo lengo kwamba tunawabagua wananchi wa aina yoyote kwa sababu ya barabara ya lami. Hakuna fedha zinazotengwa kwa barabara za Mkoa kutiwa lami kwa makusudi.

(b) Waliokwama kwenye barabara ya Kibiti-Lindi je, tutawafidia? Kama tukianza kufidia watu wanaokwamba kwenye barabara mbovu basi hatutatengeneza hata barabara zenyewe, kwa sababu nchi yenyewe barabara nyingi ni za changarawe na za udongo. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba wakati wa mvua watu wengi tu watakwama na barabara nyingi tu zitafungwa. Kwa hiyo, tunaona kwamba suala hili la kufidia wanaokwama halitawezekana na nawaomba radhi sana wale ambao wanategemea kwamba tutawafidia kwamba hatuwezi kuwafidia na ninawapa pole wale waliokwama.

Na. 115

**Ukarabati wa Barabara ya Mkoa ya Mwembe - Mbaga**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa Waziri wa Ujenzi alipokuwa akijibu swali Na. 42 la barabara ya Mkoa ya Mwembe - Mbaga aliahidi kuwa barabara hiyo ilihitaji kufanyiwa ukarabati ili kuiokoa na kwa kuwa Naibu Waziri alitembelea barabara hiyo tarehe 18/3/2002 na kuona ubovu wake mkubwa:-

(a) Je, katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2002/2003 Serikali ilikuwa na mpango gani wa kuokoa barabara hiyo isife kwa kuikarabati kwa kiwango cha changarawe?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha nguvu za wananchi wa Same ili wachangie katika kupima na kuchimba kwa mikono yao wenyewe urefu wa kilometa 670 katika Milima ya Same?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia mifuko mingine ya fedha kama vile *STABEX,* Kilimo na kadhalika kwa ajili ya kukarabati barabara zingine za milima ya Upare (Same) ambapo mazao ya biashara kama kahawa hulimwa na kustawi kwa wingi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya barabara ya Mwembe hadi Mbaga siyo nzuri kwani haijawahi kupatiwa matengenezo yanayotosheleza kukidhi uharibifu halisi uliopo. Aina ya matengenezo yanayohitajika kufanyika ni yale ya ukarabati, kazi ambayo hugharimu fedha nyingi uwezo wa Bajeti ya Serikali kwa sasa.

Kutokana na gharama ya ukarabati kuwa kubwa kuliko Bajeti, ukarabati katika barabara hiyo haukufanyika katika mwaka wa fedha 2002/2003. Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hiyo katika nyanja za maendeleo na huduma za jamii, Wizara yangu imekuwa ikiifanyia matengenezo yafuatayo kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* Mkoa wa Kilimanjaro kama ifuatavyo:-

(i) Katika mwaka wa fedha 2002/2003, jumla ya shilingi milioni 40 zimetumika kwa kazi mbalimbali katika barabara hiyo, zikiwemo zile za kuimarisha kingo za barabara kwa kuweka *gabions* kujenga *drifts* na *scour checks* pamoja na uzibaji wa mifereji, uzibuaji wa mifereji wa kupitisha maji.

(ii) Katika mwaka wa fedha 2003/2004, barabara hii ilifanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi milioni 61.626 na matengenezo ya sehemu korofi yenye jumla ya urefu wa kilomita 5 yaliyojumuisha uwekaji wa changarawe kwenye sehemu hizo korofi kwa gharama ya shilingi milioni 30.2.

(iii) Katika mwaka huu wa fedha 2004/2005 barabara hiyo imetengewa jumla ya shilingi milioni 75 kwa ajili ya matengenezo maalum *(periodic maintenance)* na shilingi milioni 29.3 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida. Kazi za matengenezo haya zimeshaanza na ziko katika hatua za mwisho za utekelezaji.

Azma ya Wizara yangu ya kuipatia matengenezo yanayotosheleza barabara hii ipo pale pale. Jitihada za kupata fedha toka vyanzo mbalimbali vya mapato ya Serikali vikiwemo wahisani zinaendelea.

Aidha, wakati mikakati hiyo ya kupata fedha za kutosheleza matengenezo makubwa ya barabara yanaendelea, Wizara yangu itakuwa inaifanyia matengenezo ya kawaida na yale ya dharura barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningeomba kufahamu kwamba kwa sababu barabara hii inapita sehemu ambapo kuna ukulima wa zao la kahawa kwa kiasi kikubwa. Je, barabara hii haikupata fedha za *STABEX?*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, swali hili la barabara la *STABEX* lipo na ni tumaini langu inawezekana nikalijibu katika kipindi hiki, lipo tayari na nitakapojibu itakuwa ni maelezo marefu kidogo ili kila mtu aweze kuelewa. Namwomba Mheshimiwa Mbunge astahimili.

**SPIKA:** Sawasawa vizuri. Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Kuna tangazo moja la Kikao cha pamoja cha Kamati mbili. Kamati hizo mbili ni Kamati ya Sheria na Katiba na Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje.

Waheshimiwa Wabunge, tumepanga Kikao cha pamoja cha Kamati hizo mbili ili ziweze kuweka pamoja au kutengeneza majumuisho ya maoni ya Waheshimiwa Wabunge yaliyotolewa katika siku mbili za Semina kuhusu njia ya kufika kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, tumeona kwamba ili maoni yaweze kufanyiwa kazi vizuri na Serikali ni vema yakawekwa katika sura ya majumuisho na Kamati hizi mbili halafu baada ya hapo ndiyo tuyapeleke Serikalini.

Kwa hiyo, Kamati hizi mbili zinakutana kuanzia saa 5.00 asubuhi ya leo hii katika chumba Na. 231 ghorofa ya pili. Kamati ya Katiba na Sheria na Mambo ya Nje. Baada ya hapo nawaomba Waheshimiwa Wabunge kuwajulisha kwamba Taarifa Maalum ya Kamati ya Haki na Maadili na Madaraka ya Bunge itahitaji uamuzi rasmi wa Bunge. Kwa sababu inahusu kuvunjwa kwa maadili ya Waheshimiwa Wabunge miongoni mwetu na inataka Bunge lifanye uamuzi juu ya mapendekezo hayo.

Kwa hiyo ningewaomba tuahirishe wote kwenda kwenye chai mpaka kwanza tufanye uamuzi juu ya Taarifa hiyo. Sidhani kwamba utachukua muda mrefu sana. Nadhani ndiyo hayo tu niliyo nayo kwa leo. Kwa hiyo, tuendelee na *Order Paper,* Katibu endelea.

## TAARIFA ZA KAMATI

### Taarifa Maalum ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, yahusu Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu tuhuma za maombi ya udanganyifu ya *Visa* za kuingilia Ujerumani yaliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge watatu.

Mhehsimiwa Spika, suala hili linawahusu Waheshimiwa Wabunge watatu ambao majina na majimbo yao ni kama ifuatavyo:-

Moja, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mbunge wa Jimbo la Chambani, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe na Mheshimiwa Kassim Ali Saleh, Mbunge wa Mgogoni.

Mheshimiwa Spika, Wabunge hawa walikwenda Ofisi za Ubalozi wa Ujerumani, Jijini Dar es Salaam na kutoa maombi ya *visa* kuingia nchini Ujerumani kwa ajili yao na wanawake waliowatambulisha kuwa ni wake zao kwa njia ya udanganyifu.

Baadaye ilibainika kwamba taarifa walizozitoa Ubalozini hadi kuwezesha *visa* hizo kutolewa hazikuwa za kweli. Ubalozi wa Ujerumani nchini umepeleka malalamiko yake Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu suala hili. Wizara hiyo ikawasilisha Wizara ya Mambo ya Ndani ili Wabunge hao washughulikiwe kwa mujibu wa taratibu na Kanuni zinazotawala maadili ya Wabunge.

Kwa kuwa jambo hili pamoja na mambo mengine linahusu ukiukwaji mkubwa na wa aina yake wa maadili ya Wabunge, Wizara ya Mambo ya Ndani ililifikisha suala hili kwa Spika wa Bunge kwa msaada wa kukomesha tabia hii mbaya.

Chimbuko la suala lenyewe, Mheshimiwa Spika, suala hili lilijitokeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Karim Said Othman, tarehe 25 Agosti, 2004 alikwenda Ofisi za Ubalozi wa Ujerumani Jijini Dar es Salaam, alifuatana na Bi. Halima Abdallah Chambo, mwanamke mwenye asili ya Kisomali aliyedai ni mkewe na anasifiri naye kuelekea matembezini Ujerumni. Hivyo akamwombea *visa* na kupewa. Katika kuthibitisha kuwa Bi. Halima Chambo ni mkewe Mheshimiwa Karim Said Othman alitoa cheti cha ndoa kinachoonyesha kuwa ndoa yao ilifungwa tarehe 30 March, 2000 Jijini Dar es Salaam. Kiambatanisho kipo na taarifa kwa Wabunge watagawiwa hivi punde.

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Septemba, 2004 Bi. Halima Abdallah Chambo aliwasili Frankfurt Ujerumani bila mumewe Mheshimiwa Karim Said Othman, kinyume na maelezo yao kuwa watasafiri pamoja. Akiwa Ujerumani Bi. Halima Abdallah Chambo alijitambulisha kuwa jina lake halisi ni Anab Abdi Mohammad, mzaliwa wa Kismayo na raia wa Somalia na kwamba ameenda nchini hapo kuomba hifadhi ya kisiasa. Bi. Halima alikiri kuwa na *passport* ya Kitanzania aliyokuwa nayo na aliipata kwa udanganyifu kutoka kwa Ahmed Ahmed kwa gharama ya dola za Kimarekani 3,000. Halima bado yuko Ujerumani. *(Makofi)*

Kuhusu Khalifa Mohamed Issa, tarehe hiyo hiyo tarehe 25 Agosti, Mheshimiwa Khalifa naye alikwenda Ofisi za Ubalozi wa Ujerumani Jijini Dar es Salaam akifuatana na Bi. Sophia Ali Rage, mwanamke mwingine mwenye asili ya Kisomali akadai ni mkewe anasafiri naye kuelekea Ujerumani kwa matembezi. Akamwombea *visa* na kupewa. Katika kuthibitisha kuwa Bi. Sophia Ally Rage ni mkewe, Mheshimiwa Khalifa Issa, naye alitoa cheti cha ndoa kinachoonyesha kuwa ndoa yao ilifungwa tarehe 18 Agosti, 2002 Jijini Dar es Salaam.

Tarehe 18 Septemba, Bi. Sophia Ally Rage aliwasili Mjini Frankfurt Ujerumani bila mumewe Mheshimiwa Khalifa Issa kinyume na maelezo yao ya awali kuwa wangesafiri pamoja.

Mheshimiwa Spika, Bi. Sophia Ally Rage alijitambulisha kuwa jina lake halisi ni Jawahir Elmi Abshir, mzaliwa wa Baidoa na ni raia wa Somalia na kwamba ameenda nchini hapo kuomba hifadhi ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bi. Sophia alikiri kuwa pasipoti ya Tanzania aliyokuwa nayo aliipata kwa njia ya udanganyifu kwa namna fulani ya rushwa kutoka kwa Ahmed Ibrahim kwa gharama ya dola za Kimarekani 4,000. Bi. Sophia alirejeshwa nchini tarehe 18 Oktoba, 2004 baada ya ombi lake na hifadhi yake ya kisiasa kukataliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kuhusu Mheshimiwa Khamis Ali Saleh. Yeye alikwenda Ubalozi wa Ujerumani na kuomba kama Waheshimiwa wengine walivyofanya na yeye akimwombea *visa* mwanamke mwingine mwenye asili ya Kisomali, Bi. Fardhosa Musa Mohamed, aliyedai ni mkewe na kwamba wanakwenda pamoja Ujerumani kwa matembezi.

Kwa kuwa mazingira ya ombi hili yalionyesha kufanana na yale mengine ya awali, Ubalozi wa Ujerumani ukakataa ombi hilo kwa kuamini kuwa ni jaribio lingine la kuwapa watu *visa* za udanganyifu. Kwa hiyo, huyu alikataliwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya mahojiano na wote watatu, kama inavyofafanuliwa katika Kanuni ya 99(2)(ii) kwamba mojawapo ya majukumu ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ni kushughulikia mambo yote yanayohusu maadili ya Wabunge. Hivyo baada ya kupata maombi ya Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Spika, kwa barua yake ya tarehe 18 Aprili, 2005 alilileta suala hili kwenye Kamati ili lifanyiwe kazi. Kamati ilifanya mahojiano na Waheshimiwa Wabunge hawa watatu na maelezo yao ni kama ifuatavyo:-

Maelezo ya Mheshimiwa Karim Said Othman. Samahani nikitaja umri utaelewa kwa nini tunataja umri baadaye. Umri wake ni miaka 44. Ana wake wawili na watoto sita. Alifahamiana na Bi. Halima Chambo Dar es Salaam katika maeneo ya Ofisi za Bunge. Alidai kuwa Bi. Halima ni mchumba wake lakini hafahamu anapoishi wala ndugu zake isipokuwa Bi. Chambo alijitambulisha kuwa yeye ni Mzaramo wa Dar es Salaam.

Walikubaliana kwenda matembezini Ujerumani ndipo akaenda kumwombea *visa* katika Ubalozi wa nchi hiyo. Alieleza Ubalozini hapo kuwa Bi. Halima ni mkewe kwa kuwa tayari alikuwa anamchukulia hivyo. Baada ya kupata *visa* alikuja Dodoma kuhudhuria Mkutano wa Bunge na aliporejea Dar es Salaam hakumkukuta Bi. Halima. Jitihada za kumtafuta hazikuzaa matunda, hata hivyo hakutoa ripoti mahali popote. *(Kicheko)*

Alidai kwamba barua ya Waziri wa Mambo ya Ndani kwenda kwa Spika wa Bunge na kunakilishwa kwake ndiyo iliyomstua na kujua kwamba kumbe Bi. Chambo alimtoroka na kwenda Ujerumani peke yake. Toka wakati huo (mwezi Machi) hadi sasa amekuwa akifikiria aandike barua ya kuomba radhi Ubalozi wa Ujerumani nchini kutokana na jambo hili. Lakini bado hajatekeleza azma yake hii. Amekiri kufanya kosa kutokana na kutojua. Aidha, ameomba radhi na kueleza kuwa jambo hili ni baya sana.

Maelezo ya Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, umri wake miaka 46, wake wawili na watoto kumi na tatu (13). *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, alisema kwamba amefahamiana na Bi. Sphia Rage kwa muda mfupi na wakakubaliana kuoana. Alimweleza kuwa anapanga kwenda matembezini Ujerumani na Bi. Sophia akamwomba waende wote kutokana na mapenzi aliyokuwa nayo kwake

walikubaliana na akalazimika kusema uongo kwenye Ubalozi wa Ujerumani ili apate *visa* na kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, akiwa mbioni kutafuta fedha zaidi kwa ajili ya matumizi yao wakiwa Ujerumani ndipo Bi. Sophia akapotea. Baada ya kushindwa kumpata alibaini kuwa mwanamke huyu hakuwa mwaminifu hivyo akamtoroka labda baada ya kupata mwanamme mwingine. Hivyo akafuta safari ya kwenda matembezini Ujerumani. Hata hivyo, hakutoa taarifa sehemu yoyote na alibaini ukweli wa mambo baada ya kupata barua ya Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa kwa Mheshimiwa Karim Othman, naye muda wote huu amekuwa akifikiria kuomba radhi kwenye Ubalozi wa Ujerumani lakini bado hajafanya hivyo.

Kuhusu swali kwamba aliwezaje kumwamini Bi. Rage baada ya kumfahamu kwa muda mfupi sana hadi kuamua kumpeleka matembezini Ujerumani kwa gharama zake, Mheshimiwa Khalifa alieleza kuwa penzi changa ndilo lilimchanganya na kujikuta anakubali kila anachoambiwa bila kuuliza maswali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Khalifa aliomba asamehewe kwani hili ni kosa lake la kwanza na limetokea kutokana na utoto. Alikiri kuwa ni fedheha kwa yeye akiwa Mbunge kufanya kitendo hicho.

Maelezo ya Mheshimiwa Khamis Ali Saleh. Umri miaka 50, wake wawili (2), watoto kumi na nne (14). Amefahamiana na Bi. Fardhosa Musa Mohammed kwa muda mfupi na kuamua kwenda kupumzika Ujerumani kwa siku 10. Kwa kuwa alikusudia kumwoa Bi. Fardhosa hakuona ugumu kumgharamia wala kudanganya Ubalozi kuwa ni mkewe.

Hana uhakika na kabila la Bi. Fardhosa ila anahisi kuwa mwanamke huyu pengine ni chotara wa Kiarabu na anaishi Dar es Salaam na Dodoma. Maombi aliyopeleka Ubalozi wa Ujerumani kwa ajili ya Bi. Fardhosa kupatiwa *visa* yalikataliwa na alielezwa kuwa endapo ataamua kwenda yeye mwenyewe angepewa *visa* ila mwanamke huyo hatapatiwa.

Jitihada za kumwona Balozi wa Ujerumani nchini ili kubembeleza mkewe apatiwe *visa* zilishindikana na alielezwa kwamba hawezi kumwona wala kufanikiwa kwani maombi ya *visa* kama hayo yamefanywa mara nyingi na wahusika wanapoingia Ujerumani wanaanza kufanya biashara ya ukahaba.

Baada ya Bi. Fardhosa kukataliwa *visa* naye Mheshimiwa akavunja safari ya kwenda Ujerumani. Alikiri kuwa amevunja sheria na pia amekiuka masharti ya dini na akaomba radhi.

Maoni ya Kamati Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa jambo hili halikutokea kwa bahati mbaya bali Waheshimiwa hawa walipanga. Kwanza, pasipoti za wanawake wale zimetolewa muda huo huo wa Agosti, hii inaonyesha kuwa zilitafutwa mahsusi kwa ajili ya safari hiyo. Pasipoti hizo zinaambatanishwa, tunazo hapa, baadaye mtagawiwa sasa hivi. Walikuwa wanatengeneza kitu kidogo pale. Aidha, pamoja na kujua kuwa wanawake wale sio wake zao, walidiriki hata kutafuta vyeti vya ndoa kuonyesha kuwa wale ni wake halali. Katika

mazingira haya huwezi kusema kuwa hili ni bahati mbaya Mheshimiwa Spika. Aidha, inaonekana wazi kuwa *visa* hizo ziliombwa kwa makusudi ili kuwawezesha wanawake wale kusafiri peke yao. Hii inathibitishwa na visingizio vilivyotafutwa na Waheshimiwa hawa ili kutosafiri mara tu baada ya *visa* kupatikana.

Mheshimiwa Karim anaeleza kuwa bada ya *visa* kupatikana yeye alikuja Dodoma kuhudhuria Mkutano wa Bunge. *Visa* iliyotolewa ilikuwa ni kwa tarehe 10 - 28 Septemba, 2004. Alikuja Dodoma kuhudhuria Mkutano wa Bunge la kipindi hicho na wakati huo Bunge halikuwepo.

Maelezo ya Mheshimiwa Khalifa pia hayana uzito. Yeye anadai kuwa baada ya kupata *visa* akaanza kutafuta fedha za kwenda kuzitumia Ujerumani ndipo Sophia akamkimbia. Je, alipangaje safari hiyo na kukamilisha maandalizi yote haya wakati akijua kwamba alikuwa hana fedha.

Kwa upande mwingine maombi ya *visa* kwa Waheshimiwa Wabunge na wake zao huwa yanafanywa na Ofisi ya Bunge - samahani. Kitendo cha wao kwenda wenyewe Ubalozini kinaweza kutafsiriwa kuwa mbinu za kukwepa ukweli usijulikane na kuvuruga mipango yao ya kuvunja sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaamini kuwa walikusudia kufanya uhalifu. Kwanza waliwatambulisha wnawake wale kuwa ni wake zao wakati wakielewa wazi kuwa si kweli. Aidha walikwenda mbali zaidi hadi kutoa vyeti vya ndoa kuthibitisha hali hii. Kamati haifahamu vyeti hivi vimepatikana kwa njia gani isipokuwa ni wazi kuwa si vyeti halali kwani hata baadhi ya vipengele katika vyeti hivyo vinapingana na maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati.

Kwa mfano, suala la umri. Mheshimiwa Karim anaeleza kuwa umri wake ni miaka 44, Pasipoti inaonyesha alizaliwa mwaka 1958, cheti cha ndoa kinaonyesha kuwa wakati ndoa hiyo inafungwa alikuwa na umri wa miaka 40, kitu ambacho hata kwa hesabu za kawaida, si kweli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa Waheshimiwa hawa wameonyesha tabia ya kutowajibika *(no sense of irresponsibility)* kwa hali ya juu.

Baada ya kufahamiana na wanawake wale kwa muda mfupi sana na kabla ya hata ya kufahamu nyumbani au ndugu wa wake hao, tayari waliamua kutangaza ndoa na kuamua kwenda kutembea Ujerumani kwa gharama zao na kudanganya taasisi kubwa husika ili kufanikisha azma yao.

Mheshimiwa Spiika, Wameidanganya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje hadi wakadhaminiwa maombi yao na kisha wakamalizia kwa kuudanganya Ubalozi wa Ujerumani. Yote haya ni kwa ajili tu ya kile walichokidai kuwa ni penzi changa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge hawa pia wameonyesha kuwa hawakustahili na hawaelewi kabisa uzito wa dhamana ya Ubunge waliopewa na wananchi waliowachagua wala hawaelewi viongozi kama wao wanatakiwa kuishi vipi ili kuwa mfano mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa Bunge na Wabunge kwa ujumla wamechafuliwa na kudhalilishwa kwa kiasi kikubwa kwa kitendo hiki. Heshima na hadhi wanayopewa Wabunge ni kwa ajili ya kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kwa urahisi. Hadhi hii inapotumiwa vibaya namna hii Wabunge watakuwa wamewekwa katika hali mbaya na ngumu wanaposafiri. *(Makofi)*

Jambo hili litafanya Ofisi za Mabalozi mbalimbali kuwatilia mashaka Wabunge wa Bunge la Tanzania wanapopeleka maombi ya *visa* kwa ajili yao na au kwa watu wanaohusiana nao kutokana na udanganyifu huu. Ushahidi kwamba athari za suala hili zimeanza kujitokeza ni kitendo cha mwanamke aliyekwenda na Mheshimiwa Khamis Saleh, kunyimwa *visa* ubalozini hapo.

Pia Kamati imepata taarifa kuwa mmoja wa Wabunge wa Bunge lako Mheshimiwa Spika, alikwenda na mtoto wake katika Ubalozi fulani na akanyimwa *visa* hiyo kwa sababu hizo hizo wakaambiwa kama ni wewe peke yako sawa, lakini huyu hapana. Mbunge yuko hapa.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya kuchafua Bunge Kamati inaamini kuwa jina la Tanzania katika mataifa ya nje pia limechafuliwa. Inapofikia udanganyifu mkubwa kama huu unafanywa na kiongozi wa watu mwenye pasipoti yenye hadhi ya kibalozi *(Diplomatic Passport)* watu wa nje watawaaminije wananchi wetu wa kawaida kama Mbunge anafanya hivi. Hii itasababisha nchi yetu kuwekwa katika kundi la mataifa yale ambayo hayaaminiki na ambayo popote pale raia wake anapoonekana ni lazima achunguzwe na kupekuliwa vikali.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi Kamati inaamini kuwa kitendo hiki kinaweza kutafsiriwa kwa njia moja au nyingine kama kitendo cha ugaidi wa kimataifa kwani haifahamiki wanawake wale wa Kisomali walikwenda Ujerumani kwa nia gani hasa au walipanga kufanya nini kule licha ya kuomba hifadhi ya siasa.

Aidha, wanashiriki katika vitendo vya utapeli. Wamewezaje kupata vyeti vya ndoa bila kufunga ndoa yenyewe. Yawezekana pia kuwa wamefahamiana na Ahmed Ahmed na Ahmed Ibrahim waliotoa pasipoti kwa njia zisizo halali na yawezekana wamekuwa wakishiriki biashara hii kwa muda mrefu bila kubainika hadi sasa. Waswahili husema za mwizi ni arobaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa Waheshimiwa hawa wamekiuka kabisa viapo vyao walivyoapa wakati wanaingia katika Bunge hili Tukufu. Waliapa kuilinda Katiba ya nchi na Sheria zote. Jambo hili walilolifanya sasa ni kinyume kabisa na kiapo kile walichokiapa. Wao ndio walitunga Sheria na wao ndiyo wamehakikisha kwamba wametumia njia zote walizoweza kuhakikisha wanavunja sheria hizo ili kuwapeleka wanawake Ujerumani ambao sio wake zao. Hawakujali kabisa kuwa dunia hii sasa iko katika mapambano makali na vitendo vya ugaidi na kuwa nchi zote ziko macho sana na watu wote wanaoingia na kutoka. Kamati ina

wasiwasi kuwa yawezekana Waheshimiwa hawa wanajihusisha na mtandao fulani unaoshughulikia biashara za kusafirisha watu nje ya nchi na mtandao huo ndiyo unasaidia kubeba gharama za fedha zinazohitajika. Hii inatokana na ukweli gharama za safari kama hizi ni kubwa sana.

Kwa mfano, nauli ya ndege Dar es Salaam-Frankfurt kwa *Business Class* ni dola za Kimarekani 4,275 kama milioni nne laki nane na ishirini na tano (4,800,825.00), wao watake kusafiri watu wawili. Pasipoti za wanawake wale zimegharimu dola elfu tatu na elfu nne yaani 3,369,000.00 na 4,492,000.00. Dola elfu tatu ni milioni tatu na kadhaa. Dola elfu nne ni milioni nne na kadhalika, bado fedha za matumizi na gharama ya malazi. Kamati inaona gharama hizi ni kubwa kwa Mbunge wa Tanzania kuzibeba labda kama kuna mfanya biashara mkubwa ama kuna mtandao mwingine unaolipia gharama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu nzima uliotumika unaleta hisia kuwa Waheshimiwa hawa wamepewa rushwa na katika baadhi ya maeneo wametoa wao rushwa ili kufanikisha jambo hili. Aidha, Kamati imepata mshangao mkubwa kuhusiana na utendaji, uwajibikaji na udhibiti wa mambo katika taasisi zetu mbalimbali za Kiserikali. Inawezekanaje vyeti vya ndoa zinatolewa tu kwa watu ambao hawajafunga ndoa, wale watu wa Serikali walifanya nini?

Je, Serikali haifahamu kuwepo kwa hawa akina Ahmed Ahmed na Ahmed Ibrahim wanatoa *passport* kwa njia zisizo halali? Wanawake wale wa Kisomali waliingiaje nchini na kukaa kwa muda wote huo na kufanya shughuli zote za namna hii? *(Makofi)*

Wamefanya mambo yao kwa urahisi bila hata ya ufuatiliaji wowote? Je, kuna watu wangapi wa aina hiyo hapa nchini na wanapanga uovu gani kwa sasa? Kamati inataka baadaye Bunge lipate ufafanuzi kutoka Serikalini hususan kuhusu Watumishi wote wa Serikali waliohusika katika kufanikisha mchezo huu mchafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msimamo wa kisheria una...

**SPIKA:** Mimi ninashauri uende kwenye mapendekezo ya Kamati.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Sawa Mheshimiwa Spika. Baada ya kupitia hayo yote na kupitia sheria zetu zote na baadaye kupitia *precedent* ambayo Bunge lako limejiwekea, kuhusiana na makosa ya huko nyuma, Kamati inapendekeza mambo yafuatayo:-

(1) Kwa kuwa, suala hili lina sura ya kijinai, Kamati inapendekeza kuwa kwa kutumia Kifungu 12(3) cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Spika alipeleke suala hili kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili hatua za kisheria zichukuliwe hasa kwa wale wote waliyohusika na udanganyifu huu ambao ni fedheha kwa Serikali na Bunge lote kwa ujumla, hasa kwa wale watu wa Serikali. *(Makofi)*

(2) Kwa kuwa Wabunge hawa wanazo *passport* zenye hadhi ya Kibalozi ambazo walizipata kutokana na Ubunge wao na ndizo zinafanya Ubalozi wa Ujerumani au Balozi nyingine kuamini na kuwapatia *VISA* wanaodaiwa kuwa wake zao na kwa kuwa inaonekana

hawaelewi maana au uzito na umuhimu wa *passport* za aina hiyo kama Wabunge, Kamati inadhani kwamba wataendelea kuzitumia kinyume na inavyotakiwa. Kwa hiyo inapendekezwa kwamba Wizara husika iwanyang'anye Wabunge hao *passport* hizo ili wasiendelee kuzitumia kwa hadhi hiyo. *(Makofi)*

Hata hivyo, kwa kuwa pasipoti ni haki ya kila raia, basi iachwe hivyo hivyo. Basi Kamati inapendekeza wapewe *passport* za kawaida *(Ordinary Passport)*. *(Makofi)*

(3) Mheshimiwa Spika, Kamati inazidi kufafanua kwamba, wote walioshiriki katika suala hilo wapelekwe Mahakamani kwa mujibu wa sheria za nchi. Kamati inapendekeza kwamba; kwa kuwa wamekiuka maadili ya Bunge lako Tukufu, Wabunge hawa wasimamishwe shughuli au kazi ya Ubunge kuanzia tarehe ya leo, sasa hivi, hadi tarehe 5 Agosti, 2005. Kwa maana hiyo, kuanzia sasa hawatahudhuria hata Kamati zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na nilimwona Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, akiunga mkono. Kwa hiyo, hoja imetolewa na kuungwa mkono. *Order Paper* inasema, Bunge sasa lipokee na likubali mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii maalum. Hii ni taarifa ya Kamati, kwa hiyo, haina Msemaji wa Serikali wala wa Upande wa Upinzani. Tunaingia moja kwa moja kupata maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu mapendekezo haya. Nani atapenda kutoa maoni kama yanakubaliwa au vipi? *(Makofi)*

Kimya cha Waheshimiwa Wabunge ni kwamba mapendekezo ya Kamati yamepitishwa.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa ya Kamati Maalum ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge yalikubaliwa na Bunge)*

**WABUNGE FULANI:** Wasimame!

**SPIKA:** Wanatolewa nje ya Bunge kuanzia sasa na wasionekane tena mpaka Bunge litakapovunjwa tarehe 5, Agosti, 2005. Majina yao yametajwa, sasa naomba wote watatu wasimame kama wapo na watoke nje ya Bunge wakisindikizwa na *Sergeant-At-Arms*. *Sergeant-At-Arms* sogea huku. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge Wote Watatu Waliohusika walitolewa nje ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge waliyosimamishwa sasa wamekwishatoka nje ya Ukumbi wa Bunge. Sasa tunaendelea na kazi iliyobaki. Wanaopenda kwenda kunywa chai sasa ni ruksa.

**Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa Mwaka 2003 na Mwaka 2004**

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama au Mwakilishi wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, awakilishe taarifa yake. Lakini nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba taarifa hizi zilishawasilishwa Mezani na zilishapelekwa Serikalini zikafanyiwa kazi. Kwa hiyo, sidhani kwamba kutakukwa na mjadala mrefu kwa sababu zimeshafanyiwa kazi na Serikali na majibu ya Serikali yameshatolewa. Tunadhani itakuwa ni kazi nyepesi tu kwa Bunge kuzipokea. Mheshimiwa Ngwatura endelea.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA (k.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Spika, taarifa ya kazi za Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha kwa niaba ya Wabunge wa Kamati, Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu shughuli zilizofanywa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha taarifa ya Kamati hii ningependa kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati nikutakie wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kheri ya mwaka mpya wa 2005. Aidha, ningependa kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Charles Nyerere kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mbunge wa Bunge lako Tukufu.

Napenda pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza na kuwatakia kila la kheri wale wote waliochaguliwa kwenda kwenye Bunge la Afrika ambao ni Mheshimiwa Getrude Mongella, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa William Shija, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou. Ninawatakia kila la kheri katika kuwakilisha nchi yetu. Pia, nampongeza Mheshimiwa Sophia Simba kwa kuteuliwa kwake kuwa Mbunge wa *SADC* kuwakilisha Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ulinzi na Usalama ina Wajumbe 14 nao ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Dr. John S. Malecela - Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge - Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Karnali Feteh Mgeni, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Haji Sereweji, Mheshimiwa Omar Mjaka na mimi Ireneus Ngwatura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 ya Kanuni za Bunge toleo la 2003, majukumu ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ni kusimamia shughuli za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama ifuatavyo:-

Kushughulikia Bajeti za Wizara hizi; kushughulikia Miswada ya sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge inayotokana na Wizara hizo; kushughulikia taarifa za kila mwaka na za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma; kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizi kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya Kamati, Kamati ilijiwekea utaratibu ufuatao:- Kupokea taarifa ya hali ya ulinzi na usalama nchini kabla ya kila Mkutano wa Bunge kuanza kutoka Ofisi ya Rais, Tawala Bora, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kutoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; kupokea taarifa za utekelezaji na kushughulikia Bajeti ya Wizara hizi kabla ya kuanza Mkutano wa Bunge wa Bajeti; Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo inatokana na Wizara hizi kila inapoagizwa na Mheshimiwa Spika; kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyoko chini ya Wizara hizi zinazowasilishwa mbele ya Kamati na mwisho kutembelea shughuli zinazofanywa na Wizara hizi katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Tanga.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa na Kamati kwa mwaka 2003 ni kuchagua Viongozi wa Kamati. Kazi ya kwanza iliyofanywa na Kamati ilikuwa ni kumchagua Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa John S. Malecela, Mbunge wa Jimbo la Mtera aliyechaguliwa bila kupingwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati tarehe 24 Machi, 2003 na Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama - Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, alichaguliwa kuwa Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati tarehe 20 Oktoba, 2003.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, waliwasilisha mbele ya Kamati taarifa hali ya ulinzi na usalama nchini. Taarifa hizi ziliwasilishwa kabla ya kuanza Mikutano ya Bunge na kwa ujumla zilieleza kuwa nchi yetu ilikuwa katika hali ya usalama na utulivu kwa mwaka wote wa 2003.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Ofisi ya Rais, Utawala Bora, ilielezea masuala mengi kuhusu usalama wa Taifa letu na namna ya kujitahadhari na mambo haya yakiwemo masuala kuhusu uhaba wa chakula, vijana kutokuwa na kazi, ujenzi holela wa Vituo vya Mafuta na kadhalika. Kuhusu hali ya chakula, Kamati ilipokea taarifa kuwa sehemu kubwa ya nchi yetu ilikuwa inakabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula. Aidha, bei ya chakula ilikuwa inazidi kupanda wakati watu wengi Mijini na Vijijini walikuwa hawana uwezo wakununua chakula hicho.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo hili, Serikali iliondoa kodi kwa wafanyabiashara ili waweze kuingiza chakula nchini na kukiuza kwa bei nafuu. Lakini lengo hili halikutekelezwa kama ilivyokusudiwa. Aidha, Serikali ilitoa ruzuku kwa mbolea iliyotakiwa kupelekwa katika Mikoa ya Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa ili iuzwe kwa bei nafuu. Matokeo ni kwamba mbolea ile haikuwafikia wakulima wa Mikoa hiyo kwa wakati wake na pale ilipofikishwa, bei ilibaki kuwa juu. Hali hiyo ilisababisha manung'uniko kwa wakulima wa Mikoa hiyo na kusababisha malengo ya uzalishaji wa chakula kutokufikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa liko kundi kubwa la vijana wasiofanya kazi nchini wakiwemo wale wanaohitimu Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Vyuo Vikuu. Iko hatari kwa vijana hawa kujihusisha na vitendo vya uhalifu. Ujenzi holela wa Vituo vya Mafuta nchini, Kamati ilisikitishwa na taarifa kwamba Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 1956 na tangazo la Serikali Na. 678 la mwaka 1964, havizingatiwi wakati wa kujenga Vituo vya Mafuta nchini. Vituo vinajengwa holela karibu na makazi ya watu, maduka na Vituo vya Mabasi na kwamba wamiliki wa Vituo hivyo wanakwepa kulipa kodi. Hali hiyo ni hatari kwa usalama wa Miji yetu hasa kwa majanga ya moto licha ya kuinyima mapato Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutangaza kuwa Ukimwi ni janga la Taifa mwezi Decemba, 1999, ugonjwa huo bado unaendelea kwa kasi kubwa Mijini na Vijijini. Aidha, elimu na huduma nyingine kuhusu ugonjwa huo hazifikishwi Vijijini. Upungufu wa elimu kuhusu ugonjwa unaendeleza mauaji kwa vikongwe, kutokana na imani ya uchawi. Kwa kifupi ugonjwa wa Ukimwi ni tishio kubwa kwa uhai na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, bado kuna malalamiko mengi nchini kuhusu watu kudaiwa na kutoa rushwa ili waweze kupewa huduma na haki zao. Haki inauzwa kama mazao au bidhaa na hivyo kuathiri misingi ya demokrasia na utawala bora. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika taarifa yake, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alieleza kuwa, mwaka 2003 makosa makubwa ya jinai na ya ajali za barabarani yaliongezeka ikilinganishwa na yale ya mwaka 2002. Makosa hayo yalihusu unyang'anyi wa kutumia silaha, wizi wa magari na mifugo. Mauaji ya vikongwe kutokana na imani ya uchawi na sababu nyingine mbalimbali. Kumiliki silaha kinyume cha sheria, kupatikana na madawa ya kulevya na ubakaji.

Mheshimiwa Spika, kosa lingine ambalo ni tishio la usalama ilikuwa ni kuzuka kwa vikundi vya kidini vya Kiislam na Kikristo vilivyokuwa vinafanya mihadhara kwa kukashifu dini za watu wengine. Mihadhara hiyo ilifanyika katika Jiji la Mwanza, Dar es Salaam, Kigoma, Ujiji, Kasulu na Shinyanga. Vikundi hivyo pamoja na Kamati ya kutetea haki za Waislam Tanzania, vilikuwa vinapandikiza chuki kati ya Waislam na Wakristo.

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ilieleza pia kwamba Jeshi la Polisi lilipambana vikali katika kuzuia uhalifu huo kwa kufanya doria na *operation* pamoja na kuimarisha mafunzo na vitendea kazi. Hata hivyo, ufanisi wa Jeshi hilo uliathiriwa na upungufu wa vitendea kazi kama vile magari na vifaa vya mawasiliano. Fedha iliyopitishwa na Bunge kwa matumizi ya kununulia magari haikutolewa, badala yake ilibaki Hazina kulipia madeni ya nyuma kinyume cha mategemeo ya wahusika.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msongamano wa wafungwa Magerezani liliendelea kukua. Wakati nafasi zilizoko magerezani kisheria Tanzania Bara ni wafungwa na mahabusi 21,000 walikuwepo wafungwa na mahabusu 47,306. Kati yao wafungwa walikuwa 26,365 na mahabusi walikuwa 20,711. Ongezeko hilo zaidi lilitokana na mahabusu wengi kukaa Magerezani kwa muda mrefu bila kesi zao kusikilizwa. Sheria za *Parole* vile vile haikutumika kwa ukamilifu katika kupunguza msongamano Magerezani. Ongezeko hili lilikuwa linaathiri utoaji wa huduma

bora za chakula na matitabu Magerezani. Hata hivyo, Serikali imeboresha huduma Magerezani kwa kuwapa wafungwa sare nzuri na chakula bora.

Mheshimiwa Spika, Wahamiaji haramu wamekuwa tatizo kubwa kwa usalama wa Taifa letu. Tatizo hilo ni kubwa zaidi katika Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa. Wengi wa Wahamiaji haramu wanajihusisha na vitendo vya ujambazi, ubakaji, wizi wa mazao na mifugo. Uenezaji wa silaha nchini, ujangili na kufanya biashara na ufugaji haramu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika taarifa yake, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alieleza kuwa, katika mwaka 2003 hali ya mipaka kati ya Tanzania na nchi jirani ilikuwa shwari. Tatizo la mpaka wa Tanzania na Uganda limepatiwa ufumbuzi kwa kuweka mawe ya mpaka Na. 27 na Na. 32 yaliyokuwa yameng'olewa na kuongeza mengine 400. Vile vile, kila upande umeshafyeka mita kumi kutoka katikati ya mpaka. Lengo ni kufyeka mita 50 kwa kila upande ili kulingana na sheria za mipaka Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo zoezi hili limesababisha familia zaidi ya 200 za Watanzania kujikuta ziko upande wa Uganda na zaidi ya familia 160 za Waganda zimejikuta ziko upande wa Tanzania. Aidha, zoezi hili limesababisha familia nyingi kubomolewa nyumba zao. Mpaka wa Tanzania na Rwanda una utata pia. Ndani ya Mto Kagera, Tanzania inatambua Kisiwa cha Mchuzi kuwa ni sehemu yake wakati Rwanda inadai kuwa ni Kisiwa chake. Aidha, Wanyarwanda hutumia vivuko haramu kuvusha mizigo na kuingiza Wahamiaji haramu nchini Tanzania. Wakati huo huo Vikosi vya Askari wa Rwanda mpakani mwa Tanzania vinaleta hofu kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama katika mipaka ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya *Congo, DRC* na Burundi, pia haikuwa shwari. Yalikuwepo matokeo ya Askari ya kuvuka mipaka na kuingia Tanzania. Askari hao Wahamiaji haramu na wakimbizi kutoka nchi hizi waliingiza silaha Tanzania na kufanya ujambazi wa kutumia silaha.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003, Kamati ilitembelea shughuli zilizofanywa na Wizara zilizotajwa hapo juu katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro tarehe 28 - 30 Mei, 2003. Kamati ilifanya majumuisho ya ziara hiyo na kuwasilisha maoni na ushauri wake kwa Serikali na Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti za Wizara hizi mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 - 24 Oktoba, Kamati ilifanya ziara nyingine katika Mkoa wa Dar es Salaam na Tanga. maeneo yaliyotembelewa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yalikuwa ni Kikosi cha Wanamaji, Karakana Kuu ya Polisi, Kikosi cha Mbwa na Farasi na Chuo Kikuu cha Polisi. Maeneo yaliyotembelewa ni Zahanati ya Polisi, Nyumba wanazoishi Polisi, Nyumba za Kikosi cha Polisi na Kutuliza Ghasia na Kambi ya Wakimbizi ya Chogo Wilayani Handeni Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yaliyotembelewa na Kamati ni Kambi ya Jeshi la *General* Twalipo Mgulani, Changanyikeni, Karakana Kuu ya Jeshi, Hospitali Kuu ya Jeshi na Nyumba wanazoishi Wanajeshi. Maeneo mengine ni Kiwanda cha Samani cha Suma, *JKT* Chang'ombe, nyumba 150 zilizojengwa na Idara ya Ujenzi ya *JKT* katika eneo la Mbweni Malindi na Bwalo la *JKT* la Ndege *Beach*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya majumuisho ya ziara, Kamati iliwasilisha ushauri wake kwa Wizara husika. Hata hivyo napenda kusisitiza maoni ya Kamati kuhusu maeneo yaliyotengwa kwa matumizi ya kijeshi kwamba yasigawiwe kwa raia. Kamati ilipotembelea Kikosi cha *313KJ* Mbuni *Brigade* ilielezwa kwamba eneo la Jeshi lililokuwa linatosheleza mafunzo ilikuwa *square kilometre 970*. Eneo hili limemegwa na kugawiwa kwa raia na kubaki na *square kilometre 540* eneo ambalo halitoshelezi kwa mafunzo. Hivyo hivyo, Kamati ilipotembelea eneo la Mbweni *JKT*, ilielezwa kuwa hekta 300 za eneo lake zilikuwa zimegawiwa kwa raia na *JKT* kubakiwa ni hekta 100 tu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kusisitiza ni la Serikali kuimarisha uwezo wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mashirika haya ni Suma *JKT*, Idara ya Ujenzi ya *JKT*, Nyumbu, Mzinga na Shirika la Magereza *(Prisons Cooperation).* Mashirika hayo kwa ujumla yanahusika na kilimo, ufugaji viwanda na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitafakari taarifa zilizowasilishwa mbele yake pamoja na shughuli ilizozitembelea na inatoa maoni yake na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali isimamie Watendaji walioko karibu na wakulima ili kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati; Mabwana Shamba na Bibi Shamba waungane na wakulima katika kutekeleza kanuni za kilimo bora ili wapate mavuno ya kukidhi mahitaji ya nchi na ya ziada. Serikali iwe inasimamia vizuri ugawaji wa chakula kutoka akiba yake *SGR* na kuhakikisha kuwa kinawafikia walengwa haraka na kiwango cha akiba kiongezwe ili kukidhi mahitaji. Pia, Serikali itazame upya sera ya mazao ya chakula. Kilimo cha umwagiliaji kiwe endelevu na Serikali itilie mkazo elimu ya kilimo hicho na matumizi bora ya maji.

Mwisho maghala yaliyopo nchini yasiuzwe na badala yake yaboreshwe ili yatumike kwa kuhifadhi chakula. Vyakula vingine viongezwe katika orodha ya vyakula vya kuhifadhiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaombwa iwafahamu wamiliki wote wa Vituo vya Mafuta visivyo rasmi na ichukue hatua za kisheria dhidi ya wamiliki hao. Kwa kuwa ni jambo la hatari kwa Vituo vya Mafuta kuwa karibu na makazi ya watu na mali zao, Serikali ichukue hatua za kinga ikiwa ni pamoja na kuwapa muda maalum wamiliki wake kuvibomoa na kujenga Vituo vinavyozingatia sheria ya Mipango Miji. Vile vile, kufuatia ongezeko kubwa la magari Jijini Dar es Salaam, Serikali itenge maeneo ya kutosha ya kujenga Vituo vya Mafuta.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kutoza kodi kwa wamiliki wa mafuta yote yanayoingizwa nchini. Serikali iziagize Halmashauri zote nchini kuzingatia sheria ya Mipango Miji ya mwaka 1956 na tangazo la Serikali Na. 678 la mwaka 1964 ili zisimamie sheria, kanuni na taratibu zote za ujenzi wa Vituo vya Mafuta. Serikali isitishe ujenzi wa Vituo vyote visivyo rasmi vinavyoendelea kujengwa nje ya utaratibu mahali popote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa Ukimwi ni tatizo na tishio kubwa kwa uhai na maendeleo ya Taifa letu. Serikali isimamie kuona kwamba elimu kuhusu Ukimwi inawafikia watu wa Mijini na Vijijini na Taasisi zote nchini kama vile Shule, Vyuo, Kambi za Majeshi na kadhalika. Aidha, Serikali ipeleke Vijijini Vituo vya Kupima Ukimwi. Msisitizo mkubwa uwe katika kubadili tabia. Serikali iendelee kushirikisha viongozi wa Taasisi za Kidini katika vita dhidi ya Ukimwi na wawezeshwe kufanya kazi hiyo.

Pia, Serikali idhibiti matumizi ya fedha zote zinazotolewa kwa ajili ya kupambana na Ukimwi ili zitumike kwa manufaa ya jamii yote na kuleta matunda yaliyokusudiwa. Matumizi ya fedha hizi kwa sasa hayaridhishi. Mwisho, Serikali igharamie utafiti wa dawa za kutibu Ukimwi na dawa za asili zitiliwe mkazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Serikali iendelee na jitihada zake za kudhibiti uhalifu unaoongezeka nchini. Serikali idhibiti mihadhara ya kidini inayopandikiza chuki kati ya watu na ichukuliwe kuwa ni tatizo na chanzo cha kuvuruga amani nchini. Serikali ichukue hatua za kukomesha mauaji ya vikongwe. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizozichukua za kuboresha huduma kwa wafungwa kama vile sare, chakula na kadhalika. Tunashauri kwamba huduma hizi ziendelee kuboreshwa kwa Magereza yote. Serikali isimamie utoaji wa leseni kwa madereva ili wawe wanapewa wanaopitia Vyuo vya kufundisha udereva.

Aidha, Serikali ihamasishe uanzishwaji wa Vyuo vya Udereva vya viwango vya juu kama viwango vya Chuo cha Usafirishaji Tanzania na Vyuo vya *VETA*. Serikali iboreshe utaratibu wa kung'oa vibanda barabarani ili uwe unafanywa kwa uangalifu na kwa ushirikiano na vyombo vyote husika ili kuepuka vurugu. Pia, Sheria ya *Parole* ifanyiwe marekebisho ili itumike kwa wafungwa wa aina zote na sio kwa wenye vifungo vifupi tu ili kupunguza msongamano wa wafungwa. Serikali iangalie uwezekano wa watuhumiwa wenye makosa madogo madogo kujidhamini wao wenyewe. Serikali pia iangalie uwezekano wa kutumia adhabu za faini na vifungo vya nje zaidi badala ya vifungo vya Magerezani.

Kwa kuwa wengi wa watu walioko Magerezani ni mahabusu, Serikali ihakikishe inatafuta njia kwa vyombo vyake kama vile Polisi, Magereza na Mahakama kushirikiana katika kupunguza msongamano wa mahabusu kwenye Magereza yetu. Kamati inawapongeza viongozi wa Wilaya ya Karagwe, kwa kuwa na utaratibu mzuri wa kuainisha wahamiaji haramu. Serikali iziagize Wilaya nyingine za mipakani kufuata mfano huo. Serikali itoe vitambulisho vya uraia ambavyo si rahisi kughushiwa na zoezi la kuvigawa lianze mara moja kwa wananchi wanaoishi mipakani. Serikali pia isimamie kuona kuwa Watumishi wa Idara ya Uhamiaji ni waaminifu na waangalifu katika kutekeleza kazi zao. Kadhalika Serikali iwe makini zaidi kuchunguza wageni wanaoomba uraia.

Sheria inayosimamia utoaji wa vibali kwa wageni vya kufanya kazi nchini itekelezwe kwa ukamilifu. Aidha, Serikali isitoe kiholela ardhi kwa wageni, hasa mipakani ili kuepusha migogoro kwa siku za baadaye. Serikali idhibiti wahamiaji haramu waliovamia katika Visiwa vyote nchini hususani katika Ziwa Victoria na hatua za kuwabaini zichukuliwe. Serikali pia ifanye *operation* maalum ya kusafisha wahamiaji haramu kabla ya uchaguzi wa mwaka 2005.

Serikali iwaelimishe wakimbizi ili waweze kujua haki, wajibu na mipaka yao. Aidha, viongozi wa makambi wawe makini zaidi katika kuishi na wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliipongeza Serikali kwa kuondoa kero za wanajeshi, hususani kuhusu likizo, sare, chakula na makazi. Serikali iendelee kushughulikia kero za wanajeshi zilizobaki. Serikali pia iendelee na juhudi zake za kidiplomasia za kuleta amani katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Serikali iwatahadharishe wananchi kuwa waangalifu na wawe wepesi kutoa taarifa kwa Askari wanapoona mabomu au vitu wasivyovielewa.

Kamati inayapongeza Mashirika ya Nyumbu na Mzinga kwa kuweka muda kuendelea kuwepo licha ya Serikali kutokutoa fedha za kutosha kuyaendesha kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi. Serikali iongeze juhudi za kuyatafutia Mashirika hayo wabia ili yaweze kujiendesha yenyewe. Serikali isomeshe wataalam wetu nchini ili kwenda sambamba na mabadiliko ya kiteknolojia duniani. Pia, Serikali itatue mgogoro wa ardhi lililopo kati ya Shirika la Mizinga na raia.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza Mashirika ya Nyumbu, Mzinga na Suma *JKT* yaundwe kisheria ili yawe Mashirika ya Umma na yawe na akaunti zake yenyewe badala ya kuwa ni sehemu ya Wizara mama. Pia, Serikali iyaimarishe Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi na Kujenga Taifa, kwa kununua bidhaa za Mashirika hayo na kuyapa kandarasi za ujenzi wa majengo ya Serikali. Idara ya Ujenzi ya *JKT* kwa mfano iliweza kukamilisha ujenzi wa nyumba 150 katika eneo la Mbweni, Malindi, Dar es Salaam kwa muda uliopangwa na bila kuongeza gharama. Serikali iangalie uwezekano wa shughuli za Serikali zilizojengwa na Idara ya Ujenzi ya Jeshi la Kujenga Taifa katika eneo la Mbweni, Malindi, Dar es Salaam, zigawiwe kwa watumishi wa Serikali haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa kumaliza taarifa hii, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Prof. Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Mheshimiwa Omar Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Wilson Masilingi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora na Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano wao mkubwa wa Kamati hii pamoja na Makatibu Wakuu na Wataalam wa Wizara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, Katibu Wabunge na *Secretariat* ya Bunge kwa kazi na huduma mliyoitoa katika kufanikisha majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa kuandaa taarifa hii na kunipa heshima ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mwisho, nawashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Unaomba kutoa hoja gani? Si umemaliza! Anatoa hoja kwamba Bunge likubali taarifa hiyo, ni kweli sasa unaweza kwenda basi. *(Kicheko)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, naomba univumilie, taarifa ya kazi za Kamati za Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa mwaka 2004.

**SPIKA:** Sasa wewe ulikuwa unasoma nini kama sio hiyo. Hiyo uliyowasilisha ni nini? Sio hiyo!

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Taarifa ya mwaka 2003 ndio ilivyo kwenye *Order Paper.*

**SPIKA:** Sasa ya mwaka 2004!

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Ziko taarifa mbili kwenye *Order Paper*.

**SPIKA:** Hapana Sagasii, Katibu tuna *Order Paper* ngapi? Sagasii, tuna *Order Paper* ngapi mimi nina moja tu.

Waheshimiwa Wabunge, naelezwa kwamba *Order Paper* imeandikwa kwa makosa. Ilikusudiwa taarifa ya mwaka 2003 ndio iwasilishwe kwa kujadiliwa na umeshaiwasilisha. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Nina wasemaji watatu kama nilivyoeleza, mambo haya yameshafanyiwa kazi ya 2003. Kwa hiyo, hawakujitokeza wengi kuchangia. Mheshimiwa Choya, Mheshimiwa Mporogomyi na Mheshimiwa Derefa, nitawaita kwa mpangilio huo.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie angalau kwa kifupi. Lakini nachangia tu baada ya kuona kwamba kuna mambo mengi ambayo nitayaongezea ili kuzidisha maana ya taarifa hii.

Kwanza kabisa, mimi naomba nijikite kabisa kwa upande wa Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusu suala la ajira. Suala la ajira nimelifuatilia kwa makini sana na kwa karibu sana nikakuta kumejitokeza matatizo mazito katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Matangazo yanatolewa kwenye magazeti na Wizara au Serikali kwa jumla inafahamu kwamba haya magazeti yanawafikia wachache na hayaendi mpaka huko Vijijini. Wakishayapata yale magazeti wanasoma matangazo wanajikuta wamechelewa na usaili wa wale ambao wameona yale matangazo katika magazeti hayo wanaambiwa kwamba usaili unapaswa ufanyike Dar es Salaam.

Sasa jambo hili limenishangaza na linanisikitisha kwa namna ya pekee na inaonekana Wizara ya Mambo ya Ndani kwa upande wa suala hili ni kama wageni katika nchi hii. Ni nani asiyejua mawasiliano yalivyo katika nchi hii, kwamba mtu anayetoka Biharamlo, Mkunya na

Mtwara amepata tangazo na anaambiwa kwamba siku ya usaili itakuwa ni Dar es Salaam tarehe fulani tena wanaweka siku kama moja au siku mbili. Mtu utasafirije kutoka Biharamlo katika Kijiji kimoja kinaitwa Nyabugombe, katika Kijiji kimoja kinaitwa Kibamba na kule Mkunya huko Mbambabay uje Mpaka Dar es Salaam?

Huyu anayesafiri kutoka kwenye Vijiji hivyo kuja Dar es Salaam anatumia nauli yake na haieleweki wala hana uhakika kama atashinda. Matokeo akishindwa inabidi arudi yeye peke yake bila msaada wowote. Wizara ya Mambo ya Ndani kama hamlielewi hili, nasema Mheshimiwa Waziri kwa kweli kuna neno moja la kilatini *effeta* (fumbuka). Hili jeshi sasa limebaki ni la watu wachache ndani ya wale wale waliomo. Wanaajiri watoto wao na hii itapelekea au itasababisha Jeshi zima lipungue lisiwe na *discipline,* maana yake kila mmoja atakachokuwa anakifanya kama ameajiriwa na anajua kwamba ndugu yangu ndiye aliyesababisha mimi niajiriwe, akifanya kosa anahamishwa. Mifano halisi tu ni kama kule Mbarali. Chunguza sana wale wote waliohusika, kila mmoja ana ndugu, ana jamaa.

Hili mimi kwa kweli nalisikitikia na nalipinga vibaya sana. Watu wetu hawataajiriwa hata kama watakuwa wameshinda masomo. Naomba tuenzi ule utaratibu wa zamani na hebu igeni utaratibu unaotumiwa na Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ule utaratibu ambao ulikuwa unatumika wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya kwa kupata vijana kutoka Vijiji kwenye Vijiji mbalimbali wanakuja wanajisajili pale, wanasailiwa, baada ya kusailiwa ndio wanapelekewa kwenye kazi hizo, wanapelekewa Vyuoni. Huo utaratibu tuuenzi. *(Makofi)*

Halafu kitu kingine ambacho kinanisikitisha ni kwamba kuna kigezo ambacho kinatumika, kigezo hicho ni cha *Birth Certificates.* Hivi mbona tunakuwa wageni katika nchi hii? Ni nani asiyejua kwamba Serikali kwa ujumla haijatengeneza mazingira muafaka au mazuri ya upatikanaji wa Vyeti vya Kuzaliwa kwa urahisi? Ni nani asiyejua? Wameshatumia hivyo vigezo kwamba usipokuwa na *Birth Certificate* wala hupokelewi. Matokeo yake wanapokelewa wale waliokuwanavyo. Kwa hiyo, sasa hivi Wizara ya Mambo ya Ndani inaajiri wale waliomo ndio wataendelea kuwemo na wale wasiokuwemo hawatakuwemo tena mpaka siku ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, nakwambia hili ni jambo la ajabu na vielelezo ninavyo. Usaili wote unaofanyika Dar es Salaam kuanzia Jeshi la Polisi, Uhamiaji, Magereza, hivi Dar es Salaam ndio Tanzania na Tanzania ndio Dar es Salaam? Watu wetu kabisa mmewaacha! Mimi naomba Wizara ya Mambo ya Ndani ihakikishe inalirekebisha hili suala haraka sana iwezekanavyo, kinyume na hapo tunasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mnaendeleza utaratibu huu wa kuwaajiri wale waliomo ina maana hata *discipline* itapungua. Utendaji kazi hautakuwa mzuri na Jeshi zima au Mambo ya Ndani itakuwa haina utaratibu mzuri katika kufanya kazi. Kwa mambo mengi, nasema mnafanya kazi vizuri, lakini katika usaili katika ajira hii ajira inasikitisha mno. Wanajiajiri wao waliomo. Kwa hiyo, ninaomba hizi *Birth Certificates* tufuate utaratibu ule wa kupata hata *affidavits*. Tuna watu wanaoaminika, Mahakimu wa-*certify* tu kwamba hii *affidavit* inaweza ikatumika kama Cheti cha Kuzaliwa, baadaye atatafuta. Maana yake sisi sote uwe Waziri, uwe nani, sote tumetoka Vijijini tunaelewa mazingira ya kule. *(Makofi)*

Sasa tumefumba, fumbukeni macho. Wizara ya Mambo ya Ndani itakuwa ni ya kundi moja. Ninaomba kabisa, mimi kwa upande wa ajira ndilo jambo ambalo limenisikitisha na kila unaposoma magazeti ya matangazo kwamba kuna ajira katika Wizara ya Mambo ya Ndani wote wanatakiwa waende kusailiwa Dar es Salaam. Kweli huu ndio utaratibu!

Halafu kwa upande wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Wizara hiyo lazima tuipongeze, naipongeza kabisa kwa namna ya pekee. Lakini kuna jambo moja ambalo nilikuwa napenda tu niijulishe Wizara kwamba, kuna hawa Askari wetu ambao huwa wanakwenda kwenye *operations* hasa kule mipakani, wale wanaotoka kwenye Vikosi mbalimbali hususani Biharamlo. Wanapokuwa wanakwenda kule, posho zao hazifikiriwi. Anakwenda kana kwamba labda kule anakwenda kupigania uhuru. Wafikiriwe, wapewe posho za kutosha na wanawaacha wake zao katika hali ngumu na familia wanaziacha katika hali ngumu. Kwa hiyo, lazima wafiriwe kuongezewa posho.

Askari hawa wanapofika kule kwenye maeneo ya kufanyia kazi, unakuta wanajenga sehemu ya kujihifadhi na jua au na mvua kwa majani. Hata *tents* hawana. Kwa hiyo naomba Wizara iliangalie hili suala kwa makini na kwa namna ya pekee. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kusisitiza Wizara ya Mambo Ndani ibadilishe mtindo wa ajira. Kamati za Ulinzi na Usalama ziendeleze utaratibu ule uliokwishaanzishwa, uliokuwepo kiasi kwamba Jeshi au Wizara ya Mambo ya Ndani iwe na watumishi wanaotoka kila kona ya nchi hii. Maana yake hii ni nchi yetu wote, si watu watoke eneo moja tu na mtu ambaye yumo anatumia nafasi yake anachukua watu wake ndugu zake, ndugu na jamaa na marafiki ndio wanaingia mle. Sasa matokeo hata *discipline* itapungua, haitakuwepo kabisa. *(Makofi)*

Watumishi wote watakuwa kila mmoja si ana mlinzi? Kila mmoja ana mtu anayemtetea na Waziri atakuja kushindwa, *IGP* atakauja kushindwa kutimiza wajibu wake, Mkurugenzi wa Uhamiaji atashindwa kutimiza wajibu wake, Kamishna wa Magereza atakuja kushindwa kwa sababu kila mmoja ana mtu ambaye anamtetea hata kama anafanya maovu.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na niunge mkono hoja iliyotolewa na Kamati ya Ulinzi na Usalama. Lakini pia naomba niipongeze Kamati hii kwa sababu kazi nyingi ambazo wamekuwa wanazifanya, zimekuwa na matokeo mazuri tu. Walitembelea Gereza langu la Kasulu, bahati mbaya mimi nilikuwa nimesafiri, lakini nilipata taarifa kazi waliyoifanya pale ilikuwa nzuri sana maana walifanya mazungumzo, na karibu Viongozi wote na wengine Viongozi wa Chama pia walihusishwa. Baada ya kuondoka hii Kamati, mambo yalionekana yanakwenda vizuri. Kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini pia ninaomba Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mabadiliko mazuri waliyoyafanya katika Wilaya ya Kasulu, baada ya kuonyesha kwamba ujambazi katika Wilaya ya Kasulu ulikuwa umekithiri na umekuwa mkubwa sana na kama ulivyokuwa tishio kwa maendeleo ya sehemu zote nchini, pale Kasulu ujambazi bado ni tishio kubwa. Mwezi uliopita nilipokuwa Kasulu, moja ya mambo niliyoshuhudia ni majambazi sasa kuteka magari kwa msululu. Wanayangoja magari yanayokuja yanatoka milimani yanakwenda Kasulu Mjini, wanayateka.

Wanakamata moja, lingine linakuja, wanakamata na wengine wanasimama hapo hapo wala hawana gari wala hawana chochote lakini wanapora mali za wale wafanyabiashara wote, kisha wanakimbia porini  na siyo kwamba pale kuna pori kubwa ambalo linaweza kuwaficha wasifuatwe.

Kwa hiyo, mimi ninachoomba ni kwamba, lazima nguvu za Polisi ziongezwe pale Kasulu ili waweze kushughulikia jambo hili la ujambazi pale Kasulu kwa sababu tatizo ni kubwa sana. Tatizo hili limeendelea na sasa majambazi wameweka Vituo.  Kuna Vituo vya Majambazi sehemu mbalimbali katika tarafa ya Manyovu kule Bukuba, kuna magari mengi yanatoka Kigoma, mengine yanatoka Kasulu, mengine yanatoka sehemu za mpakani. Majambazi pia wanajua kwamba yanayokuja na biashara yanakuja namna gani.  Wakifika pale walipo wanawateka hasa wanapokuwa wametoka kuuza mali zao, maana wanajua ndio wakati wana hela. Hatima yake wengi ndio wanakuwa maskini, wanafilisika kabisa hata hawawezi kufanya shughuli nyingine za biashara.

Lakini baya zaidi ni pale wanapoteka gari halafu wanakimbia Polisi wanawaona hawawezi kufuatilia matukio haya.  Hii imetokea Kasulu, si mara moja wala mara mbili.  Sasa ni lazima tufanye uchunguzi na Wizara itusaidie sana kufanya uchunguzi kama kweli kuna makubaliano kati ya haya majambazi.  Maana majambazi mengine hata yanapokimbia yanakwenda mpakani, wananchi wanahisi tu huwezi kupeleka kesi ya hawa wezi wanaotoka nchi jirani ukaipeleka Polisi wakafuatilia. Maana wakati mwingine wanasema wanawaona. Kwa hiyo, naomba Serikali itusaidie kufuatilia haya mambo yanayofanyika ili tuweze kupata ufumbuzi wa ujambazi huu ambao umekuwa ukiendelea katika Wilaya ya Kasulu.

Jambo la pili ambalo napenda kulizungumzia, ni biashara za mipakani.  Watu wetu wanafanya biashara ndogo ndogo zile za kupeleka ndizi, chumvi, mahindi na maharage, wanapeleka Burundi.  Wale waliofika pale, kile Kituo cha Polisi cha Mnanila wanajua kwamba ni karibu sana na nchi jirani ya Burundi. Kwa hiyo, wanapovusha na wengi wanapopeleka mali zao au wanaporudi mara nyingi wanakamatwa, wanauliza mlikuwa wapi? Wananyang'anywa mali zao, fedha zile walizokuwa wamepata kule wananyang'anywa mipakani.

Sasa mimi nafikiri tumekuwa tukiomba humu ndani kwamba utengenezwe utaratibu wa kuweka masoko katika sehemu zote za mipakani ili watu waweze kufanya biashara za namna hii. Hizi ndizo biashara zitakazowasaidia kuendesha maisha yao.  Vinginevyo hakuna njia. Lakini pili, kwenye hili la ulinzi na usalama, tumekuwa tunazungumza habari za watu wetu wanaouwawa mipakani, wanauwawa na maaskari wa nchi jirani. Tumekuwa hatupati majibu yanayoridhisha sana kiasi kwamba watu wetu sasa hata wakienda Burundi wamekuwa wanapigwa risasi, sisi tunaletewa maiti. Hata tunapoandika, sidhani kama tumekuwa tunapata majibu ya kuridhisha kutusaidia.  Lakini ni vizuri kwa kweli na sisi tukatoa sauti! Serikali ikitoa sauti, mimi nina imani wale wataogopa, hawatakuwa wanaua watu wetu ovyo ovyo.   Kwa sababu wanapokwenda Burundi watu wanapigwa risasi, wanauwawa tu hivi hivi.  Sasa watu wanakuwa hawana amani kabisa.

Kuna wakati mmoja Kijiji kimoja cha Kitambuka na Kibande kule mpakani watu walikimbia Vijiji vyao.  Kwa nini? Kwa sababu Warundi walikuwa wanaingia na bunduki

wanatishia, watu wakakimbia wakaacha mifugo. Mifugo yao ikaibiwa mingi sana! Tukaja hapa tukalalamika, tumekwenda katika mazungumzo haya tukaambiwa hii habari muiache bwana.

Lakini ni vizuri Serikali yetu ikaweka mguu kwa maana ya utaratibu mzuri wa kuwalinda raia na mali zao. Maana hii ndio kazi kubwa ya Serikali. Maana kama amani hakuna, kwa kweli shughuli za maendeleo haziwezi kwenda kama ambavyo mnaona, kama sehemu ya maziwa makuu haitakuwa na amani *perpetually*, haitawezekana Mikoa yote ya pembezoni iweze kupata maendeleo ambayo tunahitaji kuyapata, haitawezekana.

Kwa sababu nchi yetu imekuwa inatumia *resources* nyingi kwa kuhudumia shughuli za wakimbizi, kwa kujihusisha na shughuli za kuleta amani katika sehemu za maziwa makuu na haya tumeendelea nayo na mimi naomba nipongeze juhudi zote ambazo Serikali yetu kwa kweli imekuwa inafanya, imekuwa inajitahidi sana na sisi kwa hili tumepongezwa katika Kikao cha *ACP* kilichofanyika hivi karibuni nchini kwa kweli tulipongezwa na Rais wetu alipongezwa sana kwa jitihada anazofanya kwa ajili ya *FNLA* kuweza kupatana na wenzao ili amani iweze kupatikana. Mimi Mjumbe wenu na kwa kweli nilisema pindi amani itakapopatikana kutakuwapo na mashirikiano makubwa kati ya nchi yetu na nchi ya Burundi, Rwanda na Uganda. Kwa kweli jitihada za nchi yetu huko nje, wenzetu wamekuwa wanazitambua sana.

Mwisho, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Askari wote wa Wilaya ya Kasulu na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla ambao wamekuwa wanafanya kazi ya kuwahudumia wananchi. Askari wetu kwa kweli pale Kasulu hawalali, wamekuwa wanafanya kazi kubwa sana. Lakini wapo wachache ambao bado sio wazuri. Wako maaskari wengine tumewahamisha kutoka Kituo kimoja kwenda kingine kwa tuhuma za kuwanyang’anya watu mali, kwa tuhuma za kuwapiga watu, lakini huko nako walikohamia wameendelea kuwapiga watu na kuwatukana. Mimi sidhani kama hii ndio kazi ya Polisi na labda ni upungufu wa maadili unajitokeza kwa baadhi ya Askari wetu. Sisemi ni wote, lakini kwa baadhi ya maaskari wetu ndani ya Jeshi la Polisi na naomba hao waendelee kushughulikiwa na Serikali yetu kwa kweli wasichafue sifa ya Jeshi letu la Polisi. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, nachukua nafasi hii kumpongeza Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kigoma. Amekuwa anafanya kazi kubwa, nzuri na ya kuaminika, lakini kila anayefanya kazi nzuri hakosi maadui. Ziko tuhuma ambazo tunasikia huyu anatuhumiwa katika sehemu mbalimbali, lakini ni kwa sababu sisi tunaoishi naye tunajua na kwa kuwa yeye anasimamia haki za wananchi. Amekuwa anasimamia haki za wananchi katika Mkoa ule na wako wasiopenda, wale ambao wamekuwa wanajihusisha na uovu, ndio wamekuwa hawapendi jinsi anavyofanya kazi yake vizuri. Lakini mimi kama mwakilishi wa wananchi, ninaomba nimpongeze sana na nilipongeze kwa ujumla Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru sana na niunge mkono hoja ya Kamati ya Ulinzi na Usalama. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Leonard Derefa hajaanza kusema, namwomba Mwenyekiti Anne Makinda, anipokee Kiti.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti.*

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu ya Kamati ya Ulinzi na Usalama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nilitaka niongelee suala la Ukimwi. Sasa hivi Ukimwi katika nchi yetu hasa katika Mkoa wetu wa Shinyanga na hasa Mji wa Shinyanga, unazidi kukithiri sana. Lakini cha kushangaza ni kwamba mwaka jana tulikuwa tunaomba kwenye Bajeti karibu milioni 500, lakini hela zilizotolewa tukapewa Shilingi milioni 24 tu. Sasa hii vita kama hatupewi vitendea kazi, tutaweza vipi kupigana? Kwa bahati nzuri nimejaribu kufuatilia *TACAIDS* wanasema kwamba, walikuwa bado wanaandaa utaratibu kwa kuteuwa *Agents* ambao tutakuwa tunafanya nao kazi kwa kushirikiana na Maanispaa yetu. Lakini kazi hii imecheleshwa sana kiasi kwamba vita hii itatushinda na watu wetu wanaendelea kufariki na fedha hazipatikani.

Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali ihakikishe kwamba kama ni vita, tunapewe vitendea kazi, hela za kutosha tulizokuwa tumeomba ili kusudi *NGO* zinazojihusisha na kazi hii ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilitaka niliongelee kwa kifupi hapa ni suala la Chakula. Kutokana na hali mbaya ilivyojitokeza, mwaka huu mvua zilianza kunyesha vizuri sana na tukategemea kwamba hali itakuwa ni nzuri. Lakini kwa bahati mbaya mvua zikakosekana karibu kwa siku 40 na kwa hiyo, mazao yote yamekauka. Kwa hiyo, tutakuwa na upungufu mkubwa wa chakula katika Mkoa wetu na hasa kwenye Jimbo langu la Shinyanga Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka iliyopita, Serikali iliwatuma kwenda kufanya tathmini katika Wilaya mbalimbali. Lakini kwa mfano Wilaya yangu ya Mjini haikupewa chakula cha msaada, badala yake majirani zangu wenyewe walipewa chakula cha msaada lakini sisi tukawa hatumo. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali katika suala hili inapofanya utafiti wa upungufu wa chakula, ielewe kabisa kwamba na sisi Shinyanga Mjini hatuna. Maana yake na sisi huwa tunalima, lakini mvua zisiponyesha za kutosha kwa kweli tunakuwa tuna matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, naomba tusisahauliwe.

Mara nyingine niliwahi kuomba hapa kwamba kama jina la Mjini ndio linalotuponza, tungeomba Majimbo ya Mjini yaitwe majina kwa mfano mimi niliomba kama Shinyanga Mjini ndio balaa, kwa sababu wanafikiri kwamba watu wa Mjini ni matajiri, basi Jimbo kama hilo liitwe labda Jimbo la Kizumbi, kwa sababu hata wakati mwingine tulikuwa tunaomba. Mkiomba kwa wafadhili, wanasema kwamba wa Mjini hatuwasaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nililotaka niliongelee ni suala la usalama katika nchi yetu. Ni kweli mimi napenda niseme tu kwamba napenda kwa kweli niwapongeze Polisi wa Mkoa wetu wa Shinyanga hasa *RPC*. Shinyanga tulikuwa na matatizo makubwa sana, lakini Polisi wamejitahidi kufanya kazi nzuri na sasa hivi hali sio mbaya na mambo mabaya tunayasikia katika Mikoa mingine. Ninaomba Serikali iendelee kusaidia katika kupambana na ujambazi kwa sababu ujambazi huu unawafanya watu wanaishi kwa hofu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo ni kwamba Polisi hawatoshi na nchi yetu ni kubwa na wakati mwingine hawana vitendea kazi, hawana magari. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, kwa nyakati hizi za amani kama itabidi hata Wanajeshi wa *JWTZ* na wenyewe wasaidie katika kukabili suala hili kama walivyofanya Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nililotaka niliongelee ni suala la mauwaji ya vikongwe. Mauwaji ya vikongwe katika Mkoa wetu na katika Mikoa ya jirani kwa kweli yanatisha, taarifa ambazo zinatolewa ni kwamba wakinamama wengi sana wanauwawa. Lakini katika nchi nyingi, hata mtu mmoja akifa kutakuwa na *inquest*. Hivi Serikali kweli tumelishindwa hili tatizo?

Nilikuwa naomba Serikali ijiweke sawa na ijaribu kulikabili tatizo hili kwa sababu pamoja na kwamba mimi ninatoa msukumo, vile vile linanipa balaa. Ni kwamba, makabila mengine mtu anapokuwa mzee anapata heshima. Wachaga wanawaabudu wazee wao. Lakini sisi sijui ni tatizo gani! Lakini utakuta kwamba Wachaga wanakwenda kwa wazee wao wanatemewa mate wanajipaka mate ya wazee wao kama baraka. Lakini sisi tunaangamiza wazee wetu. Kwa kweli hii inatupa aibu sana na nilikuwa naiomba Serikali itumie nguvu za kila aina itusaidie katika kuondokana na balaa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilitaka niliongelee kwa haraka haraka ni suala la wafungwa. Kuna tatizo moja kwamba, kesi nyingi haziishi mapema. Hi ni kwa sababu zamani tulikuwa na utaratibu kwamba mashahidi walikuwa wanapewa hela wanapokwenda kutoa ushahidi. Lakini kwa siku za hivi karibuni utakuta kesi nyingi zinachelewa kuisha kwa sababu mashahidi wanaweza wakaitwa halafu hela hawana za kwenda kuhudhuria kwenye kesi. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali vile vile ijaribu kurudisha utaratibu wa zamani kwamba mashahidi wanaoitwa kwenye kesi wawe wanaitwa halafu wanalipwa mapema gharama zao za kusafiri pamoja na kulala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nililotaka niliongelee ni kwamba, wapiganaji wetu na Polisi wetu lazima wahudumiwe vyema. Kwa mfano mimi nimelalamika katika upande wa Polisi, pale Shinyanga tuna nyumba za matope ambazo zilijengwa kwenye miaka ya 1970 na nyumba hizi nyingine zina vichuguu humo ndani. Lakini kwa muda mrefu sana pamoja na kwamba nimekuwa nikiwasilisha na leo nina miaka kumi Bungeni, lakini hata nyumba moja haijawahi kuboreshwa.

Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali, Jeshi la Polisi nyumba zao angalau zikarabatiwe ama wajengewe nyingine. Halafu wakati mwingine utakuta kwa mfano wengine wanalala kwenye Bwalo. Wakati watu wanakunywa bia, wanakunja virago, mkiondoka wanalala mle. Sasa kwa kweli ni aina mojawapo ya kuwadhalilisha hao Watendaji. Vile vile, Jeshi la Polisi katika Vituo vyangu pale *Old* Shinyanga pamoja na Kizumbi nyumba zao zimeharibika sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara zinazohusika na zitusaidie na sisi angalau hata nyumba chache wawe wanaziboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilitaka niliongelee kuhusu Vituo vya Mafuta ambavyo vinajengwa kihorela. Vituo hivi vya Mafuta vinavyojengwa kihorela kwa kweli lazima vitizamwe na vitizamwe kwa jicho hasa la husuda. Kwa sababu ukitizama Vituo hivi vinavyojengwa holela katika makazi ya watu utakuta kwamba vituo hivi ni vya kuibia mafuta,

*Transit Oil.* Kwa mfano ukienda njia inayotoka Dar es Salaam kwenda Lindi hutaona Kituo chochote kilichojengwa sana, ukipita Mbagala hutaona kingine, lakini hii njia ya kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma utakuta Vituo vingi sana, vingine viko porini tu. Sasa hivi vinauza mafuta kwa watu gani?

Watu wengi wanatuambia kwamba Vituo hivyo vinasafirisha mafuta yale ambayo yameandikwa *Transit*, yanawekwa kwenye malori halafu yanamwagwa kwenye Vituo hivyo halafu yanakuwa yanarudishwa pole pole Dar es Salaam Mjini kwenda kuuzwa. Halafu nilikuwa naomba, watu wa *TRA* wajaribu kutafiti, hivi kwa nini mafuta yanaweza kuwa ghali Dar es Salaam ambapo ni karibu na Bandari halafu yakawa rahisi Morogoro au Musoma? Hata kama yametoka Mombasa. Hii hata hatujiulizi! Kwa hiyo, lazima hili Watendaji wetu walifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nililotaka niliongelee ni suala la usalama katika Maziwa na Bahari zetu. Siku moja niliwahi kuongea hapa nikasema kwamba hivi kuna ubaya gani kwa mfano Mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera, Kigoma, Rukwa na Mbeya, kwa nini hata wale Wakuu wa Mikoa wanunuliwe *boats* ambazo wakitaka kwenda kutembelea vile Visiwa wapate namna ya kwenda kule? Kwa mfano, *Lake Victoria* utakuta kabisa kwamba kuna Visiwa ambavyo vingine vimekaliwa na majambazi waliouwa watu huku ughaibuni huku kwetu, halafu wanakimbilia huko. Nilikuwa naishauri Serikali ijaribu kujitahidi kutatua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nilitaka niliongelee kuhusu Mahakama pamoja na Polisi. Ukienda Ulaya, ukienda America, hela za Serikali zinalipa mtu anayefanya kazi Mahakamani na mtu anayefanya Polisi kwa sababu wao ndio Serikali. Idara hizi zikishindwa kufanya kazi kutokana na upungufu wa fedha, utakuta Serikali haionekani kama inafanya kazi. *In actual fact,* katika nguzo tatu, Bunge tunapotunga Sheria, tunazikabidhi Mahakama na Mahakama inawaambia Polisi kwamba mtafuteni anayevunja Sheria mniletee nije nimshughulikie. Sasa kama watu hawa hawalipwi vizuri, Mahakama hailipwi vizuri, Polisi hailipwi vizuri, kwa kweli wakimkamata jambazi akiwapa visenti, kwa kweli lazima wakati mwingine anaweza kuwaachia majambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja tena mara ya pili. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja iliyotolewa na Kamati ya Ulinzi na Usalama. Kwanza nianze kuwatambua wale ambao wamechangia. Alianza Mheshimiwa Ireneus Ngwatura (k.n.y. Kamati ya Ulinzi na Usalama), Mheshimiwa Anatory Choya, akafuata Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Mheshimiwa Leonard Derefa. Nawashukuru sana kwa yote mliyoyasema. Kama Spika alivyosema, taarifa nzima ya Kamati ya Ulinzi na Usalama hoja zao tumeshazijibu na zimo katika vitabu ambavyo mmepewa kuanzia jana. Kwa hiyo, majibu mengi yamo katika yale majibu yetu ya kitabu ambacho mmepewa jana. Kwa hizi hoja ambazo zimezungumzwa leo, nikianza na Mheshimiwa Anatory Choya amezungumzia kwa kirefu sana habari ya ajira hasa katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, tunavyo vitengo vikubwa vitatu ambavyo vinafanya ajira karibu kila mwaka. Kuna Polisi, Magereza na

Uhamiaji. Polisi na Magereza kwa kawaida nafasi zao zinakuwa nyingi na utaratibu wao wanatangaza. Sio kweli kwamba wanapotaka kuajiriwa Polisi au Magereza wanakwenda mpaka Dar es Salaam kama alivyosema Mheshimiwa Anatory Choya. Nafasi zinatangazwa, kila Wilaya inapata mgao wake kwa Tanzania nzima na vigezo wanapewa kwamba Wilaya fulani mgao wenu ni vijana kadhaa kama ni 20 au 30 na sifa za hao vijana ni kadhaa. Sifa ni hizo hizo kwa nchi nzima. Sifa ya elimu ni *Form Four* kuanzia *division three* na kuendelea na sifa nyingine ni uraia na tabia nzuri.

Kwa hiyo, matangazo yakitoka kwenye magezeti, yanapelekwa mpaka kwenye Ofisi za Ma-*DC* na Ma-*DC*, nao vile vile matangazo haya wanayapeleka mpaka kwenye Kata na kwenye Vijiji. Kwa hiyo, usemi kwamba matangazo hayafiki kwenye Wilaya na kwenye Kata na kwenye Tarafa sijui Biharamlo, lakini kwa kweli katika nchi nzima ndio utaratibu kwa Magereza na kwa Polisi. Vikao vya kuwachuja vinafanyika huko huko kwenye Kata na kwenye Wilaya. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya chini ya Mwenyekiti wa *DC* ndio wanaochuja wale vijana wanaoatakiwa kwa idadi ya hiyo. Wilaya baadaye inapeleka katika Mkoa, Mkoa unaunganisha Wilaya zake zote na sisi kule Dar es Salaam tunaletewa majina kutoka kwenye Wilaya kupitia katika ngazi ya Mkoa.

Sasa tuhuma kwama wanachukuana wao kwa wao, Polisi wanachukua watoto wao, Magereza wanachukua watoto wao, kama kweli linatokea hili, basi lawama isije katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Labda sasa lawama iwe kule kule Vikao vinakochuja kwenye Wilaya chini ya Ma-*DC* kama upendekeo upo. Mimi sitaki kukataa, kama upo basi utakuwa katika ngazi hizo na tutafuatilia. Lakini sisi kule Wizarani tunaletewa majina ambayo yamechujwa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya. Utaratibu huu huu ndio unaotumiwa na Jeshi la wananchi, kama alivyosema mwenyewe, ndio unaotumiwa na Polisi na ndio unaotumiwa na Magereza.

Kwa upande wa Uhamiaji, nafasi zao huwa ni chache na pengine alikuwa anazungumzia kwenye Uhamiaji. Kwa hiyo, hata ukizigawa kwenye Wilaya haina maana. Nafasi 60 au 100 Wilaya ziko zaidi ya 100, sasa utasema kila Wilaya labda ipate nusu mtu, haiwezekani. Kwa hiyo, hawa Uhamiaji, kwa sababu nafasi zao huwezi kuzigawa, mgao ukifika kwenye Wilaya hawa ndio wanatangaza katika magazeti na hawa wanaoomba ndio wanaoitwa kwenye usajili Dar es Salaam kwa sababu nafasi ni chache. Mbele ya safari, kwa sababu tunafungua Vituo vingi vya mpakani kama tukikubaliwa ajira iwe pana, Uhamiaji na wenyewe watalazimika mgao ufike katika kila Wilaya na mchujo ufanyike kwenye Wilaya. Lakini kwa sasa hivi, kwa sababu nafasi ni chache, ndio maana wanaitwa Dar es Salaam.

Polisi na Magereza wanawaita kwenye *interview* Dar es Salaam wale wataalam, nafasi za utaalam. Wakitaka kwa mfano watu wenye *degree* kwa kazi chache za utaalam, hawa ndio wanaitwa kwa *interview* Dar es Salaam. Kwa Magereza na Polisi, nafasi za wataalam ni chache, lakini nafasi nyingine zote kwa kweli shughuli zote zinafanyika katika Wilaya. Kwa hiyo, ningependa kumweleza Mheshimiwa Anatory Choya kwamba hili la kuitwa Dar es Salaam ni Uhamiaji tu kwa sababu nafasi ni chache na Magereza na Polisi kwa zile nafasi za wataalam wanapotaka *graduates* ni chache.

Kuhusu kigezo cha Cheti cha Kuzaliwa, hilo nalo amelilalamikia. Sasa hivi kwa sababu ya utandawazi na maingiliano, sifa ya Cheti cha Kuzaliwa, sifa ya kuhakikisha kwamba wewe ni Mtanzania sasa inatiliwa mkazo kabisa katika Majeshi yetu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nitumie nafasi hii kuwaeleza Watanzania kwamba, sasa Cheti cha Kuzaliwa ni muhimu kabisa, tuviandae mtoto anapozaliwa, anapokuwa mchanga, ni rahisi zaidi kukipata na gharama ni ndogo sana. Ukichelewa pale sasa ndio unakuwa mlolongo mara u-*apply* Uhamiaji uende wapi, uende ukaape Mahakamani, lakini ni vizuri watoto wetu wawe na vyeti vya kuzaliwa. Sasa hivi wala si katika tu Wizara ya Mambo ya Ndani wala sio katika Majeshi, hata mtoto huyu wa sasa anapokwenda *Form Five* watakwambia kwamba anapokuja katika mambo ya kuleta vyeti aje na Cheti cha Kuzaliwa kumthibitisha. Hata anapokwenda Chuo Kikuu na katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika suala la Cheti cha Kuzaliwa, Waheshimiwa Wabunge sasa waelewe kuwa ni njia muhimu kabisa tuwatafutie watoto wetu Vyeti vya Kuzaliwa ili kuwatambulisha wakati tunaandaa taratibu nyingine za vitambulisho vya uraia. Sasa hivi kwa sababu havipo, kwa hiyo cheti cha kuzaliwa ni muhimu watoto wetu wawe navyo. Kwa hiyo, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, Cheti cha Kuzaliwa ni moja ya vitu muhimu ambavyo lazima awe nacho mtoto anapoajiriwa katika Majeshi yetu na sasa hivi wala sio majeshini tu na hata katika Wizara mbalimbali vinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Anatory Choya vile vile alizungumzia suala la Askari wanapokuwa katika *operation* kwamba posho zao zitazamwe. Nataka kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba posho za hawa Askari wanapokuwa katika *operation* kwa kweli zinatazamwa na kwa sababu ya mazingira yao, hata posho zao, *ration allowance* ni kubwa kuliko za Majeshi mengine na Majeshi mengine wanalalamika mbona wenzetu wa Jeshi la Wananchi posho ya *ration allowance* yao ni kubwa? Ni kubwa kwa sababu ya mazingira yao. Wakati mwingine wanatakiwa waache familia zao waende mpakani wakakae mwezi, miezi miwili au miezi sita. Kwa hiyo, r*ation allowance* yao ni kubwa. Kwa sasa hivi kweli haitoshi, lakini wakijilinganisha wao kwa wao nafikiri Jeshi la Wananchi wanapata Sh.60,000/= wakati hawa Polisi Magereza wanapata Sh.28,000/=. Lakini hazitoshi, nakubali. Tunaendelea na mchakato wa kuzihuisha si za Jeshi la Wananchi tu, lakini za Majeshi mengine. Hata juzi kulikuwa kuna swali tulilijibu kwamba; Je, posho za hawa zitahuishwa lini? Zitahuishwa. Hayo yote yanategemea na hali ya uchumi unavyokuwa bora zaidi na posho zao zinaboreshwa.

Kwa hiyo suala la posho kwa askari wetu wanapokuwa katika *operation* maalum linatazamwa kwa mtazamo huo. Kuhusu makazi yao, ni kweli ninapofanya *operation* kule mpakani wanakuwa katika makazi ya muda, hatutegemei kuwe na majengo mazuri katika maeneo ya porini mpakani, lakini tunajitahidi kuwapatia mahema pale inapowezekana.

Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi ametoa shukrani katika Gereza la Kasulu, tunashukuru marekebisho yaliyofanyika. Lakini vile vile amezungumza suala la kupambana na ujambazi katika maeneo yale. Tunakubali kwamba tuongeze nguvu.

Sasa hivi maeneo yote yenye wakimbizi pamoja na nguvu za kawaida za Polisi lakini tumeongezea nguvu ya ziada ambayo tunakusanya Askari katika Mikoa yote kuwapelekea kule.

Baada ya miezi sita, lile kundi linarudi na tunapeleka kundi lingine, kwa sababu ya kuona hali halisi ya mazingira ya Mikoa ile ya Kagera na Mkoa wa Kigoma, ndio Mikoa miwili ambayo imeongezewa nguvu za Polisi kuliko Mikoa mingine kwa sababu ya tatizo la mpaka wao si shwari, kutokana na matatizo ya wakimbizi na hili zoezi tunaendelea nalo kwa kushirikiana na *UNCCR*. Kwa hiyo, kila baada ya miezi sita tunapeleka Polisi wa nyongeza kwa sababu ya matatizo yale.

Mheshimiwa Mbunge ametushauri tuongeze nguvu zaidi. Tutatazama uwezo wetu wa kuongeza nguvu zaidi kwa sababu tunakubali kwamba maeneo yale kwa sababu ya wakimbizi na vurugu za mpaka inatakiwa nguvu ya nyongeza. Kwa hiyo, Polisi tunao wa nyongeza pale. Jeshi la Wananchi vile vile linayo *detachment* (viteule) katika maeneo yote yale ya mpaka na Kamati ya Ulinzi na Usalama tunashukuru imeshavitembelea karibu viteule vyote katika mpaka ule. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi suala la kutazama kuongeza nguvu katika eneo hilo tunalo, tutalishughulikia kulingana na hali halisi ilivyo.

Vile vile, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi amezungumzia suala la biashara za mpakani. Sisi kwa upande wa Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa yale maeneo ambayo Halmashauri za Wilaya wanakubaliana na mamlaka za nchi za jirani waweke masoko, tunatoa idhini. Sasa hivi ukienda pale Holo Holo utakuta wameweka taratibu, pale Holili wameweka utaratibu kwamba siku fulani soko liko Tanzania.

Kwa hiyo, wale Wakenya wanakuja Tanzania kwa wenzao kwenye soko, hatuwaulizi *passport,* wala nini, wala *visa,* wanafanya biashara. Siku fulani soko liko upande wa Kenya hawa Watanzania na wenyewe wavuka pale Holili wanakwenda Kenya hatuwaulizwi *passport,* wala nini kwa sababu ni taratibu tu ambazo tumekubaliana na ndivyo ilivyo katika mipaka yetu yote.

Mpaka wa Magharibi kwa sababu ya vita vya wenyewe kwa wenyewe ndio maana utaratibu huu Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi haujakamilika. Lakini nina hakika kabisa hali ikitulia, huu utaratibu unaofanywa katika maeneo mengine ya mipaka mingine vile vile tutautumia kwa upande wa mpaka wetu na Burundi na Rwanda.

Mheshimiwa Mbungepia amezungumzia suala la raia wetu wanaouwawa kule mpakani. Ni kweli kwa sababu ya hali ya kule, kulikuwa na vurugu, kuna mapigano ya wenyewe kwa wenyewe na Askari na wale waasi wanavuka mipaka. Vurumai hiyo ndiyo iliyosababisha baadhi ya matatizo ambayo ameyasema kuwa wananchi wetu wengi, wamepoteza maisha kule. Tunasikitika, lakini jawabu la hili ni hizi nchi za Burundi na Rwanda kuacha mapigano, zitulie na sisi ndipo tutakapotulia. Kwa wakati huu tunachofanya ni kuweka Askari wetu kule mpakani kulinda mpaka wetu, kulinda watu wetu. Lakini jawabu la kweli kabisa ni pale ambapo mapigano yatakwisha Burundi, amani itapatikana Burundi na sisi ndio tutapata amani ya kweli katika maeneo haya.

Ametoa pongezi kwa *RPC* wa Kigoma, tunashukuru. Mara chache sana tunapokea pongezi. Wizara ya Mambo ya Ndani ni Wizara ya lawama, tunapokea pongezi chache sana kwa mbali. Kwa hiyo, zinatufariji, tunashukuru. Lakini hao wachache ambao amewasema kwamba bado wanaokiuka maadili ya kazi zao, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Waheshimiwa

Wabunge, tupeni taarifa tu. Sisi kwa kweli hatuna huruma wala msamaha kwa Askari wanaokiuka maadili ya kazi zao. Tunatoa wito kwa wananchi kwa ujumla tupeni taarifa ya Askari wenye tabia mbovu, wanaowasumbua huko kwa mambo mbalimbali, ili tuweze kuwashughulikia. Sisi kama Wizara hatuna huruma wala msamaha kwa Askari wa namna hiyo.

Mheshimiwa Leonard Derefa, amezungumzia mambo mengi ya Ukimwi. Nataka nimwarifu tu kwamba tayari zile *NGO* za kutushauri, *consultancy* wale wameshateuliwa juzi kwenye magazeti wameorodheshwa. Kwa hiyo, watakuja watasaidiana na sisi katika kuweka taratibu, kuweka mipango *(action plans)* za Wilaya mbalimbali ili *action plans* hizo tuzitumie sasa kwenda kuomba hela *TACAIDS*. Kwa hiyo, nadhani hili tayari limeshughulikiwa.

Hali mbaya ya chakuka Mheshimiwa Leonard Derefa, sio Shinyanga tu. Wengi tumepata balaa la ukame sehemu za Mkoa wa Tabora, kule kwetu Mkoa wa Singida na hata Wilaya yangu ya Manyoni, hasa Jimbo langu la Manyoni Mashariki ukipita sehemu za Kintinku kule utakuta sifuri kabisa. Sehemu za Mkoa wa Dodoma, sehemu za Mkoa wa Arusha huko Ngorongoro na kadhalika kote wamepata balaa hili la njaa. Kwa hiyo, ni tatizo ambalo limetukumba maeneo mengi.

Nataka tu nimhakikishie kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, pale kuna kitengo cha maafa wakishirikiana na Maafisa Kilimo wa Mikoa na Wilaya sasa hivi wameshaanza kupita kutathmini hali ya ukame ilivyo na athari ilivyo ili Serikali iweze ikaona upana wa tatizo na watusaidie kama ambavyo kila wakati Serikali imekuwa inasaidia maeneo yanayopata maafa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Leonard Derefa Serikali iko na sisi katika yale maeneo ambayo tumepata athari hizi.

Vile vile, Mheshimiwa Leonard Derefa naye ametoa pongezi kwa *RPC* wa Shinyanga. Tunazipokea, tunashukuru sana. Kama nilivyosema, mara nyingi sisi hatupewi pongezi, lakini tunapozipata zinatutia moyo na yeye mwenyewe tutamfikishia. Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba tuangalie utaratibu wa kuongeza nguvu za kupambana na majambazi, ikiwekana tutumie msaada wa Jeshi la Wananchi. Hilo liko ndani ya utaratibu kama alivyosema mwenyewe. Mwaka juzi tulifanya *operation* ya pamoja Polisi na Jeshi la Wananchi kule Mkoa wa Kagera. Kwa hiyo, muda muafaka ukifika hili linawezekana na tuangalie jinsi ya kufanya.

La mauaji ya vikongwe, amesema: Je, Serikali mmeshindwa? Sasa hili tatizo la vikongwe kuuwawa ni tatizo ambalo kwa kweli si la Serikali peke yetu. Kweli Serikali tupo na vyombo vya dola vinafanya kazi, lakini na jamii nzima kwa kweli Mheshimiwa Mbunge naomba tusaidiane kabisa. Vyombo vya dola na jamii nzima, tuendelee kuelimisha watu wetu kule Shinyanga ili tuone kwamba hakuna haja ya kuendelea kuuwana. Mimi naamini tunavyoongeza Shule za Msingi, tunaongeza Shule za Sekondari, tunaongeza huduma za afya, nayo vile vile baadaye italeta matokeo mazuri tu, kwa sababu mengi haya ni ushirikina na ujinga.

Ushirikina na ujinga ndio chimbuko kubwa la haya. Sasa kuyapiga vita haya, vyombo vya dola kweli tumo, lakini vile vile na jamii tuendelee kuelimishana tuachane na hayo. Lakini tarakimu zinaonyesha sasa haya matukio yanapungua. Kwa hiyo, inaonekana kwamba juhudi hizi tukiongeza matukio yatapungua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala kwamba kesi zinachelewa kwa sababu mashahidi hawagharamiwi, ni kweli kesi haiwezi kuendelea kama mashahidi hawakuja na mashahidi kuja ni lazima Serikali iwagharamie kwa maana ya nauli zao na matunzo yao. Sasa wakati mwingine kama hela hazipo, inakuwa ni shida kwenda kuwatafuta mashahidi. Lakini sasa hivi kwa sababu ya utawala bora, tunajitahidi kabisa kutafuta hela za kuwaleta mashahidi.

Vile vile, tunajitahidi kuharakisha upelelezi kwa sababu mashahidi wanaweza kuwepo lakini Polisi wakasema hatujamaliza upelelezi. Tunajitahidi vile vile katika upelelezi sasa uwe unafanyika kwa haraka na hakika.

Hata juzi nadhani Waheshimiwa Wabunge mmesikia kwamba Rais amezindua Maabara ya kisasa ya upelelezi. Ile Maabara sasa itawezesha Polisi kujua nani amefanya kosa kwa muda mfupi iwezekanavyo. Zamani hii *finger print* walikuwa wanatazama kwa jicho tu hivi, mtu mmoja kumchambua vidole kumi inachukua hata masaa mawili. Lakini sasa hivi wamepata *computer* ni sekunde moja, mbili inatoa majibu. Kwa hiyo, yote hiyo tunafanya ili kuweza kuharakisha upelelezi ili tuharakishe kesi huko Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Derefa vile vile alikuwa na tatizo la nyumba. Ni kweli tatizo la nyumba katika nchi nzima ni kubwa na sisi ambao tuko Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni katika mambo ambayo yanatusikitisha sana. Unapopita katika kila Mkoa zile nyumba ambazo ni mbovu kabisa wala huulizi ni za nani. Unajua moja kwa moja ama za Polisi au Magereza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufumbuzi wa hili kwa kweli ni hela tu, ni bajeti. Mnakumbuka tangu mwaka 1994 fedha za maendeleo zilisimama katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, hata Jeshi la Wananchi, karibu miaka kumi. Tunashukuru sana Kamati hii ya Ulinzi na Usalama chini ya Mheshimiwa Mzee Malecela katika mambo ambayo wameyasukuma kwa nguvu zao zote ni kurudisha sasa Fungu la Maendeleo kwa Wizara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wa tatu tu tangu tumeanza kupata hizi hela za maendeleo na sasa tumeshaanza kujenga. Katika miaka hii mitatu tumejenga nyumba za Polisi kule Hai, Kiteto nadhani Wabunge wanaotoka kule wanajua. Chakechake kule Pemba, wanaotoka kule Pemba wanajua, tumejenga Ukonga na juzi tu Jumamosi iliyopita Mheshimiwa Rais amezindua nyumba mpya za Polisi karibu 130 kule Kunduchi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Derefa tumeanza kujenga na huko Shinyanga tutafika tu. Tunachoomba ni kwamba kila bajeti endeleeni kutupa hela za maendeleo ili tubadilishe sura ya nyumba za Polisi ambazo kwa kweli kila Mbunge akisimama hapa atazungumza habari za ubovu wa nyumba za Polisi huko anakotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Vituo vya Mafuta kujengwa holela, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge inalishughulikia na mamlaka zinazohusika zimeshaelezwa ili zifanye marekebisho.

Vile vile, amezungumzia suala la usalama majini kwamba Ma-*RC* na Ma-*DC* katika maeneo ya Maziwa wapate boti. Tatizo la hili ni gharama. Lakini sasa hivi nataka kulieleza

Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge katika mambo ambayo sasa hivi wanayasimamia kwa karibu sana ni kupatikana kwa boti kwa ajili ya Polisi na Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wakipata boti, Mkuu wa Mkoa anapotaka kusafiri kwenda kwenye Kisiwa fulani na yeye mwenyewe ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa wake, yeye ni kutoa taarifa tu kuwa nataka kwenda mahali fulani atapelekwa. Kwa hiyo, tukitatua tatizo la hizi boti za Polisi na Jeshi la Wananchi tutakuwa vile vile tunatatua tatizo la Ma-*DC* na Wakuu wa Mikoa wanapotembelea maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa sababu katika kipindi hiki wameleta mabadiliko makubwa sana katika vyombo vyetu. Jinsi walivyotukuta mwaka 2000 si jinsi watakavyotuacha mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jeshi la Wananchi, vifaa vingi ambavyo walikuwa hawana kwa sababu ya Kamati hii kupigania sana, sasa hivi Jeshi la Wananchi tumeanza kupata zana mbalimbali, wameshaanza kujenga nyumba katika *barracks* mbalimbali kwa sababu ya msukumo wa Kamati hii. Katika Wizara ya Mambo ya Ndani, vile vile, asubuhi hapa mmesikia kwamba karibu sasa Ma-*RPC* wote wana magari mapya, Ma-*OCD* wanapata magari mapya. Yote hiyo ni juhudi ya Kamati hii na ninyi Bunge hili.

Juzi juzi hapa Mheshimiwa Rais amezindua mtambo wa kisasa wa mawasiliano wa Jeshi la Polisi ili kukabiliana na majambazi ambayo yenyewe yana mawasiliano makubwa. Yote hii ni juhudi ya Kamati hii na Bunge hili. Hata kule Magereza, juzi mmesambaziwa hapa Taarifa ya Haki za Binadamu wakisema Magerezani hali ni mbaya sana, lakini kwa kweli katika kipindi cha miaka mitano Bunge hili kupitia Kamati yenu ya Ulinzi na Usalama tumebadilisha sana hali ya Magereza. Sasa hivi Magereza chakula wanachokula ni bora zaidi kuliko wakati wowote huko nyuma. Magereza sasa wanavaa suruali na shati, wanaonekana kama ni binadamu badala ya vikaptura.

Magereza yote sasa wanalalia magodoro. Sasa hivi wanapata haki ya kupata habari, Magereza yote sasa yana *radio* wanasikiliza taarifa za habari na katika Magereza makubwa sasa tumeanza kupeleka *television*. Haya yote Waheshimiwa Wabunge mmeyafanya ninyi kupitia Kamati ya Ulinzi na Usalama na tutakuwa wachoyo wa wafadhila kama hatatushukuru Bunge hili kwa mabadiliko makubwa kabisa ambayo mmefanya katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wale wote waliopaswa kuchangia hoja ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, wamehitimisha. Sasa nitawahoji.

*(Hoja iliamuwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo yaliyomo Katika Taarifa ya Kamati ya Ulinzi naUsalama kwa Mwaka 2003 na Mwaka 2004 yalikubaliwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi.

**WABUNGE FULANI:** Mtera!

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti ama Makamu wake au mtu mwingine.

**WABUNGE FULANI:** Mtera wote!!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, itabidi tuahirishe Kikao. Hata hivyo dakika zake thelathini zilikuwa hazitoshi. Kwa hiyo, naahirisha Kikao mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.37 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa Mwaka 2003**

.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, asubuhi tulikuwa tujadili Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, sasa taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira imeunganishwa na ya mwaka 2004 kwa hiyo itaondoka hapa.

Taarifa ya Mambo ya Nje pia imeunganishwa na Taarifa ya mwaka 2004 kwa hiyo, kutakuwa na mabadiliko haya. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi au mwakilishi wake.

**MHE. JOEL N. BENDERA (k.n.y MWENYEKITI KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 88(11) ya mwaka 2003 ya Kanuni za Bunge, naomba kutoa taarifa ya shughuli za Kamati ya Kilimo na Ardhi kuishia Januari 2004, lakini kabla sijaanza kutoa taarifa yangu nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha mwaka 2004 na tunaendelea kumwomba Mungu ili atuepushie na mabaya yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ni mojawapo ya Kamati 13 za Kudumu za Bunge na imeundwa rasmi mwaka 2003 baada ya kuvunjwa Kamati za Kisekta. Kamati ni ya Kipotifolio na inashughulikia Wizara za Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati hii yameainishwa kwenye Kanuni Namba 103A(2) ya mwaka 2003 na yanatajwa kama ifuatavyo:-

Moja, kushughulikia Bajeti za Wizara hizo, pili, kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa na Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo.

Nne, kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni 103A(1) ya mwaka 2003 Kamati hii ilikuwa na Wajumbe wafuatao:-

Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa, John Singo, Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Philip Magani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizofanywa na Kamati, Kamati hii ilianza kazi zake rasmi mwezi Machi, 2003 kwa kupokea taarifa kuhusu majukumu ya Wizara zilizounda Kamati hii pia wakati huo huo Kamati ilipata nafasi ya kujielimisha juu ya shughuli za Mashirika ya Umma na asasi zilizomo chini ya Wizara hizo.

Kwa nyakati tofauti Kamati ilikutana na Mawaziri na Wataalam wa Wizara husika kwa lengo la kufahamiana na kujulishwa kuhusu Wizara hizo. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri na Watendaji wote kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa kwa Kamati yetu. *(Makofi)*

Aidha, shughuli zilizofanywa na Kamati Kiwizara ni kama ifuatavyo:-

Moja, Wizara ya Kilimo na Chakula, ziara mkoani Mbeya. Tarehe 6 Agosti, 2003 mpaka tarehe 9 Agosti, 2003 Kamati iliwakilishwa na Wajumbe watano wakitembelea maonyesho ya sherehe za nane nane zilizofanyika Kitaifa Mjini Mbeya.

Mbili, Taasisi ya Utafiti wa Minazi Mikocheni, Kamati ilitembelea Taasisi hii ili kwenda kuona shughuli za utafiti zinazoendelezwa na Taasisi hiyo, Taasisi kwa sasa inafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani na *Irish Development Agency* ambapo Serikali ya Ujerumani inasitisha ufadhili wake mwezi Desemba, 2004 na baada ya hapo itabidi Serikali yetu iiendeshe. Wajumbe waliona uzalishaji wa minazi na mimea mingine mbalimbali kwa teknolojia ya kisasa ambapo mimea imezalishwa kwa kutumia vikonyo *micro propagation* kwa mimea husika.

Tatu, Kiwanda cha Sukari Kilimbero na wakulima wadogowadogo wa miwa. Kampuni hii ilibinafsishwa kwa wawekezaji wa *Ilovo Sugar Limited* na *E&F Man* kwa asilimia 75 ya hisa tangu mwaka 1998. Hisa asilimia 25 zinamilikiwa na Serikali ya Tanzania, tangu Kampuni hiyo ibinafsishwe uzalishaji wa sukari umeongezeka sana kutoka tani 29,517 mwaka 1997/1998 hadi tani 98,412.65 kwa mwaka 2000/2003.

Kampuni imewawezesha wakulima wadogo wadogo *(Out growers)* kuongeza uzalishaji wa miwa kutoka tani 95,753 mwaka 1997/1998 hadi kufikia tani 245,105 kwa mwaka 2002/3 ambazo kwa msimu wa mwaka 2002/2003 ziliwapatia wakulima hawa wadogo wadogo bilioni 4.1. Kamati imefurahishwa sana na kazi nzuri iliyofanywa na Mwekezaji huyo pamoja na kuweka miundombinu ya kisasa kwenye mashamba ya wakulima wadogo wadogo. Kampuni imekuwa ikiwapatia misaada ya kitaalam kwa kilimo bora cha miwa. Kiwanda kiko karibu na wananchi wanaokizunguka na kinasaidia katika shughuli za kimaendeleo za wananchi hao.

Kuhusu Kiwanda cha Sukari Mtibwa na mashamba ya wakulima wadogo, Kampuni hii inaendeshwa na wawekezaji binafsi na tayari mitambo ya kuzalisha sukari imekwisha karabatiwa, kampuni ina uhusiano mzuri na wakulima wa miwa wadogo wadogo wanaoizunguka yaani *out growers* ambapo huwapatia utaalam na mbegu za miwa kwa bei nafuu. Kutokana na uhusiano na huduma hizo wakulima wadogo wadogo wameweza kuongeza uzalishaji wa miwa toka tani 120,124 kwa mwaka 2000/2001 hadi tani 207,854 mwaka 2001/2002. Kampuni imeweka miundombinu endelevu ndani ya mashamba yake ya miwa na hata kwenye maeneo ya wananchi wanayozunguka mashamba hayo.

Aidha, kampuni inatoa huduma za jamii kama vile kuchimba visima vya maji, kutengeneza barabara, kusaidia shule za msingi na moja ya sekondari, pia kiwanda kinaendesha kituo cha watoto wadogo.

Tano, tulitembelea Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Mlingano, tarehe 20 hadi tarehe 21 Januari, 2004, Taasisi ilianzishwa mwaka 1934 kama Taasisi ya kutafiti zao la Mkonge Kitaifa na ilikuwa chini ya Wakulima wa Mkonge Tanganyika. Mwaka 1972 Taasisi iliongezewa jukumu la kuratibu utafiti wa udongo Kitaifa kwa sasa kituo hicho pamoja na kufanya utafiti kwa zao la Mkonge pia inafanya tafiti zinazohusu mazao ya nafaka, mikunde, minazi, korosho na mbegu za mafuta.

Sita, Chuo cha Kilimo *(Agro Mechanization)* Mlingano tarehe 21, Chuo hiki ambacho kiko katika eneo la kituo cha utafiti wa Mlingano kinatoa mafunzo ya Stashahada, *Diploma* ya Kilimo cha Matrekta *Agro Mechanization* pamoja na kutoa mafunzo hayo kwa wanachuo lakini pia kinatoa mafunzo hayo kwa wanakijiji walio jirani na Chuo hicho. Wanafunzi pia wanahusishwa kutoa mafunzo kwa wakulima vijijini kama sehemu ya mafunzo yao kwa vitendo.

Chuo pia hutoa mafunzo ya kozi fupi katika fani za uzalishaji mazao, ufugaji, utumiaji na utunzaji wa matrekta, utunzaji wanyama kazi na uongozi. Chuo pia kimekuwa kikiendesha kozi fupi fupi za rejareja kwa Maafisa Ugavi kutoka Wilaya mbalimbali Tanzania Bara.

Saba, Mashamba ya wakulima wadogo wa Katani, Mweria. Tulitembelea huko tarehe 21 Januari, 2004 mashamba hayo ambayo yako Wilaya ya Korogwe yanamilikiwa na Kampuni ya

*Katani Limited,* kutokana na uhaba wa ardhi kampuni hiyo iliamua kuwaazima wananchi waliozunguka maeneo ya kulima. Pamoja na kupanda zao la biashara yaani katani wananchi hao wanapanda mazao mengine kama vile mahindi, maharage, kunde na kadhalika katikati ya mraba wakati katani ikiwa changa. Wakulima hao waliomba wapatiwe hatimiliki kwa mashamba hayo ambayo walieleza kuwa Kampuni ya *Katani Limited* wako tayari kuwaachia mashamba hayo.

Nane, kuhusu shamba la Katani Gomba. Shamba hilo ambalo linamilikiwa na *GAI Limited* liko Wilaya ya Korogwe na moja ya mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na Mamlaka ya Mkonge Tanzania. Shamba lilikabidhiwa kwa mmiliki binafsi mwaka 1998, Januari.

Shughuli muhimu ambazo mwekezaji amezifanya ni kukarabati mitambo na mashine za kusaga mkonge, kupanda miche mipya ya kupanua mashamba, mwenye shamba alielezea kuwa hadi sasa amekwisha panda zaidi ya hekta 1067 za mkonge mpya ambapo alitarajia kuwa angepanda zaidi ya hekta 1215.25 ifikapo Desemba, 2003. Kampuni inajishughulisha pia na Huduma za Jamii ambapo huduma zifuatazo hutolewa na kampuni hiyo. Huduma za Afya zinatolewa bure kwa wafanyakazi na wanavijiji wanaozunguka shamba hilo, gari la kubebea wagonjwa mahututi hadi Hospitali ya Wilaya, huduma ya maji safi kwa wafanyakazi wanakijiji, shule ya msingi pamoja na mikopo ya elimu kwa wafanyakazi ili watoto hao waweze kusoma hadi sekondari.

Pia Kampuni ni mlezi wa shule za msingi Mtarawanda, Gomba, Mwenga na Chepete, ukarabati wa barabara na madaraja ili kurahisisha usafiri, mwekezaji huyo aliomba apatiwe hatimiliki ya shamba hilo kwa vile bila hati hiyo anashindwa kupata mikopo benki ya kuendeleza mashamba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Seriani Arusha, tulitembelea huko tarehe 23 Januari, 2004. Taasisi hii ilianzishwa mwaka 1970 baada ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Canada kusaini mkataba wa kuanzisha mradi wa kuboresha uzalishaji wa zao la ngano uliojulikana kama *Tanzania-Canada Wheat Program.* Seriani ni Makao Makuu ya Utafiti Kanda ya Kaskazini, Kanda inahusisha mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Wilaya ya Lushoto na Muheza katika Mkoa wa Tanga.

Kanda inavyo vituo vya utafiti viwili ambavyo ni Taasisi ya Utafiti Seriani na Taasisi ya Utafiti wa Mboga, Matunda, Maua na Viungo Tengeru, Taasisi ina eneo la hekta 769 ambalo linatumika katika shughuli za utafiti na pia kuzalisha mbegu mama kwa ajili ya Taifa zima. Mwaka 1992 mradi wa *Tanzania-Canada Wheat Program* ulimaliza mkataba wake na ndipo kituo kikaongezewa mazao mengine kuyafanyia utafiti. Mazao hayo ni Mahindi, Maharage, Shayiri na Mazao mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafadhili wakubwa wa Taasisi hii ni Serikali ya Tanzania, Mradi wa Utafiti wa Kilimo Tanzania awamu ya pili *TAPRP,* Mfuko wa kanda wa utafiti wa kilimo *(NZRARPF),* Makampuni ya Mbegu na Madawa na Taasisi na mitandao ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliopo ni kuwa tangu mwaka 1975 hadi sasa Taasisi imetafiti na kutoa mbegu bora za ngano aina 13, aina 4 ya mbegu za Shayiri, aina 5 ya mbegu ya Maharage na aina 9 za mbegu za Mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna matatizo, pamoja na kuwa eneo walilopewa awali halikuwa linatosha limepunguzwa zaidi ili kutekeleza agizo la Serikali la kutoa hekta 150 kwa ajili ya upanuzi wa uwanja wa ndege wa Arusha.

Kumi, Taasisi ya Utafiti wa Mboga, Matunda na Maua *(Horticulture)* Tengeru tulitembelea huko tarehe 24, kituo hiki kilianzishwa mwaka 1980 kutokana na ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uholanzi, lengo la mradi ni kufanya utafiti wa mazao ya mbogamboga *Horticultural Crops* ili kuimarisha afya za Watanzania kutokana na lishe bora, kuwaongezea kipato, kuhamasisha uwepo wa viwanda vya kusindika vya Mazao ya Kilimo pamoja na uhakika wa chakula wakati wote. Kituo kinalo eneo la hekta 235 ambalo limegawanyika katika maeneo madogo madogo likiwemo eneo la miti, miche mama na maeneo ya kufanyia utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli  zinazofanywa na Taasisi hii ni pamoja na haya yafuatayo:-

Kufanya uchunguzi wa aina ya mazao ya mboga na maeneo yanayofaa kuzalisha mbegu za mboga, kuanzisha mpango mahsusi wa uzalishaji wa mbegu bora za mboga nchini, kuhifadhi aina mbalimbali za mboga, kuzalisha mboga za awali na msingi, kusimamia ubinafsishaji wa shughuli za uzalishaji wa mbegu za mboga, kuusimamia ubinafsishaji wa shughuli za uzalishaji wa mbegu bora kibiashara, kusimamia na kutoa ushauri juu ya uzalishaji wa mbegu za mboga katika ngazi ya mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio, utafiti uliofanyika kwa mbegu mbalimbali zikiwemo mbegu bora za machungwa, ndizi, nyanya, maparachichi, bamia, kabichi, papai, *African night shaitts,* vitunguu pia Taasisi ilipanda miti mama ya miembe, migomba, *citrus species,* makadamia, ngogwe, figiri, mnavu na kadhalika.

Aidha, tafiti hizo zinazohusisha aina ya mbolea kwa mboga mbalimbali, makampuni mawili ya kuzalisha mbegu kibiashara zilizothibitishwa na kituo hiki *Alfa Seed* na *Incofin* yalianzishwa kwa watu binafsi kwa kushirikiana na Serikali. Zaidi ya wakulima wa mkataba 200 wamefundishwa jinsi ya kuzalisha mbegu bora, kuanzisha na kusimamia kikamilifu uzalishaji wa mbegu za mboga katika vijiji zaidi ya 70 vilivyo katika Wilaya 12 za mikoa ya Morogoro, Dodoma na Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba 11 ni kuhusu shamba la mfano la migomba ya mbegu bora Tengeru, tulitembelea huko tarehe 24 Januari, 2004. Shamba hilo linapanda migomba kwa kutumia miche iliyoendelezwa na kituo cha utafiti cha Tengeru, ndizi zinazotokana na migomba hii ni zile zinazohitajika katika soko la Kimataifa.

Narudia, ndizi  inayopatikana katika migomba hii ni zile zinazohitajika katika soko la Kimataifa, ikitunzwa vizuri zaidi migomba hii ina uwezo wa kuzaa mikungu 1,111 kwa hekta kwa mwaka.

Kumi na mbili, ni kuhusu duka la shamba la mfano la umwagiliaji, tulitembelea huko tarehe 24 Januari, 2004. Duka hili ambalo linamilikiwa na *BAACON TANZANIA* linajishughulisha na uuzaji wa vifaa vya umwagiliaji sifa ya vifaa hivi kwa kutumia maji kwa uangalifu kwa matokeo mazuri, wajumbe walionyeshwa shamba la mfano ambalo linamwagiliwa kwa kutumia *Micro Drop Irrigation* ambapo uwezo wake ni kumwagilia shamba la hekta moja hadi nne kwa mazao mbalimbali.

Namba kumi na tatu, Kituo cha *Asian Vegetable Research Development Centre, Regional Centre for Africa.* Kituo hiki kiko Arusha Duruti na tulitembelea huko tarehe 24 Januari, 2004. Kamati ilitembelea kituo na kupata maelezo kuhusiana na shughuli zinazofanyika hapo, kituo hiki chenye makao yake makuu nchini Taiwan kilianzishwa hapa nchini mwaka 1992. Kituo kiko jirani na Kituo cha Utafiti cha *Horticulture,* Tengeru, lengo la kituo ni kufanya utafiti wa kuwaongezea lishe na kipato watu maskini katika nchi zinazoendelea kutokana na kilimo bora, mauzo hifadhi na usambazaji wa mazao ya mbogamboga, mboga zinazofanyiwa utafiti katika kituo hiki ni pilipili, vitunguu, kabichi, nyanya na bamia na kadhalika.

Namba kumi na nne, shamba la maua *(Tengeru Flower Limited),* tulitembelea huko tarehe 25 Januari, 2004. Shamba hilo ambalo linamilikiwa na Mtanzania linazalisha maua kwa ajili ya soko la nje na hivyo linachangia katika kuiletea nchi fedha za kigeni, shamba huzalisha aina sita za maua ya aina ya waridi *(Roses),* uzalishaji wa maua umeongezeka na kufikia vikonyo milioni 6,750,000 Juni, 2002 kutoka vikonyo 6,441,790 mwaka 2001. Shamba hili huajiri wafanyakazi wa kudumu 136 ambapo kati ya hao 80 ni wanawake na 56 ni wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shughuli za uzalishaji shamba pia hujihusisha na shughuli za maendeleo ya wananchi kama vile shamba limeshirikiana na wananchi kuleta maji safi kwa wananchi, kujenga zahanati ya kisasa na kijiji, tulipitiapitia pia tukaona shamba la Mheshimiwa Felix Mrema. *(Makofi)*

Namba kumi na tano, Taasisi ya Utafiti wa zao la Kahawa *(Tanzania Coffee Research Institute)* Lyamungo tulitembelea huko tarehe 25 Januari, 2004. Taasisi ilianzishwa mwaka 1930 na wakulima wa kahawa wa kizungu, jukumu la kituo hiki kama ilivyo sasa ilikuwa ni kutafiti miche bora ya kahawa ambayo imezaa sana na kuvumilia magonjwa baadaye kituo kilichukuliwa na Serikali ya Tanzania chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula na hivyo kuendeshwa kwa ruzuku toka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2000 kituo kilirudishwa ili kiendeshwe na wakulima wenyewe na kuanza kisheria Septemba 2001, lengo la kituo ni kutoa huduma muhimu kwa wadau ambao ni wakulima wa kahawa nchini kwa kuwapatia teknolojia muafaka inayofaa na kutekelezeka na ushauri kuongeza sifa na ubora wa kahawa. Jukumu la *TACRI,* kwa sasa ni kubainisha aina ya kahawa inayotoa mavuno mengi na isiyoshambuliwa na *CRL* au *CDD* pia yenye matunda makubwa na muonjo mzuri na kustawi vizuri kwenye maeneo tofauti yanayozalisha kahawa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi inamilikiwa na wadau ambao ni wazalishaji wadogo wadogo na wakulima wa kahawa Vyama vya Ushirika vinavyohusika na uzalishaji wa kahawa,

wasindikaji wa kahawa, wafanyabiashara wa kahawa, asasi zisizo za Kiserikali, Sekta Binafsi na Serikali.

Kuhusu mapato, Taasisi ya *TACRI* inapata mapato yake kutokana na michango ya wanachama wake kupitia ushuru, michango ya Serikali na wafadhili, shughuli za kushirikiana pamoja na mauzo ya nyenzo za huduma.

Namba kumi na sita, ni kuhusu shamba la Kombo la miche bora ya kahawa la mtu binafsi Ndugu Kishumbua, Lyamungo, tulimtembelea Mzee Kishumbua na familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu Kishumbua na familia yake wanapanda miche bora iliyotafitiwa na Kituo cha Utafiti cha Lyamungo na hivyo amekuwa mkulima wa mfano kuonyesha faida ya miche bora ameanza kupanda miche bora mwaka 1999 na kutokana na ubora wa kahawa anayoilima mwaka 2003 alipata wastani wa shilingi 1,500 kwa kilo ya kahawa na aliuza kwenya mnada moja kwa moja, yeye huuza moja kwa moja kwenye mnada wa Kimataifa, cha msingi hapa ni kuwa kahawa anayopanda ambayo ni miche bora kutoka *TACRI* ambayo inavumilia magonjwa kama *CDD* na ugonjwa wa kutu ya majani. Mzee Kishumbua alieleza kuwa magonjwa madogo yaliyobaki anayadhibiti kwa mmea wa asili uitwao utupa na mwarubaini ambayo haiharibu mazingira na imekuwa inatumika na mababu zetu kwa miaka mingi kama *Pestsides.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Kishumbua amepunguza kwa asilimia 40 gharama za uzalishaji kwa vile hana haja ya kutumia mruturutu, *blue copper* na *red copper* au *simdhin* ili kuzuia wadudu waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, hii ni moja ya Wizara ambayo iko chini ya Kamati yetu.

Moja, mradi wa Shirika la Nyumba *(National Boko)* tulitembelea huko tarehe 27, mradi huu ulibuniwa kwa lengo la kupunguza tatizo la nyumba za kuishi katika jiji la Dar es Salaam na ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya kujenga nyumba za kuishi katika Mji Mkuu na Mikoa ya Tanzania Bara. Mradi huu una lengo la kuwafanya Watanzania na hasa Watumishi wa Umma kuwa wamiliki wa nyumba badala ya kuwa wapangaji.

Mradi ulianza kutekelezwa tangu mwaka 2000 na utakuwa una jumla ya nyumba 200 za aina mbalimbali katika eneo hilo pia yametengwa maeneo ya huduma za jamii kama vile masoko, maduka, sehemu za kuabudu na sehemu za burudani, utakapokamilika mradi utagharimu jumla ya 3.95 bilioni ambapo kati ya hizo shilingi 1.5 bilioni ni mkopo kutoka shirika la *SHELTER- AFRIC* lenye makao yake mjini Nairobi.

Namba mbili, Makao Makuu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Mjini Dar es Salaam tulitembelea huko tarehe 23. Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Idara mbalimbali za Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi zikiwemo Idara Uimarishaji na Upatikanaji wa Kumbukumbu za Hifadhi yaani *Management Information System,* Idara ya Maendeleo ya Makazi na Idara ya Upimaji wa Ramani. Katika Idara ya Uimarishaji na Upatikanaji wa

Kumbukumbu, Kamati ilijionea hatua kubwa iliyofikiwa na Wizara kwa kuweka kumbukumbu nyingi kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Kamati iliona jinsi ambayo *letter of offer* inavyoweza kuandaliwa na kutolewa kwa muda usiozidi dakika tatu na hata kutolewa kwa kipindi kisichozidi wiki mbili, Kamati pia ilitembelea Idara ya Upimaji na Ramani ambapo ilijionea ramani na kumbukumbu muhimu ambazo ni hazina kubwa yenye kuelezea kwa kina michoro mbalimbali ya kijiografia kama Uoto wa Asili, Hali ya Hewa, Mabonde na Mito, Miinuko na kadhalika.

Pia Kamati ilipata maelezo na kuona jinsi ramani zinavyotayarishwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa *(Digital System)* ambayo imeleta ufanisi mkubwa katika zoezi la upimaji wa viwanja hali ambayo inaweza ikaepusha kiwanja kimoja kupewa mtu zaidi ya mmoja pamoja na kupunguza migogoro ya mipaka ya ardhi katika mashamba.

Tatu, mradi wa kupima viwanja Jijini Dar es Salaam, tulitembelea huko tarehe 28, mradi huu ulikisiwa kugharimu 8.9 bilioni una jumla ya michoro 44 yenye viwanja 20,000 vya makazi na 4,000 vya huduma mbalimbali za jamii, viwanja hivyo vimepimwa katika maeneo ya Twangoma, Kizota, Mbweni, Mpiji, Buyuni, Mbweni JKT. Hadi Kamati inatembelea mradi huo jumla ya viwanja 15,008 vilikuwa vimekamilika kupimwa na jumla ya shilingi saba bilioni tisa milioni zilikuwa zimelipwa fidia kwa wananchi waliokuwa na makazi yao katika maeneo hayo.

Wizara nyingine ambayo iko chini ya Kamati yetu ni Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Moja, mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Dar es Salaam *(DAWASA)* tulitembelea huko tarehe 29, Kampuni hii imekodishwa kwa mwekezaji binafsi kwa lengo la kupata teknolojia ya kisasa fedha za kuwekeza katika mfumo wa Maji Taka na kuboresha ufanisi katika uendeshaji na matengenezo jukumu la msingi kisheria *DAWASA* ni kutoa huduma ya Maji Safi na kuondosha Majitaka katika Miji ya Dar es Salaam na Miji ya Bagamoyo na Kibaha. Kwa sasa uwezo wa kuzalisha maji ni galoni 62 milioni za maji kwa siku ukilinganisha na mahitaji ya galoni 90,000,000 kwa siku na hivyo uwezo huo kutekelezeka kwa asilimia 99 tu.

Aidha, asilimia 55 ya maji yanayozalishwa hupotea njiani kutokana na uchakavu wa mabomba ambayo yaliwekwa miaka ya 1940 na 1980, ni asilimia 7 tu ya wakazi wa Jijini Dar es Salaam wameunganishwa kwenye mfumo wa Majitaka, kampuni hukusanya jumla ya shilingi 1.3 bilioni kwa mwezi. Tatizo kubwa katika utoaji wa huduma ya Majisafi ni wananchi kutoboa mabomba na kuchota maji bila kibali.

Pili, Mnada wa Mifugo wa Pugu, tulitembelea huko tarehe 30 Oktoba. Mnada huu ni mmoja wa minada 56 iliyojengwa kote nchini ya mradi wa kuboresha vituo vya kupokelea na kuuza mifugo kama ng’ombe, mbuzi na mauzo yake chini ya mradi huu ulioanza rasmi mwaka 1997 pia vituo 13 vya karantini na kukarabati njia za mifugo zimejengwa.

Mradi huu pia umejengwa machinjio ya kisasa Mjini Dodoma, mnada huu ndiyo soko kubwa la mifugo kama ng’ombe na mbuzi hapa nchini ambapo hata wanunuzi kutoka nje ya nchi

hutegemea mnada huu. Tatizo kubwa linaloukabili mnada huu ni wakulima na wajenzi wa makazi huvamia maeneo yake.

Tatu, Kiwanda cha Kusindika Maziwa cha *Tommy Dairy,* kiwanda hiki tulitembelea tarehe 31, kiwanda hiki kinamilikiwa na mtu binafsi. Kamati ilikitembelea kwa lengo la kujifunza na kujionea jinsi sekta binafsi inavyojihusisha katika kuendeleza sekta ya mifugo nchini na kuchangia katika uchumi wa Taifa. Kiwanda kina uwezo wa kusindika maziwa lita 20,000 kwa siku na kinatoa ajira kwa watu zaidi ya 100 wanaojishughulisha na kuuza maziwa kwenye vioski Mjini Dar es Salaam.

Aidha, kiwanda kinatoa soko la maziwa kwa wazalishaji wa maziwa wa Mikoa ya Iringa na Tanga.

Kuhusu *Tegeta Afiauna Farm Limited* tulitembelea tarehe 25, shamba hili ambalo linamilikiwa na mtu binafsi hujishughulisha na ukamataji na uuzaji wa nchi za nje wa wanyamapori na ndege.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa una dakika tatu tu.

**MHE. JOEL N. BENDERA (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisome mapendekezo.

Baada ya kutoa maelezo ya shughuli zilizofanywa na Kamati hii naomba sasa kwa niaba ya Kamati nitoe maoni na mapendekezo ambayo tunadhani kutekelezwa kwake kutaleta ufanisi katika Wizara na asasi zilizo chini ya Kamati hii, kuhusu Wizara ya Kilimo na Chakula:-

(a) Serikali iziimarishe taasisi za utafiti wa mazao, mifugo na wadudu waharibifu kwa kuvipatia vitendea kazi na vivutio kwa watafiti ili Taifa liweze kunufaika na matokeo ya tafiti mbalimbali.

(b) Wananchi wahamasishwe kutumia matokeo mazuri ya tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na Serikali kutoa ruzuku kwa watumiaji wa tafiti hizi ili kuboresha mazao watakayozalisha.

(c) Serikali iweke mikakati madhubuti kulinda matokeo ya tafiti zetu ili yaweze kuchukuliwa kiujanja unjaja, hii ni pamoja na mimea yetu.

(d) Serikali ilinde viwanda vyetu kutokana na ushindani usio halali unaotokana na kuingiza bidhaa kwa magendo na kukwepa ushuru.

(e) Gharama kubwa za umeme na miundombinu mingine zinafanya bidhaa zetu zisiweze kushindana Kitaifa na Kimataifa kutokana na bei zake kuwa kubwa, hivyo Serikali iangalie namna ya kutatua tatizo hilo.

(f) Wenye viwanda vya sukari nchini wahamasishwe pia kutengeneza *industrial sugar* ambayo ndio inatumika viwandani.

(g) Kamati inashauri Serikali ihakikishe ulinzi na kuhifadhi nasaba za mimea yetu kwa jumla na hasa nasaba zile ambazo zinapatikana hapa Tanzania peke yake kwa kuleta Sheria Bungeni itakayosimamia hifadhi na matumizi endelevu ya nasaba za mimea yetu.

(h) Serikali ihakikishe inatoa hatimiliki kwa mashamba ya katani yaliyobinafsishwa ili walionunua waweze kutumia katika kuyaendeleza mashamba hayo.

Kuhusu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi:-

(a) Serikali ipitie upya Sheria ya Viwango vya Pango ili kuliwezesha Shirika la Nyumba la Taifa kukusanya mapato yake kwa ufanisi. Hii ni muhimu Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu walio katika nyumba za *National Housing* hawalipi kodi.

(b) Serikali ianzishe mpango wa kutoa mikopo ya muda mrefu kwa ujenzi na ununuzi wa nyumba.

(c) Wakulima wadogo wadogo waliopewa ardhi na makampuni ya *Katani Limited Mwelio* wapewe hati miliki ya ardhi. Wizara zingine zitumie ramani ambazo zimetayarishwa na Wizara ya ardhi zinapopanga mipango yao inayohusika na ardhi.

(d) Utafiti uliofanywa na *Building Initiate Unit,* vifaa vya ujenzi hivyo vitumiwe kwa sababu vina bei nafuu.

(e) Shirika la Nyumba liangalie uwezekano wa kujenga nyumba za bei nafuu zaidi kwa vile nyumba walizojenga sasa ni ghali kwa wananchi.

(f) Mradi wa upimaji wa viwanja uendelezwe nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo:-

(a) Wazalishaji wa maziwa nchini wapewe fursa na kipaumbele katika kuuzia maziwa taasisi za Serikali hasa hospitali, shuleni na ofisini badala ya taasisi za kununua maziwa ziwe zinatoka nje.

(b) Baada ya *DAWASA* kukodishwa, maslahi ya watumishi yaangaliwe na kama italazimu kuwapunguzia basi wawapunguzie usumbufu katika kupata mafao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza kwamba Kamati hii sasa iitwe Kamati ya Ardhi, Kilimo na Mifugo ili iweze kutambua Wizara zote zilizomo ndani ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru wewe binafsi na nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kunipatia nafasi ya kusimama hapa mbele ili kusoma kwa niaba ya Kamati kwa kupitia nafasi hii taarifa yetu Bungeni pia kwa kuiwezesha Kamati yetu kufanya kazi zake kama ilivyopangiwa.

Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge aliyepita maana hii ni taarifa ya mwaka uliopita Ndugu Kipenka Mussa, msije mkaniona nakosea na wasaidizi wake kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi zake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa michango yao katika kuboresha mjadala, maoni na mapendekezo ya Kamati, kwa hakika tulikuwa na Kamati nzuri. Pamoja nao pia nawashukuru sana Mawaziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, Naibu wake Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Naibu wake Mheshimiwa Tatu Ntimizi na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati yetu muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru wataalam mbalimbali walioshirikiana na Kamati katika kutoa ufafanuzi tuliouhitaji. Wadau wote waliofika mbele ya Kamati kutoa maoni yao juu ya Miswada iliyoletwa na Mheshimiwa Spika mbele ya Kamati, walikuwa hazina kubwa ya ubora wa Miswada iliyochambuliwa katika Kamati yetu. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Wachangiaji kwenye hoja hii wapo saba. Kwanza kabisa nitamwita Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, atafuatiwa na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Edson Halinga, Lekule Laizer, Mheshimiwa Phillip Magani, Mheshimiwa Leonard Shango na Mheshimiwa Dr Diodorus Kamala.

Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, naona Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, hayupo.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa sana ambalo limefanya nisimame hapa, kwanza, ni kupongeza Kamati yenyewe. Hii Kamati inafaa kuigwa na Kamati zingine kwa sababu kwa muda mchache imeweza kuzunguka Tanzania nzima mpaka huko Mtwara ambako watu wengine hawaendi, lakini Kamati hii ilifika. Kwa hiyo, naipongeza sana Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa jitihada zake binafsi pamoja na Wizara yake jinsi walivyofuatilia mambo ya mbolea ya ruzuku ambayo tuliomba iwe nchi nzima na kweli imekuwa nchi nzima. Mwaka juzi ilikuwa sehemu chache tu katika Mikoa ya Kusini, lakini mwaka huu imeweza kutembea sehemu zote ambazo wakulima wanalima na nimemshuhudia

Waziri mwenyewe akitembelea kwenye Mikoa hiyo akiangalia ufanisi na taratibu zinazoendelea katika mpango mzima wa mbolea ya ruzuku

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri asichoke, kuna wakati walitaka kusimamisha mbolea ya ruzuku, lakini Waziri akatangaza kwamba inaendelea na naomba sauti hiyo iendelee kwamba mbolea ya ruzuku iendelee, kwa sababu kama utasimamisha sasa hivi ina maana kwamba wale walionunua ambao hawajamaliza kuuza watauza kwa *hijack price* ambako italeta hasara kubwa kwa Serikali, au wengine watafaidi kitu ambacho sio haki yao. Kwa hiyo, tuendelee na msimamo wa mbolea ya ruzuku ili watu wote waendelee kufaidika na wale waliotaka kupata faida kwa haraka haraka waweze kukosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaulizwa kwamba sasa kama unapongeza unasimama kufanya nini? Lakini kupongeza ni wajibu. Kuna hatua zingine ambazo pamoja na Kamati yetu maana mimi mwenyewe ni mjumbe mmojawapo wa Kamati hii, tumeshindwa kuzifikia hivyo naomba niziseme hapa Bungeni kusudi wote tutafute njia, tupeane mawazo ya namna ya kufikia hapo.

Moja, jambo linalonyanyua sana wakulima ni *STABEX* na nilivyojaribu kuuliza na kufuatilia nilikuta pamoja na kwamba Kamati ilishughulikia na Waziri alishughulikia, lakini kumbe lipo nje hata ya uwezo wa Waziri. Nimekwenda kwenye *internet* nimeangalia katika Mkataba wa *Lome Convention* na Mkataba mwingine wa *Cotonou agreement* ambao ulifanyika mwaka juzi. Nikachukua ile *copy,* inatoa maelekezo kabisa kwamba tumetoa bilioni 42 kwa maana ya *Euro 39 million* kwa ajili ya kuboresha kahawa, *heading* inasema hivyo. Nilivyofuatilia kusoma zaidi hiyo mikataba, wanatoa maelekezo wale wa *European Union* ambao wanatoa fedha hizo kwamba, fedha hizi zilime barabara za Mikoa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hilo nasema lipo juu ya Waziri kwa sababu, wale wanaotoa pesa wanatoa maelekezo, najiuliza ni kwa nini tunakubali maelekezo hayo, kwa nini wale wasiseme kwamba hizi hela ni za barabara na sio za kuboresha kahawa? Hilo limekuwa ni gumu hata kwa sisi wa Kamati ya Kilimo na Ardhi tumeshindwa kulitatua mpaka nikafuatilia huko kwenye *internet* kugundua kwamba kumbe sio Wizara hii inayotunyanyasa, kumbe ni wale waliotoa pesa ndio wanatoa maagizo. Lawama hapa nasema tu kwamba kwa nini Serikali yetu inakubali mambo kama hayo, mambo ambayo yanakwenda kinyume? Leo asubuhi hapa liliulizwa swali kwa Waziri wa Ujenzi kuhusu fedha ya *STABEX,* akasema anaandaa majibu. Kwa nini hizi Wizara zinaingiliana ingiliana kama ni *STABEX* ya kahawa ishughulikiwe na Waziri wa Kilimo na Chakula, ndiye anayejua wakulima wake na ndiye anayejua matatizo ya wakulima.

**MBUNGE FULANI:** Na ya pamba.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Nazungumzia *STABEX* ya kahawa, ya pamba itazungumzwa na wewe Mheshimiwa utasimama utachangia. Nasema *STABEX* ya kahawa ambayo mimi naijua ilitoka *Euro* milioni 39, kwa nini watoe maelekezo kwamba ziende kwenye barabara wakati kwenye Mkataba wanasema ni za kuboresha kahawa? Angalau hata wangesema *feeder road,* lakini wanasema ziende *TANROAD.* Sasa hilo linanitatanisha, naomba kama Waziri atakuwa na majibu zaidi lakini nimefuatilia nikafikia hapo ninaposema mimi kwamba, nimeona

niliseme hilo kwamba hawa wanatupa sijui ni mikopo au misaada ambayo wanatupa masharti ambayo hayafanani na ule msaada wenyewe. Sisi tunasumbuliwa huko Vijijini, hela ya *STABEX* Ngawaiya ulisema, iko wapi? Hela ya *STABEX* tulisikia Bungeni ni bilioni 42, sasa ziko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, walielekeza zaidi kwamba fedha bilioni 12 nyingine ziende Lyamungo, lakini wakatoa masharti eti zikae benki kama *sinking fund,* wao wenyewe kumbe ndio wanaelekeza, mimi nilikuwa namlaumu Waziri wa Kilimo na Chakula, kumbe si yeye. Wanaelekeza zikae kule benki kama *sinking fund,* mchukue tu faida inayopatikana huko benki, mtumie kwa ajili ya kununua *furniture* ofisini, kupika chai, kupaka rangi ofisi, kulipa na mishahara. Sasa huko ni kuboresha kahawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko sio kuboresha kahawa. Kwa nini tusiwaambie hawa kwamba mambo haya mnayofanya si sahihi kabisa na watu wetu siku hizi wameamka huwezi kuwadanganya?

**MBUNGE FULANI:** Hawataki kuambiwa.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Kama hawataki kuambiwa basi wakae na pesa zao. Kama hawataki kusema kwamba hizi ni za barabara na ziwe ni za barabara, hizi ni za kahawa na kweli ziwe ni za kahawa. Wanatuyumbisha huko mitaani, tutakosa kura sisi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waseme moja kwamba hii ni hela ya mahali fulani na iwe ya mahali fulani kuliko kusema tumetoa hela halafu wanatuchonganisha sisi na wapiga kura. Kwa hiyo, bado naomba Wizara na Waziri afuatilie, aongee tena upya na hawa watu wenye hizo fedha kwamba tuna misukosuko, Wabunge akina Ngawaiya hawakubaliani na maelekezo hayo, kwamba fedha mmesema ni ya kuboresha kahawa halafu mnaipeleka *TANROAD.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANROAD* sheria zake zipo wazi, haishughuliki na barabara za Vijijini na kahawa haikai Mjini. Sasa leo unapopeleka hela *TANROAD* kwa ajili ya kushughulikia kahawa inakuwaje. Hayo ni mambo ambayo hayaingii akilini lakini nakubali kulisema hapa nitoe dukuduku langu kwamba siku zote nilikuwa nasema huyu Waziri kwa nini anafanya hivi, huyu Waziri wa Fedha kwa nini anafanya hivi, kumbe maskini ya Mungu nawaonea.

Naomba leo nitoe dukuduku, tupambane na hao watu wanaotoa fedha, tuwaambie waelekeze fedha vizuri sehemu ambayo inatakiwa kuelekezwa, bilioni 42 zilizotoka kwa ajili ya kahawa basi wazitoe kwa ajili ya kahawa ili wakulima waweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naona limepelea katika Kamati yetu, mwaka 2001 nilitoa maelezo hapa kwamba kuna shilingi 460,000 ambazo kwa jumla zote ni 580,000 za wakulima wa kahawa *KNCU* ambazo hawakulipwa za mwaka 1988. Nimekuwa nikiahidiwa kwamba zitalipwa, zitalipwa. Kila mwaka Waziri amekuwa akiniahidi kwamba tutashughulikia, tunafanya mahesabu, tumeleta ma-*auditor* wanafanya mahesabu. Sasa kwa kuwa leo tunatoa taarifa ya Kamati na muda wetu umekwisha, tunaondoka hapa Bungeni, hatutakuwepo tena akina Ngawaiya tutetee tena hizo hela, vile vile tunataka hilo lishughulikiwe na litolewe majibu, bwana hizo fedha milioni 580 zilizopunjwa mwaka 1988 hatulipi tena.

Tujue kwamba hazilipwi, lakini sio tunaambiwa mwaka kesho tunalipa, mwaka kesho tunalipa, mwaka kesho kutwa tunalipa, tunafanya mahesabu, tunaleta ma-*auditor* hela ya mwaka 1988! Hawa wakulima ni watu maskini sana, wasaidiwe hizo fedha kwa sababu ahadi ya Waziri ilishakuwepo na hawa ma-*auditor* watafanya kazi miaka mingapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, mkulima anapolima na kuuza mazao yake halafu anakopwa halafu mazao hayo hayalipwi, hebu fikiria anawaza nini ndani ya Serikali hii? Kuna wakulima hata hawa wa pamba, wameuza pamba yao na mpaka leo hawajalipwa, wamedhulumiwa. Kuna hizo za kahawa, hazijalipwa, wale wakulima wamekaa tu hawalipwi, kwa nini? Wakati Serikali ina fedha nyingi? Kwa nini wasilipwe wakati wanalalamika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo haya naona yapo juu ya Wizara, kwa sababu kama Waziri anaahidi, halafu hela hailipwi, nisemeje? Sasa naomba Bunge hili hapa lisikilize, halafu litaangalia namna ya kumsaidia huyu Ngawaiya, hapa anapiga kelele fedha za hawa wakulima zilipwe au hazilipwi. Sasa ningeomba zilipwe na hizo za pamba nazo zilipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, narudia tena kusema kwamba napongeza Kamati, nampongeza Waziri kwa juhudi na bidii yake na vile vile kwa mimi niliyetoka Kilimanjaro kutokana na hali inayoendelea vizuri, sasa hivi kule mashamba yanaanza kuwa mazuri hivyo. Vile vile siwezi kuwasahau viongozi wa Mkoa kama Mheshimiwa Sarungi ambaye alikuwa pale, tulikuwa tukishirikiana naye kwa masuala ya kilimo na yeye anafahamu bidii yangu anajua, nilikuwa nafanyaje.

Pia Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa sasa hivi, Mheshimiwa Hilda Ngoye naye tunafuatilia mambo ya kilimo vizuri sana. Kwa hiyo, nimesimama hapa kwanza kuwapongeza, lakini tushirikiane kufuatilia hayo ambayo tunaona kwamba yamevuka mipaka au yametuzidi nguvu. Hata mimi Ngawaiya nitasaidiana na Wizara kwenda huko, kama ni huko *European Union* nitakwenda kuwauliza kwamba hebu nipeni ufafanuzi kuhusu hii fedha kwa nini mnafanya hivi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nikushukuru wewe pamoja na Kamati hii ya Kilimo katika maelekezo yake kwa Serikali na wote wahusika. Uchambuzi wao ni makini na kwa kweli ipo haja ya kuzingatia kama tunataka kupata mabadiliko ya kweli na mafanikio katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi nimefurahi kuona Kamati imeliona suala hili kwamba maendeleo ya nchi na kukua kwa uchumi kunatokana na kilimo na katika nchi yetu ni wakulima hawa wadogo wadogo. Tutakuwa tunapoteza muda kuzungumza juu ya kilimo cha mashamba makubwa wakati mashamba yenyewe makubwa hatuna. Tukianza kuzungumza na kutilia uzito huo, tutakuwa tunazungumzia watu wachache, the haves ambao wamepata maeneo na wanayatumia kwa kutaka kutumikisha watu wengine wawazalishie na kuishi kwa nguvu ya watu wengine, hili tutakuwa hatuendi mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wadogo ndio njia pekee ya kuweza kukwamua tatizo la uchumi wa nchi yetu na hasa kama Serikali itaweza isaidie kuwakwamua ili waweze kulima kwa jembe la ng'ombe ama punda. Nadhani tukifanya hivi tutakuwa tumekwenda kwa mafanikio mazuri, lakini kilimo hiki kinaweza kufanyika hata kwa eka moja au mbili ambayo ndio Watanzania walio wengi wapo kwenye kundi hilo. Lakini matrekta pamoja na mikopo mimi nina wasiwasi kidogo, kama kule kwangu kwanza ardhi ya kupata trekta, uipate wapi, hata kupata eka kumi si rahisi. Kwa hiyo hali hii mimi nasisitiza Serikali ione hilo la kuwapa msaada hawa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naishukuru Wizara ya Kilimo na Chakula na Serikali kwamba imekubali kutoa ruzuku ya mbolea, lakini ruzuku iliyotoka safari hii, haikulenga ukanuni wa kutoa mbolea. Mbolea tuliyokuwa tunaitumia sisi kule ni *Can, Urea* na *DAP* au *TSP* ambayo wakulima wetu kule pamoja na kwamba hawana vyeti vya kuonyesha utaalam wao wa utafiti, wamethibitisha kwamba ukitaka upande upate mazao mazuri unachanganya *TSP* na *Can* unapata mazao mazuri na hili limethibitika ni utafiti wa kiasili.

Kwa hiyo, wataalam mnaweza kufuatilia hilo muone mafanikio yake. Sasa hapo Serikali ilitoa ruzuku kwa *Urea* na *DAP,* sasa *Can* katika utafiti wa kiasili na watu wanavyolima kule, hata mimi mwenyewe kwenye vishamba vyangu vidogo natumia mbinu hiyo. Ukipandia *DAP* peke yake ukakuzia *Urea* mazao kama mahindi yanakuwa kwa urefu sana na ubebaji wake ni mdogo na yanaanguka sana hasa kukiwa na upepo. Lakini ukipandia *Can* na *TSP,* ukikuzia *Can* mazao yake yanakuwa mazuri zaidi na yenye uzao mzuri na upambaji mzuri wa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nililoliona, ni urasimu wa kugawa mbolea Mikoani. Kwa kweli unasababisha hata magendo na rushwa na hasa kule kwetu pembezoni. Mbolea nyingi namna hii wafanyabiashara wanaichukua, wanaiuza Malawi na Zambia na mwaka huu imethibitika maana imekamatwa. Alipofika Mheshimiwa Waziri Mkuu watu walilalamika ndipo ukweli ulipoeleweka. Kwa kweli kama ni kugawa mbolea, ni vizuri Mkurugenzi wa kila Wilaya ahusike na kama akichanganya basi yeye mwenyewe awajibishwe. Huu ndio utakuwa usalama, lakini sasa hii ya kumweka Afisa Kilimo wa Mkoa ndio anasimamia kugawa mbolea, kwa kweli hapa nadhani tulifanya makosa na kama tutaendelea, basi mradi huu wa kutoa mbolea kwa namna hiyo hautafanikiwa hata kidogo. Mkurugenzi ana maghala, watendaji kazi, kwa nini asipelekewe yeye akagawa kwa wakulima wake katika Wilaya yake. Hilo likisawazishwa hali ya ruzuku itakuwa ni nzuri sana na itawasaidia na mbolea itafika kwa watu wanaohusika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kilimo hiki kina tatizo, wataalam hawapo Vijijini. Sasa waliopo ofisini sielewi kama wanasaidia vizuri, sijui katika maeneo ya wenzangu kwa kweli tuna upungufu mkubwa wa wataalam, wananchi wanatumia ujuzi tu wanachanganya ule wa asili na ule walionao wenyewe, ndio unaosaidia kufanikisha shughuli hizi. Tungeomba basi wataalam waongezwe katika maeneo ya Vijiji ili waweze kufanikisha kilimo. Hata hivyo, usimamizi wa shughuli hizi za utafiti na nini unaonekana ni hafifu. Huko Wilayani kwangu tuna Kituo cha Utafiti, Mbimba, huko nyuma kilikuwa kwa kweli kinatoa mazao mazuri na mafanikio mazuri sana. Lakini kumepita pita mbinu pale, kimevurugwa vurugwa, leo ndio hakina kitu. Sasa usimamizi nadhani hili ni tatizo la nchi. Tuwajibishane katika kusimamia utekelezaji. Kila mtu apewe muda na apewe kiwango cha kukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Warusi walifanikisha hilo wakati huo wa ujamaa, ingawa watu wanaubeza sasa, ilikuwa mtu akiambiwa afanye kazi na amepewa hela ya umma, lazima athibitishe kazi ile aliyopewa na vifaa vilivyopo vinatekeleza mafanikio, kama hakutekeleza huyu ni mhujumu. Lazima tufike hapo na tupeane masuala hayo kwa nguvu zote. Hakuna sababu ya kusema huyu ni mtaalam awe ana *degree* ya kilimo na nini, basi hapo yeye ni *manager,* kama hajafanikisha u-*manager* wake ni bure. U-*manager* wa mtu ni mafanikio ya kazi yake, bila kuwa na mafanikio hata maana ya elimu yako hakuna. Tusije tukaishi na tabia ile ya kuthamini cheti ukutani wakati matendo hayapo, hatutakwenda mahali. Lazima tukubaliane kubadili na naomba Wizara hii ya Kilimo ianze kubadilika kwa mafanikio hayo tunayoyatarajia na yatakayotuwezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tukitaka kweli tudhamirie, tunazungumza sana juu ya kilimo cha umwagiliaji. Sasa mazingira yenyewe yameharibika, hata vijito vidogo vimekauka. Sasa tufanyeje, lazima tuwe na utaratibu kuna hivi vi-*streams* vidogo, watu wangeweza kujenga kuzuia maji wakati wa masika, tukajenga mabwawa ya kutosha, badala ya kutafuta magreda na makatapira kuchimba, tuzibe, kuna hali nzuri si mbaya maana unaona nchi yetu ni ya vilima na vikorongo, kwa hiyo tunaweza kujenga hapa tukazuia maji, masika yote yakajaa hapa na yakaweza kutusaidia hata kiangazi. Nadhani hilo ni suala ambalo lingetusaidia kuleta mabadiliko katika sehemu zile zenye miinuko na vitu kama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huu usimamizi hafifu unatokana na nini? Ni kwamba hakuna fedha. Fedha haipo ya kuwapa watu uwezo wa kufanya kazi na kufanya mambo. Sasa kama tunafikiri mradi hauna fungu ni afadhali tukanyamaza kuliko kuingiza watu waajiriwe na kazi haipo pale, haitusaidii. Ni afadhali kwa kweli tukubaliane, ziwepo fedha za mahali ambapo tunataka tupaendeleze. Leo hii pale Mbimba hata majengo yanabomoka hayana *repair,* wale wa Uyole wanahamisha watu wao. Sasa wameleta hawa wa *TACRI*, hawa wa mbegu bora ya kahawa. Hawa wenyewe nao hawana hata usafiri, wana kigari kimoja ki-*landrover* cha zamani kinachokwenda kwa kujikokota tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya tuyatilie katika hali ya kuyazingatia. Pili, naona afadhali tujisahihishe, hivi huu ujenzi wa nyumba wa Wizara ya Ujenzi na kuwauzia watu kwa nini unafanyika hivi? Kama ni hivyo basi tuipe Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ijenge nyumba na iuze. Iko haja ya kuona tuna Mashirika kama *PPF, NSSF* yana fedha zinalala *idle* kwenye benki hawana pa kuziwekeza kwa nini tusiwape mradi huo wakajenga nyumba wakawa wanawauzia watu. Lakini hii ya kujenga nyumba za Serikali tunazigawana Serikalini, sasa tupange kila mwaka kutafuta fedha kwa nini usiwe ni mradi huo wa kujiendeleza. Bodi mbalimbali za Mashirika haya zina uwezo wa kusimamia hili. Mimi nadhani hili tuangalie tusirudi nyuma.

Halafu suala lingine linaloua hata maendeleo yetu, Miji yetu yote kwa kweli inaonekana imechakaa hata hii Dodoma. Hii Dodoma hata ukisema ni Makao Makuu kwa kweli ni aibu hakuna Makao Makuu Dodoma yenye sifa hiyo. Wewe unakwenda hapo karibu unaona matembe hata Mjini sasa ni maendeleo gani hayo? Kweli Manispaa imepimia watu viwanja vya kujenga nyumba, lakini hakuna hata barabara wala masuala ya maji, sasa maji ya watu kutumia hakuna pale. Nashukuru mimi nimepata lakini niweka juhudi yangu binafsi kusukuma kwa

Waziri. Sasa tunataka maendeleo gani hasa na upimaji haupo Mijini? Sasa tutaendeleaje? *(Makofi)*

Sasa ni vitu ambavyo lazima tuvisahihishe na lazima tuvizingatie, tusipofanya hivi Miji itakuwa ya ovyo na tutabaki kwenye mazingira ya ovyo. Nenda nje hapo Makole utaona nyumba imekaa na choo kiko pembeni pale na nyumba imekaa upande sasa huu ni Mji gani Mkuu? Kumepimwa viwanja Ipagala kule hata njia hakuna hivi maana yake nini? Sasa hili kwa kweli Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iwe tayari kubadili utaratibu huu. Ipime viwanja watu wapewe.

Lakini Serikali inakimbilia kwenye *property tax, property tax* si pale ulipopima na unapahudumia. Sasa watu wanadaiwa *property tax* hakuna huduma yoyote ya Serikali. Sasa hii sijui tuseme Serikali imegeuka kuwa mwizi wa kudhulumu watu? Ni vizuri tulione hili suala kwa kweli vinginevyo hatutakwenda mahali.

Naomba hata fedha ya *STABEX* Mheshimiwa Waziri ni vyema azifuatilie kwa kuwa nilikwishazungumza na yeye, naomba uzifuatilie. Inaonekana hii fedha inayumba tu. Mara kule wasema imekuja sijui kwa msaada wa Uholanzi sijui wapi. Sasa haya mambo ya *STABEX* kama yamekuja kuendeleza kilimo cha kahawa, basi ziende kwenye kilimo cha kahawa siyo kuwapa watu wanaanza kulipana posho na wanalipana nauli. Sasa ni maendeleo gani tunayoyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono mia kwa mia Kamati hii iliyotayarisha hii ripoti. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Taarifa ya Kamati hii iliyopo mbele yetu sasa.

Kwanza, ningependa kuwashukuru sana na kuwapongeza Kamati pamoja na Wizara zote zilizopo chini ya Kamati hii. Ningependa kuishukuru Serikali nzima kwa kuweka utaratibu huu wa Kamati zote kuzunguka. Mheshimiwa Joel Bendera alisema kwamba ni Kamati yao ndiyo imezunguka. Lakini mimi nadhani ya kwetu ndiyo imezunguka zaidi ikiongozwa na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti. Mtwara wanasema haijawahi kufikiwa na sisi tumefika. Huo utaratibu ni mzuri kabisa kwa sababu tumejua matatizo yaliyopo katika nchi yetu.

Kwa hiyo, tunaweza tukayazungumzia hata maeneo ambayo Mbunge siyo kwake anaweza tu akayazungumzia matatizo ya wananchi kwa sababu anaelewa fika matatizo yaliyopo huko. Kwa hiyo, ningependa kuishukuru Serikali sana kwa utaratibu huo na ningependa kusema kwamba huo utaratibu uwe unaendelea ndiyo sasa Waheshimiwa Wabunge, wanaweza wakachangia vizuri hoja na miradi iliyopo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza na Wizara ya Kilimo na Chakula. Ukiangalia hili suala la pembejeo ni maeneo machache sana wanaopata ruzuku. Wananchi katika maeneo yetu kule Arusha wakisikia kitu kinachoitwa ruzuku ni kwamba hawaelewi kabisa kwa sababu hawajawahi kupata. Kwa bahati nzuri kule Arusha sisi hatuhitaji sana mbolea, hatuna haja na mbolea kwa sababu ardhi ni nzuri, lakini kuna pembejeo nyingine

ambazo tunazihitaji hatuzipati. Hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Wizara ya Kilimo na Chakula sidhani kama wananchi wa Jimbo langu wamewahi kumwona labda kama wamemwona kwenye televisheni akitoa hoja zake hapa Bungeni. Kila siku nalalamika kwamba na sisi tunahitaji pembejeo, huko kwangu bado wananchi wanatumia jembe la mkono ndilo linatumika kulimia mpaka sasa. Naulizwa kila wakati hiyo ruzuku ni kwamba wao hawapati, wanahitaji mbegu, wanahitaji majembe ya kukokotwa na ng'ombe hawapati.

Kwa hiyo, naomba katika Bajeti ijayo na sisi tukumbukwe kabisa msituone kwamba sisi ni wafugaji tu, siku hizi sisi ni wakulima. Kwa hiyo, tunahitaji pembejeo na tunahitaji ruzuku ya Serikali. Mnatuhesabu Monduli kwamba ni wafugaji tu kwa hiyo, mambo ya kilimo mnapeleka katika Mikoa mingine, sijui Rukwa, Mbeya mnatusahau kwamba na sisi tuna mashamba. Kwa hiyo, ningependa kuomba hili suala la pembejeo kidogo tulichonacho kitawanywe katika Mikoa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la ardhi. Nizungumzie kuhusu hatimiliki. Siku hizi Serikali imejitahidi sana wananchi wapate mikopo na ndiyo namna ya kuondoa umaskini. Lakini hiyo mikopo huwezi ukapata hivi hivi mpaka uwe na hatimiliki, hiyo mikopo haigaiwi kama mahindi ya msaada mpaka uwe na hatimiliki ya nyumba au hatimiliki ya shamba ndiyo upate mkopo. Sasa kule vijijini upimaji haufanyiki kule, upimaji unafanyika Mijini tu.

Kwanza, hicho kipengele cha kusema kwamba nyumba zilizopo vijijini vilivyopimwa mimi naomba kabisa kiondolewe kwa sababu ukifuata utaratibu huo wananchi wengi watakosa mikopo. Ukiwa na nyumba yako kijijini kule si inafaa iwe na hatimiliki uweze kufaidika na wewe ukaweka rehani ukapata fedha za mikopo. Kwa hiyo, naomba sana huo utaratibu ufutwe nyumba zipimwe popote vijijini. Utaratibu mwingine hizo hatimiliki ziharakishwe bado tunalalamika kwamba siyo vizuri kufuatilia hatimiliki Dar es Salaam. Kuna wananchi wengi sana ambao wako mbali na Dar es Salaam hawajawahi kufika hata siku moja. Ukimwambia aende Dar es Salaam ni shida kwake. Kwa hiyo, naomba kila Mkoa uruhusiwe ili wananchi wafuatilie hatimiliki zao Mikoani. Kila mara Waheshimiwa Wabunge wanapiga kelele kwamba tunahitaji hizo hatimiliki ziwe karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu mifugo. Sijui mifugo tumeipata tu kwa bahati mbaya lakini mimi sioni kwamba mifugo inathaminiwa katika nchi yetu. Sijui kwa sababu Bunge hili wengi siyo wafugaji sijui. Nasikia kila siku utetezi mkubwa sana ni suala la kilimo tu. Madawa, mbolea lakini madawa ya mifugo katika nchi hii ni shida kulizungumza au kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi sana wanategemea mifugo na baada ya ukame pamoja na magonjwa kupunguza mifugo imekuwa watu wachache sana nchini wenye mifugo ndiyo maana mnawaona wafugaji wengi sana wako Mijini ni umaskini wa kukosa mifugo ndiyo umaskini umewapeleka huko. Lakini bado sioni Serikali hii inazungumzia au inaona tatizo la hawa watu wanaofukuzwa na umaskini vijijini hawana mifugo bado Serikali inakaa kimya. Wenzetu wa Kenya na tupo mpakani pale wanatoa mikopo kwa hao wafugaji, ndiyo maana wao hawana walinzi wanaokwenda Mijini. Kwa sababu wanatoa mikopo kwa wafugaji, wanapewa fedha wanakwenda kununua mifugo na kuinenepesha na baadaye wanauza,

wanalipa madeni na kubakiwa na fedha na kuendelea na utaratibu wao. Lakini Serikali ya Tanzania haiwaoni wafugaji, inawaona tu kwamba sijui ni nini kimewapeleka pale, wafugaji hawapendi kwenda Mijini ni umaskini ndiyo umewapeleka pale, sasa hawajui nini kingine wafanye. Lakini bado mnazungumzia umaskini tu, lakini msaada wa namna ya kuwasaidia hawa watu mimi sijaona kwamba mnawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba Serikali kabisa itenge fedha kwa ajili ya madawa ya mifugo. Wizara hizi zina danadana kila siku kwamba ohoo mimi sina fedha za madawa wanasema Wizara ya Kilimo na Chakula, sijui hizo fedha zinapita wapi mpaka leo na hapa Bungeni kuna kasma yenye hizo fedha imesomwa Bungeni, Waziri Mkuu mwenyewe amehakikisha hata kwenye majibu yao kila siku wanasema watakaa wataangalia ziko wapi, kwa nini wasijue ziko wapi?

Kwa hiyo, napenda kusema kwamba madawa ya mifugo yapatikane kama inavyopatikana mbolea na nini. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba na sisi tupate madawa ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu mabwawa. Kuna mabwawa mengi sana yamejaa matope hayatumiki tena wala siyo Monduli tu ni katika maeneo mengi sana. Hayo mabwawa yakarabatiwa kwa sababu yatasaidia wafugaji kwenye tatizo la maji. Nasikia mnataka kutunga Sheria kwamba wenye mifugo wasihame tena. Je, watakaaje kama hawana maji lazima watahama tu.

Kwa hiyo, mabwawa yote yalijaa matope yakarabatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kuiuliza Serikali na baadaye nijibiwe hivi ni kwa nini mifugo haiundiwi chombo cha kuzungumzia ndiyo maana inasahaulika. Nasikia kwamba kuna Bodi ya Korosho, kuna Bodi ya Kahawa, kuna Bodi ya Mkonge, kuna Bodi ya Pamba, kuna Bodi nyingi za wanyamapori, lakini hakuna Bodi ya Mifugo. Hivi ni kwamba mifugo siyo zao kwa nini kusiwe na Bodi ambayo itazungumzia mifugo.

Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba kwa sababu mifugo ni zao mojawapo na yenyewe iwe na Bodi itakayozungumzia matatizo yake. Nadhani kila Bodi inapeleka taarifa na kila Bodi inayasemea matatizo ya zao linalohusika, lakini hakuna Bodi inayozungumzia mifugo ndiyo maana inasahaulika. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba na hilo nadhani kwenye bajeti ijayo tusikie kwamba na mifugo imeundiwa Bodi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi nichangie hoja ambayo iko mbele yetu.

Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi pamoja na Wajumbe wake kwa kazi nzuri waliyofanya kama inavyoonekana ndani ya ripoti hii. Hongera sana. Mchango wangu utalenga sehemu mbili.

La kwanza, ni kwenye upande wa utafiti, research. Kilimo bila research ni sawasawa na gari isiyo na sterling, huwezi kuiendesha. Nafurahi kuona kwamba katika ripoti hii research ya kilimo au utafiti wa kilimo umepewa kipaumbele karibu katika kila zao. Hii ni hali ya kupongezwa. Lakini napenda kuzungumzia kidogo juu ya kituo cha utafiti cha Serieni ambacho kiko kule Arusha. Kituo hiki kilianzishwa mwaka 1975 maalum kwa ajili ya kufanya research ya zao la ngano. Hii iliwezekana kwa msaada ya Serikali ya Canada na kama ripoti inavyosema Kituo hicho kilifanya nzuri katika muda wa uhai wake kimeweza kuzalisha aina ya mbegu ya ngano 13, aina nne ya mbegu ya shairi ambayo ni jamii ya ngano na aina tano ya mbegu za maharage na aina tisa ya mbegu za mahindi. Kwa kweli hili ni jambo la kufurahi sana.

Lakini nasikitika kuona kwamba katika ripoti hii imesemwa pale katika ukurasa wa 11 kwamba eneo la Kituo hicho ambalo lenyewe liko kidogo sana, kituo kizima kina eneo la eka 769, lakini pamoja na udogo wake Serikali imeona ni bora kumega eka 150 ili kuongeza uwanja wa ndege wa Arusha uwe uwanja wa Kimataifa. Kwa wale wanaojua Arusha na Tanzania watajua kwamba Arusha au Moshi kuna uwanja wa Kimataifa uko pale *KIA* ni kama kilometa 40, nadhani kutoka Arusha. Uwanja ule wa *KIA* wa Kimataifa hautumiki kutosheleza *capacity* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa kuona kwamba pamoja na uwanja wa *KIA* hautumiki *full capacity* wakati huo huo Serikali inaamua kujenga uwanja wa Kimataifa mwingine pale Arusha Mjini hapo Salien kwa kumega eneo ndogo ambalo lilikuwa limetengwa kwa ajili ya *research* au utafiti wa mazao muhimu sana ya chakula. Sasa najiuliza *priorities* zetu ziko wapi? Hivi ni kweli Serikali imeona ni lazima kujenga uwanja wa Kimataifa pale Arusha Mjini?

Nakubali kuboresha uwanja uliopo kwa kuweka lami kwenye *runways* ubaki mdogo kama ulivyo, lakini suala la kupanua uwanja huo kuwa wa Kimataifa kwa kweli suala hili naomba Serikali ilifikirie upya hasa ikimaanisha kwamba wanamega ardhi ambayo ilitengewa kwa ajili ya utafiti wa kilimo. Mimi nadhani uamuzi huo siyo wa busara kusema moja kwa moja hivi. Naomba utazamwe tena. *(Makofi)*

La pili, naomba niongelee kidogo juu ya zao la korosho. Nafurahi sana kwamba utafiti ambao unafanywa na Kituo cha Naliendele cha Utafiti wa Korosho wanafanya kazi nzuri sana wamepata mbegu za aina mbalimbali pamoja na mbegu ambayo inachukua muda mfupi kuzaa. Katika kufuatilia hili Mkoa wa Lindi ulijiwekea utaratibu wa mradi wa kupanua kilimo cha korosho ili kujaribu kupunguza makali ya umaskini ya wakulima wa Mkoa ule. Tuliazimia kwamba kila Wilaya katika Mkoa wa Lindi ijiwekee lengo la kulima au kupanda miche ya mikorosho mipya kwa kutumia mbegu hii mpya miche milioni moja kwa kila Wilaya na tulifanya mawasiliano na Bodi ya Korosho ili wao wawasiliane na Kituo cha Utafifiti cha Naliendele ituwekee mbegu hizo tuwagawie wakulima wetu. Bodi ya Korosho ilifanya vile ikaagiza zile mbegu na ikalipia jumla ya shilingi milioni 24. Lakini la ajabu ni kwamba siku ya siku wakati ambapo mbegu zinatakiwa sasa zigawiwe kwa wakulima tulipokwenda kule tuliambiwa kwamba ile mbegu imekwishauzwa na haikuuzwa kama mbegu. Tuzingatie kwamba uzalishaji wa mbegu ni wa aghali sana unachukua fedha nyingi mpaka uzalishe variety ya mbegu ambayo unaitaka. Kwa hiyo, thamani yake inakuwa kubwa kuliko zao la kawaida. Lakini cha kushangaza tuliambiwa kwamba mbegu hiyo imeuzwa kwenda kubanguliwa.

Kwa hiyo, mradi wetu wa kupanua kilimo cha korosho kama tulivyoazimia Mkoani umeanguka, sasa tumlaumu nani. Fedha zililipwa kwa Taasisi husika, lakini Taasisi husika ikaamua kuuza hizo mbegu kwenda kubanguliwa. Tulipouliza kwa juu juu tunaambiwa kwamba Kituo cha Naliendele kilikuwa hakina fedha ya kutosha kwa ajili ya kushughulikia kazi zao na ndiyo maana waliamua kuuza hiyo mbegu. Lakini kuna Mfuko wa *CIDEF* ambao umewekwa kando una fedha kwa ajili ya kuendeleza shughuli za korosho pamoja na research. Lakini fedha hizi zimezuiwa na Wizara ya Kilimo na Chakula kwa miaka miwili iliyopita eti kwa sababu wanasema Bodi ya Korosho imeshindwa kusimamia.

Sasa sisi tunashangaa Bodi ya Korosho hii imekuwa *appointed* na Wizara hiyo hiyo na Wizara kama inaona Bodi haiwezi kufanya kazi kwa nini basi Bodi hiyo isifutwe ikaletwa Bodi ambayo inaweza kufanya hiyo kazi ili Fedha hizo za *CIDEF* ziweze kutumika kwa shughuli ambazo zilikuwa zimewekwa kando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani siyo haki kuwaadhibu wakulima kwa sababu ya uzembe kama upo, uzembe wa Taasisi nyingine, lakimi mimi naamini uzembe haupo isipokuwa mahusiano yaliyopo kati ya Bodi ya Korosho na Wizara naomba yatazamwe ili Bodi hiyo ifanye kazi kulingana na maagizo katika sheria ambayo yameunda Bodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono ripoti hii moja kwa moja na nawatakia kila la kheri wale ambao wamehusika na shughuli hii wachaguliwa tena warudi hapa watuletee ripoti nyingine nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo katika ripoti hii ya Kamati ya Kilimo na Ardhi.

Kwanza kabisa nawapongeza Wanakamati hii pamoja na Wizara zinazohusika, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.Mimi nitaongelea zaidi katika eneo la kilimo na labda kidogo eneo la mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hii *makes very beautiful reading,* imeandikwa vizuri, takwimu zote zipo, maelezo mazuri na utekelezaji. Lakini mimi ninavyoona ripoti ni mwanzo au chanzo ambacho kingetupa sisi kama Waheshimiwa Wabunge katika kutoa maagizo na maelekezo kwa Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo tunavyokielewa cha sasa kinaendelea kama kilivyoendelea miaka 47. Kilimo kinachotakiwa ni kilimo kile ambacho kitawafanya wananchi washughulike wakati wote katika mashamba yao, lakini kilimo cha leo ni cha kutegemea mvua. Mwaka juzi tulikuwa na balaa la njaa na mwaka huu limetunyemelea. Lakini Serikali ina kigugumizi haitoi tahadhari kuwa mwaka ujao tutaponaje na hii njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningetegemea taarifa hii ingeelekeza zaidi nguvu zake katika kuelekeza kuleta mageuzi kwenye kilimo. Suala la kilimo ni suala la maji, kama huna

maji hujalima hata ukipewa mkopo, hata ukipewa pembejeo, hata ukipewa matrekta utakuwa hujalima.

Sasa mimi ningeomba au ningeshauri Kamati hii ingetoka na programu au ushauri kwa Serikali kuwa ratiba ya kuvuna maji yaani kuchimba mabwawa na malambo, kukinga maji katika mito na mahali ambapo maji yanaweza kuhifadhiwa. Hivi sisi hapa kama Taifa siyo kisiwa tunaona Mataifa mengine na nchi nyingine kilimo chao kinabadilika kinakuwa cha kisasa.

Sisi kilimo chetu cha kisasa au kilimo cha kumwagilia kinaendelea zaidi kwenye makabrasha na kwenye utafiti lakini ukiangalia kwenye ardhi, *on the grounds* hakuna kitu. Sasa tunamdanganya nani? Tunasema hata kwa takwimu Serikali inakuja juu inasema kwa takwimu sisi tunaendelea katika kilimo cha kumwagilia. Hivi ningeomba labda kama kuna wakati wa majumuisho kwa mwaka kilimo cha kumwagilia kinakuwa kwa kiasi gani kwa eneo na kwa kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa kuwa asilimia 80 ya watu wetu wapo Vijijini ni wakulima wadogo wadogo na wao kilimo chao ni cha jembe. Wakienda kukopa benki haziwezi kuwapa kwa sababu tatizo ni kuwa hawana dhamana na pili hata wakikopeshwa mvua isiponyesha watalipaje? Katika nchi jirani wakulima wadogo wadogo wanaweza kukopa kiasi chochote lakini sharti ni moja tu kuwa wanaulizwa je shamba lako lipo karibu na maji au lina uwezo wa kupata maji ya kumwagilia. Kama akijibu swali hili na kama Benki itathibitisha inapokwenda kukagua itaona labda mkulima huyu alikuwa ameomba kukopa kwa ajili ya pembejeo au kwa ajili ya mashine na vitu vingine vingine. Lakini Benki ikaona kuwa labda kuna umuhimu wa kuimarisha miundombinu ya kumwagilia maji katika shamba lile itamwambia au itamshauri yule mwombaji tafadhali uongezee ombi la mkopo wako tukuongezee kusudi uimarishe miundombinu ya kumwagilia.

Kwa hiyo, ndiyo inakuwa thamani ya shamba (kuthaminisha) na inakuwa ni dhamana tosha yake kwa sababu lipo karibu na maji na huyu mkulima anayekopa anapokuwa mzembe labda anakuwa mvivu asipozalisha vya kutosha na anashindwa kulipa mkopo basi Benki inachukua lile shamba na kumpa mtu mwingine ambaye atalima kwa kilimo cha kumwagilia na baadaye anaweza kulipa salio la mkopo. Sasa wakulima wetu wanategemea mvua kama hizi mwaka huu mvua hii imetuchenga. Kama wakulima wengi walikuwa wamekopa na wakashindwa kulipa mikopo yao je sio kufilisika kwa Benki hizi. Sasa mimi ningeomba Kamati hii ingetoa agizo kuwa Serikali ianze kutayarisha ratiba au programu kwa kila Wilaya jinsi ya kupata maji kwa kilimo cha kumwagilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sielewi kama tunangojea labda siku moja kutoka mbinguni, tukakuta mabwawa yamejengwa, malambo na mifereji na maji yako mashambani kama sisi wenyewe tusipofanya juhudi kuleta mageuzi haya. Kuna nchi nyingi ambazo maji yanakuwa haba lakini sisi tuna neema ya mvua. Lakini mpaka leo mvua hii haitumiki kikamilifu, hivi tuna mikataba gani na Bahari ya Hindi kuiachia maji yote yaende katika Bahari ya Hindi badala ya kuyatumia katika matumizi yetu hasa kwa kilimo. Kuna Mto Rufiji unamwaga maji yake baharini. Mwaka juzi kama Kamati ya Bunge tulikwenda kukagua daraja la Rufiji. Lakini cha kushangaza mashamba yaliyopo kando kando ya mto huu yalikuwa

yamekauka kwa kukosa maji. Maji ya mto Rufiji yako pale lakini hayatumiki. Serikali haielekezi.

Kwa hiyo, hili suala la kilimo ningeona kuwa sio suala la kuleta taarifa za takwimu na utekelezaji wa miradi midogo midogo tunataka mabadiliko, tuone sura ya nchi yetu katika mashamba kubadilika na wananchi waweze kulima kwa miezi 12 wakati wote kwa sababu watakuwa na maji. Hiyo ndiyo ingekuwa lengo kubwa sio suala la kuendelea na kilimo cha kutegemea mvua. Tunahitaji haraka iwezekanavyo tuone mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Wizara ya Maji na Mifugo. Mimi sielewi kwa nini shughuli za maji na mifugo zipo pamoja. Kwa sababu maji wateja wake ni wengi na pamoja na mifugo, kilimo, binadamu, viwanda, nishati. Kwa nini Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo isiwe pekee kusudi iwe na mtizamo mzuri zaidi katika sekta zingine. Leo mkulima na mfugaji hawaelewani katika matumizi ya maji kwa kupeleka maji mashambani atakuja kupitisha ukichimba mifereji mfugaji mifugo yake patakuwa na kuvuruga mifereji. Ningeshauri uwezekano wa kuanzisha Wizara ya Maji kusudi wateja wa kutumia maji watendewe haki na kwa uhuru zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa suala la mifugo kuna matatizo makubwa ya magonjwa. Katika Wilaya yangu ya Iramba, mifugo yote imepukutika, wananchi wamepiga kelele lakini hakuna linaloendelea. Ningeomba kwa kuwa teknolojia inayojulikana ya kutibu mifugo kwa nini leo hakuna kinachoendelea katika kuhakikisha kuwa suala hili la kupoteza mifugo au magonjwa ya mifugo yatokomezwe na mifugo ifufuliwe tena katika Wilaya ya Iramba.

Kwa hiyo, ningeomba Wizara inayohusika itazame suala na isiendelee kulifumbia macho kwa sababu mifugo ni uchumi na sehemu makini ya kuondoa umaskini, unapokuwa na mifugo kuna mbolea, kuna lishe bora na kipato cha fedha lakini sasa mahali unakuta majani yanajiotea kwa sababu hakuna ng'ombe wanaoweza kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ningesema tu kuwa suala la kuvuna maji ni suala muhimu. Mimi mwenyewe katika Jimbo langu nimebuni mradi na nimeupeleka Wizara ya Fedha wanauombea misaada lakini Wizara bado naendelea kuzungushwa. Ningeomba Wizara hii itazame kuwa mradi huu ni muhimu kwqa uchumi wa Wilaya ya Iramba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono ripoti ya Kamati na naomba Wizara husika wayafanyie kazi mapendekezo yangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja muhimu inayohusu kilimo na ardhi. Naomba nianze kwa kusema kwamba Tarafa ya Misenyi ambayo iko katika Jimbo la Nkenge ni Tarafa ambayo kiuchumi ni muhimu na kwa hivi sasa ni uti wa mgongo wa uchumi wa Mkoa wa Kagera. Lakini tatizo kwa kuwa Mkoa wa Kagera uko karibu na *Equator* na unafahamika kwamba ni eneo ambalo linapata mvua nyingi kwa hiyo mara nyingi ukiongea kwamba eneo hili ni kame nadhani Mheshimiwa Waziri wa Maji haimuingii akilini sawa sawa.

Sasa ni vizuri iwekwe kwenye rekodi na bahati nzuri yuko humu aelewe kwamba eneo la Misenyi pamoja na ukweli kwamba liko Mkoa wa Kagera ni kati ya maeneo kame. Ili wakati wowote ule akiona mradi wowote wa kwenda kuhudumia maeneo kame basi eneo hili la Misenyi lipewe kipaumbele kabla ya kufikiria maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua Wizara ilijitahidi kusaidia kupunguza tatizo hili. Tulifanikiwa kupata visima vinne virefu, lakini ilikuwa bahati mbaya sana kisima kimoja kilichochimbwa kwenye Kata ya Kilimilile na ambacho kiligharimu zaidi ya shilingi 12 milioni hadi leo ninapoongea hakijatoa maji. Ingawa mwanzoni nia ilikuwa ni nzuri inageuka inakuwa kero. Inakuwaje kero? Inakuwa kero kwa sababu hii Kampuni iliyochimba hiki kisima na visima vingine yenyewe ilidai kwamba bomba zilicheleweshwa kuletwa kwa hiyo ndiyo maana kiliziba. Lakini wale walioweka bomba zilipofika wanasema hapana inawezekana mchimbaji hakuchimba sawa sawa kwa sababu maeneo mengine pamoja na kwamba pampu zilichelewa kisima cha Nsunga maji yanatoka na ni maji mazuri. Kule Maruku na wao walifaidika kwa sababu wakati ule nilikuwa mlezi wa eneo hilo na wao wakapata maji, Kakunyu wakapata lakini Kilimilile ikawa ni tatizo.

Sasa nadhani ingekuwa vizuri Mheshimiwa Waziri mhusika basi alivalie njuga suala hili ili tuweze kujua shilingi 12 milioni hizi zinapotea namna gani. Lazima tupate mtu wa kuwajibisha ama aliyechimba ama aliyecheleweshа kuleta pampu. Kama aliyechimba alichimba vibaya basi achimbe tena maana pampu zipo. Kwa sababu huwezi ukatumia shilingi milioni 12 lakini baadaye ukashindwa kuwa na majibu ya uhakika kwamba tatizo lilitokea wapi.

Kwa hiyo, hilo ni ombi langu kubwa kwamba lazima tujue hizi shilingi milioni 12 zisipotee ili tuweze kujua tunaweza tukapata ufumbuzi namna gani. Sasa ukikutana na wataalamu wengine wanasema mara wanaweza wakafanya *fishing,* sasa hizi lugha zingine nyingine hatuzielewi vizuri. Ukiuliza fishing lini wanasema mpaka tupate kamera ya kupiga ndani tuone kuna nini. Sasa sisi kama wanasiasa inakuwa taabu sana kueleza maneno haya kwa watu wasiokuwa na maji. Ukianza kuelezea mambo ya fishing, mambo ya kamera hayaingii akilini sawa sawa. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba unisaidie hapa ili tuweze kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nashukuru vile vile kwamba walau tumefanikiwa kupata malambo kama mawili na kuweza kupunguza tatizo la maji. Lakini hili eneo la Misenyi tuweze kupata ufumbuzi wa kudumu wataalamu mbalimbali wamenishauri kwamba ingekuwa vizuri tukatumia maji ya Mto Kagera na wamesema uwezekano huo upo. Kwa bahati nzuri umeme upo na kwa bahati nzuri vile vile hata Wabelgiji ambao walitoa fedha nyingi kwenye mradi wa Kaempu walipokuja kwenye ziara ya mahitimisho ya mradi wa Kaempu walionyesha nia kwamba wapo tayari kusaidia upande wa maji eneo la Misenyi. Lakini wangependa wasikie Serikali inasema nini. Sasa kupitia Bunge hili naomba nitoe ombi rasmi kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji suala hili aliangalie kwa jicho la karibu ili hawa Wabelgiji ambao wamesema wako tayari kusaidia kwenye mradi mkubwa sio miradi midogo midogo basi waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi ambayo kwenye miaka ya 1970 ilianzishwa. Ilianzishwa miradi mingi ya maji, ukienda maeneo ya Ruzinga, Gera, Ishozi, Kanyigo na Minziro utakuta kuna mitambo ya kusukuma maji, kuna matanki mbalimbali lakini bahati mbaya

maji hayapo. Sasa suala hili unaweza ukalaumu kwamba wale walioanzisha miradi hii hawakufikiria sawa sawa. Lakini mimi nadhani kulaumu peke yake haitoshi. Kama walifanikiwa kuanzisha miradi hii na maji yakatoka kwa miezi miwili, mitatu, minne baadaye hayakutoka unaposimama ukalaumu walioanzisha haitoshi lazima wewe ujiulize je, baada ya kuwa wameanzisha miradi hii ikafanya kazi baadaye ikashindwa kufanya kazi wewe ulifanya nini kusaidia miradi hii ili ianze kufanya kazi tena. Sasa ndipo narudi tena kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na kumuomba na hilo alitizame tuone miradi hii tunaweza tukaikarabati namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka upande wa maji niongelee kidogo upande wa *vanilla.* Mwanzoni nilipokuwa napigia debe zao la *vanilla* watu wengi walikuwa hawajaliewa na wengine walifikiri labda ni matunda, hawakujua kwamba *vanilla* ni zao muhimu, ni zao lenye bei kubwa.

Kwa hiyo, mwanzoni nilionekana labda napiga piga *blaa blaa* tu lakini nikaendelea na nilijua kitu ukiwa unaanza na watu hawaelewi ukisema ni wachache watakuelewa. Lakini bahati nzuri wananchi wakaitikia na hivi sasa wananchi wengi wanalima *vanilla* na wanapata wastani wa shilingi 15,000/= hadi 30,000/= kwa kilo.

Kwa hiyo, hata wale mwanzoni waliofikiri naimba sasa wanaelewa kwamba hazikuwa nyimbo tu zisizokuwa na mafanikio na naweza nikajivunia kwamba baada ya kuimba vanilla kwa miaka minne baadaye yako mafanikio ya kwamba walau mtu anapata shilingi 14,000/= kwa kilo. Lakini lipo tatizo kwamba sasa wananchi wengi wana shauku ya kulima vanilla. Lakini tatizo ni miche. Kwa sababu mche mmoja hata ukiwa umekuwa *subsidized* zinatakiwa walau kati ya shilingi 500/= mpaka 1,000/= kupata mche. Sasa hapo ndipo namwomba Waziri wa Kilimo na Chakula ambapo tunasema sasa tutumie kilimo kupambana na umaskini hapa ndipo anaweza akaingia kwa kujaribu kuangalia tufanye nini ili kuwawezesha wakulima kupata miche. Wako tayari kulima lakini tatizo ni miche.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuongelea suala la *STABEX.* Wote mnafahamu nimelipigia sana kelele suala hili la *STABEX.* Lakini ukipiga kelele lazima ifike wakati ukubali kwamba hili jambo lilipofikia hapo ndipo lilipo na ukubali kulifanyia kazi kwa mtizamo huo. Maana fedha hizi si zetu lazima lieleweke kwa kila mtu kwamba hizi fedha zinatolewa na watumiaji wa kahawa zetu wa Ulaya na mtu anayetoa fedha anaweza akakupa masharti ya kutumia fedha hizo namna gani. Unaweza ukakataa kabisa kuzichukua ama unaweza ukazichukua ukakubaliana na masharti yake ukaendelea kujenga hoja ili baadaye abadilike.

Sasa mimi nadhani busara ni kuchukua hizi fedha kwanza tukazitumia wakati tunaendelea kumshawishi ili aweze kufikiri kama tunavyofikiri. Kwa hiyo, nimpongeze Waziri wa Kilimo na Chakula walau amenipa barabara tatu na hizi barabara ni kwa bahati nzuri ndizo barabara pekee nilizokuwa nimeahidi wakati naomba kura kwamba bila ya kutengeneza sigombei. Lakini nashukuru sasa kwa kupitia fedha za *STABEX* fedha zimepatikana kwa hiyo naweza nikarudi kwa wananchi wakati ukifika nikasema niliahidi na nimetekeleza. *(Makofi)*

Kuna barabara kwa mfano ya kutoka *Ruhoya.* *Ruhoya* kwa Kihaya maana yake ni wimbo. Sasa walishasema hii *Ruhoya* kila mtu anasema ni wimbo, wimbo lakini sasa

wamesema zitaitwa barabara za Kamala kwa sababu sasa fedha imepatikana. Kwa hiyo, tunashukuru Mwenyezi Mungu kwamba sasa na barabara zinaweza zikaitwa Kamala. Lakini kuna barabara nyingine ya Kyabajwa kwenda Kyaiyoma-Kitobo na hii ni barabara muhimu kwa sababu inapitia kwenye mradi wa Nkenge ambao Mheshimiwa Waziri amefanya kazi nzuri ya kufufua na juzi walinisomea risala wakasema mradi huu umefufuliwa kwa asilimia 90. Basi nikasema kama ninyi wahusika mnasema hivyo sina haja ya kusema hakuna kazi iliyofanyika na mimi nikawapongeza walau kwa kuona kile tulichojaribu kufanya.

Kwa hiyo na barabara hii itatengenezwa ili mitambo yetu iweze kufikishwa maeneo hayo kwa haraka haraka. Lakini kuna barabara nyingine moja Bugorora hadi Kabingo na yenyewe itatengenezwa vizuri tu. Nashukuru nimepata zaidi ya shilingi 300 milioni kwa kufanya kazi hizi. Ukipata kidogo shukuru ili uweze kujenga msingi wa kuomba kikubwa. Hilo ni jambo la msingi.

Lakini vile vile kuhusu fedha za *STABEX* hizo hizo tulisema nyingine zitatumika kuboresha kilimo cha kahawa. Naambiwa fedha nyingine zimepelekwa kwenye Chuo cha Kilimo Maruku kwa ajili ya miche ambacho nahitaji ni kuona hiyo miche inapatikana na inafika kwa wananchi. Vile vile ingekuwa vizuri sasa tukajaribu kuhakikisha kwamba tunapata wataalamu wa kuishauri kilimo cha zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niseme kwamba nashukuru kwa kazi walizofanya Wizara zinazohusika. Kwa kuwa nimeshukuru kwa haya machache naomba mniongezee makubwa zaidi ili tuweze kusonga mbele. Kwa hayo, machache naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kutoa pole tu maana yake ni mara yangu ya kwanza kuzungumza hapa katika Bunge hili. Pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria na wananchi wa Jimbo la Rahaleo, kwa msiba huo na Watanzania wote kwa ujumla tumesikitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi hii kwa ujumla Kamati zetu hizi za Bunge tangu zimeanza kufanya kazi kisekta zimesaidia sana Bunge kulielimisha na Wabunge kuelimika na kutimiza wajibu wao Kikatiba kuisimamia Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Kwa hiyo, tuna haki kabisa kujipongeza Wabunge kwamba tumeweza kutimiza wajibu wetu vizuri mpaka hapa tulipofika. Kwa kweli hata Serikali sasa ina ufafanuzi mzuri kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii kwa kweli kama tulivyoambiwa inahusika na Wizara tatu na muda hautoshi kuongea Wizara zote lakini nitagusia Wizara chache tu. Nikianza na Wizara ya Maji na Mifugo niseme tu kwamba nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kweli wanajitahidi sana angalau unaona Wizara inafanya juhudi za kukidhi na kujibu matatizo makubwa ya wananchi wetu. Nitazungumzia Mkoa wa Shinyanga na hasa Wilaya ya Bariadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza sana wafadhili wetu Waholanzi ambao walifadhili mradi mkubwa kwa uenezaji wa maji Vijijini katika Mkoa wa Shinyanga ingawaje matatizo bado tunayo na vile vile tuipongeze Serikali kwa kuanzisha mradi mkubwa ambao sasa

Mji wa Shinyanga utapata maji ya uhakika ya kutoka Ziwa Victoria ni maajabu maana watu wengine walikuwa wanasema maji ya Ziwa Victoria hayatumiki Tanzania. Sasa leo tunayatumia Tanzania. Tutaoga tutanywesha ng'ombe zetu, tutalima. Kwa kweli ni baraka. Tumpongeze Mheshimiwa Waziri na Wizara yake na Serikali kwa ujumla . *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tutapata na samaki kila mahali mpaka Bariadi. Niseme tu kwamba wafadhili wetu Waholanzi sasa msaada ambao walikuwa wameutoa kwa Shinyanga karibu shilingi bilioni 8 na kitu sasa umeisha lakini katika *process* ya kutumia huo msaada wananchi wengi sana wamehamasika. Iko mifuko mingi ya maji katika Vijiji kwa ujenzi wa mabwawa, malambo na visima virefu. Kwa kweli wamehamasika wamechanga wameunda mifuko mingi lakini sasa mradi huu ndio umefikia mwisho. Sasa tunaomba tu Mheshimiwa Waziri apokee juhudi za wananchi ili katika Bajeti zijazo wananchi hawa wa Shinyanga wasiweze kukosa *support* kutoka Wizara ili waweze kuendeleza miundombinu ya maji ambayo kwa kweli itasaidia sana upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Shinyanga. Tatizo kubwa la maji sio visima vifupi hivi kila siku mimi nazungumza hapa. *Water table* ya Shinyanga inayumba, inapwaya. Leo unachimba kisima unapata maji lakini ukiyatumia baada ya muda kiangazi kikizidi kisima hakitoi maji tena.

Kwa hiyo, dawa ya kujibu kiu ya maji Mkoa wa Shinyanga ni mabwawa au malambo au visima virefu sana. Kwa sababu matumizi ya maji kwa kweli katika Mkoa wa Shinyanga ni makubwa. Watu ni wengi, mifugo ni mingi na ni wakulima wazuri. Kwa hiyo, bustani ni nyingi vile vile. Kwa hiyo, jibu la kiu ya maji katika Mkoa wa Shinyanga mimi nasema bado tunahitaji kujenga mabwawa na miundombinu ya visima na malambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa baada ya kuupongeza mradi wa kutoka *Lake Victoria* kuja Shinyanga basi Mheshimiwa Waziri apokee ombi hili na ni la muda mrefu. Kwamba sasa mradi mwingine wa kutoa maji Victoria utoke Nassa uje Ngasamo uje Bariadi na maji yakatiririka kwa *gravity* mpaka Singida. Kwa hiyo, tutakuwa tumetibu kiu ya maji kwa Mikoa na Wilaya nyingi angalau tuweze kumaliza matatizo ya maji katika Mikoa hii. Kwa hiyo, hili nafikiri ni la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mifugo ningependa kusema tu kwamba Waheshimiwa Wabunge tusipende nyama tu bila ya kumpenda mnyama mwenyewe anayetoa hiyo nyama. Hapa Bungeni sioni mtetezi wa ng'ombe zaidi ya Wabunge wa Kimasai na Wasukuma wachache. Wengi tunazungumzia kupunguza ng'ombe. Nchi hii na Serikali kila kitu inasisitiza kuongeza uzalishaji. Kilimo ongeza, viwanda ongeza, sijui nini ongeza, hata biashara fanya sana. Ukifika kwenye ng'ombe punguza, utapunguzaje? Maana yake hatusemi ni namna gani tutaongeza ng'ombe. Hiyo ndio iwe motto ya nchi hi. Kama tunahimiza kuongeza uzalishaji, ushughulikiaji kila mahali sasa na ng'ombe tuongeze uzalishaji ili ng'ombe wawe wengi lakini wawe bora. Sasa namna gani tutafika huko ndio Serikali ilete mkakati isituambie tupunguze ng'ombe. Tupate malisho maana hata mnaona Wizara Mheshimiwa Waziri anafungua machinjio sasa ng'ombe tukiwamaliza hayo machinjio yatafanya nini tutachinja binadamu. Kwa hiyo, iko haja kwa kweli ya kuongeza idadi ya ng'ombe na ng'ombe wana kazi nyingi sana ndugu zangu. Wewe kama hujafuga ng'ombe ukapenda kula nyama lakini ukatamani ng'ombe wapunguze hataeleweka! Lakini siku utafuga ng'ombe mmoja, wawili utatamani wawe ishirini wawe mia mpaka mia tatu, jaribuni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisimalize muda wangu kabla sijasema kilimo na niingie sasa katika Wizara hii nyeti kabisa ya Kilimo. Watanzania tumekuwa na misemo mingi sana. Siasa ni kilimo, Kilimo ni uchumi, Kilimo uti wa mgongo, sasa tunasema kilimo sekta kiongozi. Sasa sijui msemo mwingine utakuja unasemaje. Lakini kila msemo tunaousema hausaidii kuboresha kilimo, hausaidii kuondoa njaa katika nchi, hausaidii hata wakulima hawa wauze wapi mazao yao na kwa bei gani. Sasa iko haja basi ya kusema kilimo ni nini. Kama kimeshindwa kujibu maswali haya basi kilimo isiwe sekta kiongozi, isiwe uti wa mgongo, kilimo isiwe ni uchumi. Kilimo sasa tutafute jina.

Mimi ningependa kusema Waheshimiwa tutatafuta jina nafikiri Mheshimiwa Waziri atakuwa nalo lakini misemo hii kwa kweli haijasaidia. Mimi nitasema tu katika zao la pamba hasa Wilaya ya Bariadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Bariadi ni wakulima hodari sana katika nchi hii na Mheshimiwa Waziri amejionea alikuja Bariadi mwezi Desemba tukamtembeza akaona maajabu. Kwa kweli kilimo cha Bariadi kwa kiasi kikubwa kinatumia maplau ya ng'ombe na matrekta kwa hiyo, kiko *mechanised to somehow.* Wanalima sana na labda tu katika uzalishaji wa pamba msimu uliopita Wilaya ya Bariadi iliongoza nchi nzima. Pamba iliyozalishwa Bariadi ni sawa na pamba iliyozalishwa Mkoa wa Mara wote.

Kwa hiyo, sisi ni wazalishaji wazuri na tunalima *mechanically.* Sasa nilitegemea basi Serikali ilete *support,* ku-*support* wakulima hawa wa kilimo cha pamba katika Wilaya ya Bariadi kwa kuwaletea madawa viua wadudu ya pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Bodi ya Pamba ilipanga Bajeti yake kuleta chupa zile za viua wadudu 297,000, lakini mpaka nazungumza hapa zimekuja chupa 190,000 bado 107,000. Sasa madawa ya viua wadudu ambao sasa hivi mpaka nazungumza hapa hali ni mbaya sana, wadudu ni wengi pamba hatutegemei kama tulivyokuwa tumeazimia pamba tutapata kiasi hicho na kwa sababu ya viua wadudu havipatikani.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nasema na kuna Bodi ya Pamba ambayo ina vyanzo vingi tu vya mapato na Serikali kwa ujumla. Nimezungumza suala hili kwenye Ofisi za Bodi nimezungumza suala hili na Waziri lakini sioni ufumbuzi. Mimi ningependa basi angalau wakidhi Bajeti waliyoipanga wafike chupa 297,000. Ndiyo!

Sasa kupanga Bajeti halafu hufikii malengo na hela mimi siamini kama hawana. Wanakusanya hela nyingi sana. Sasa kwa kweli nimezungumza sana lakini nimefika hapa nizungumze mbele ya Bunge na Mheshimiwa Waziri, atupe majibu fasaha siyo majibu ya kujihami, nataka majibu fasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile msimu wa pamba, katika msimu wa pamba sisi tunapangiwa, sisi tunalima pamba sawa na Brazil na nchi hizi za Kusini mwa *Equator.* Sasa wakulima wa Brazil ni wakubwa, wakulima wa Asia ya Kusini ni wakubwa, sisi tunapangiwa kufungua msimu wa pamba mpaka mwezi wa sita au wa saba mwanzoni, kumbe pamba sisi tumeshavuna tangu mwezi wa nne mwishoni, mpaka mwezi wa tano watu wanaweka majumbani

msimu haujafunguliwa. Kwa nini pamba isifunguliwe msimu mwaka mzima? Nchi zingine zinafanya hivyo, mtu akivuna pamba yake akauze pale na mtu mwenye *ginnery* aweze ku-*gin* apate mikataba ya kuuza pamba auze kabla ya wakulima wakubwa wa Brazil na kwingineko hawajavuna na kuuza pamba kwenye soko la dunia, bei inakuwa nzuri. Sasa ukisubiri wakulima wengine wakubwa kule wavune wewe utauza pamba ya Tanzania kwa bei ndogo sana ambayo hailipi mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, msimu ungekuwa wazi kwa muda wa mwaka mzima. Halafu na hii bei ya pamba ingekuwa nzuri, wakulima wa pamba Tanzania wangeuza kwa bei nzuri kwa sababu muda huo wakulima wakubwa watakuwa hawajavuna pamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kumalizia tu kwamba hela ya *STABEX* kwa barabara za Bariadi ni zipi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja hii muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Singida na kwa wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuchukua nafasi hii kwa heshima sana kutoa salaam zangu za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria na kwa wananchi wa Jimbo la Rahaleo kwa msiba mkubwa sana walioupata wa Mheshimiwa Mzee Balozi Ahmed Hassan Diria ambaye kusema kweli alikuwa ni rafiki yangu sana na tumefanya naye kazi katika Kamati yetu ya Mambo ya Nje pamoja. Hali kadhalika nachukua nafasi hii kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mzee Balozi Paul Bomani, wana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wananchi wote kwa msiba mkubwa sana wa baba yetu wa heshima Mzee Paul Bomani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nielekeze macho yangu Singida, Tanzania. Kama kuna jambo zuri sana ambalo limetokea Singida na hususan Singida Kaskazini kwa miaka mitano iliyopita ni kazi nzuri sana iliyofanywa na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kutuwezesha sisi wana Singida, kuwa katika mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia pamoja na Serikali yenyewe ya Tanzania kwa kuwahusisha wananchi wachange, ili waweze kupata miradi ya maji wanaochagua wenyewe. *(Makofi)*

Nafikiri dhana hii ya ushirikishwaji imekuwa siyo tu kivutio sana na hamasa kubwa kwa wananchi, lakini imewafanya kila mwananchi ajisikie kwamba anamiliki sehemu ya mradi husika. Kwa sasa tumeanza na vijiji vitano, Singida Kaskazini, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwa michango yao ya hali na mali na niseme tu kwamba wananchi Watanzania wana moyo sana wa kuchangia. Kila wakati walipoambiwa wachange na wakajua ni kwa nini wanachanga waliingia mifukoni mwao wakauza walivyonavyo, wakachangia maji. *(Makofi)*

Sasa viongozi wamesaidia na Serikali imefanya kazi kubwa ambayo kwa kweli historia itakuja kuji-*judge* kwamba Awamu hii ya Tatu imewezesha Singida kuanza kuelekea katika maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kuchimba visima virefu na vifupi, tunategemea kutengeneza miundombinu ya maji *(distribution systems)* ambapo maji yatatolewa kwenye kisima kirefu yatapelekwa kwenye shule za misingi yatapelekwa kwenye vituo mbalimbali vya wananchi kwanza ili kupunguza muda ambao akina mama wanautumia kwenda kuchota maji, kuimarisha na kuongeza tija, kuokoa wakati na kuharakisha shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza vijiji havitakuwa kama vile vijiji ambavyo tulikuwa tunavifahamu vya watu kubeba ndoo na kwenda kuchota maji. Ni matumaini yangu kwamba baada ya muda siyo mrefu tutaweza kufikia mahali familia ambazo zinajiweza zinavutiwa maji na wanaweza kuchota maji wakiwa wamekaa nyumbani kwa mabomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kuna maji mengi sana yatakayopotea kwenye kisima kirefu. *System* ya kuyatoa haya maji na kuyatawanya kuna maji mengi sana ambayo yatapotea ama kwa jua kali ama kwa kumwagika chini na maji yale mimi napendekeza tuanze na Singida Kaskazini kuyatumia.

Hivi karibuni baadhi ya Wabunge na mimi tulitembelea Taifa la Israel na katika kitu tulichokifanya tulitembelea shamba la mfano la teknolojia ya *drip irrigation.*

Kama tunavyojua Israel na nchi zingine za Arabuni ni jangwa. Kama mtu anafikiri Singida kuna ukame basi ukitembelea Israel, Singida ni mbinguni. Singida hakuna ukame wa aina yoyote. Tuna uwezo wa kupata maji ya kutosha kutoka vyanzo vyetu vya maji chini ambavyo wananchi watatumia, mifugo itatumia lakini maji yanayobaki mimi ningependekeza yatumike kwa teknolojia ya *drip irrigation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya teknolojia ya *drip irrigation* ni ya gharama kubwa lakini uendeshaji wake ni rahisi sana kwa mkulima wa kawaida. Tunao mfano wa shamba zuri sana la *drip irrigation* hekta 250 nje kidogo ya Mji wa Asmara kule Eritrea na lilitengenezwa na teknolojia ya Waisrael lakini baada ya kufanya haya mazungumzo na nikaliona tangu hili shamba lianze likiwa na mazao mchanganyiko mboga mboga na mazao mengine halijawahi kupata hasara hata mwaka mmoja. Wananchi wamefaidi na Asmara kama mnajua ni eneo kavu sana mara tano au kumi ya Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida Kaskazini tungependa tuanzishe shamba la mfano kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia teknolojia ya *drip irrigation.* Nimefanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa *The Moshevu* ambalo ni shirika la Israel linalosimamia maendeleo katika nchi za Afrika. Kimsingi tumekubaliana naye kwamba shamba hilo la mfano katika Tanzania litaanza Singida Kaskazini. Jambo lililobaki Waisrael watatoa teknolojia lakini lazima mtu mwingine atoe fedha.

Tumeanza mazungumzo na *USAID* na tunafanya mazungumzo na watu wengine lakini ninatumaini Wizara ya Kilimo na Chakula, ingefurahi sana kupata teknolojia hiyo na kuingia katika utaratibu huu iweze kushiriki kama sehemu ya ufadhili wa shamba hili la mfano la kutumia teknolojia ya *drip irrigation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida tuna shamba la mbegu linaitwa Mpambaa na ni kama hekta 250 liko Jimboni kwangu. Lakini tuna Ranchi, kama Ranchi ya Sagara zaidi ya ekari 5000 na tuna mashamba ya wananchi wa kawaida.

Sasa kitu ambacho tunataka tufanye na tunafikiri mahali ambapo miradi ya maji imeanza kutekelezwa tutatumia nafasi hiyo kuweza kuwa na hii teknolojia ya kuwa na shamba moja tu kwanza la mfano. Shamba hili la mfano litawawezesha wananchi wa kawaida kwanza kuweza kulima wakati wote, pili kuwa na *sustainable agriculture production* na kushirikiana kwa pamoja kuwa na soko la pamoja kwa sababu watakuwa wanazalisha vitu wanavyovijua na tutajua ni wapi waviuze.

Natoa wito kwa sababu Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, imeshiriki kwa kiwango kikubwa sana kuleta maji Singida. Miundombini hii inaanza kujengwa wakati wote sasa hivi, nafikiri zaidi ya shilingi bilioni moja zinatumika mwaka huu kwa Jimbo la Singida Kaskazini peke yake, zaidi ya bilioni Singida Kusini na kadhalika. Nasema jitihada hizo za Wizara hii zihamishiwe sasa kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula. Wizara ya Kilimo na Chakula ije Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza wananchi wasisome magazetini utafiti wa mboga na matunda na maua huko Tengeru, utafiti wa miwa huko Morogoro na kadhalika huko mahali pengine utafiti mwingine ufanyike pale pale Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakubaliana na watu wa nchi hii kwamba Singida ni mfano wa Mikoa mingine yote ambayo tunaweza tukaita ni *semi arid* na kwa sababu hiyo kama shamba hili litafanikiwa Singida nina uhakika kabisa Wilaya zote ambazo zinaweza zikapata maji na zinaweza zikapata teknolojia na Serikali, ikashirikiana na wadau wengine wote kuwapatia ufadhili wa kuweka miundombinu ya *drip irrigation* tutatumia maji kidogo sana kunyunyizia mazao mchanganyiko na wananchi hawa wataweza kufaidi matunda ya uhuru wa nchi hii baada ya miaka 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba kwa heshima na taadhima nirudie tena kukushukuru kwa kunipa nafasi na nirudie tena kuzipongeza Wizara zote tatu ambazo sijaweza kuzielezea zote Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kazi nzuri walizozifanya, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kazi thabiti kabisa ambayo inaiweka Singida katika ramani ya nchi hii na Wizara nyingine iliyotajwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Kazi kwa kazi ambayo tunaliona na naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri sana ambayo imefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naitakia Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi Uchaguzi Mkuu mwema na baraka za Mungu katika awamu ya nne. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia kwa muda mfupi sana kuhusu hoja ambayo iko mbele yetu.

Kabla sijaendelea na mimi napenda nijiunge na Waheshimiwa Wabunge, wenzangu kutoa salaam za pole kwa familia za Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria na familia ya mzee wetu Balozi Paul Bomani, Mwenyezi Mungu aendelee kuziweka mahali pema peponi roho za Marehemu. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili napenda kuwashukuru sana Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa kazi yao nzuri na kwa taarifa yao nzuri ambayo imewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Kwa taarifa ya Kamati napenda niseme tu kwamba kwa Wizara yangu tumekwishajibu hoja zote na tumekwishazigawa kwa Waheshimiwa Wabunge, pengine si lazima kurudia majibu ambayo tumekwisha yatoa, lakini hoja zote tumekwisha zijibu na tutaendelea kushirikiana na kamati hii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Napenda nitumie nafasi hii kwa kweli kuwapongeza sana kwa jinsi wanavyotoa msukumo na kufuatilia shughuli za Wizara yangu wametusaidia sana katika mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya matokeo tutayaona katika mkutano ujao kuhusu marekebisho ya sheria ya shirika letu la nyumba ambayo tutaiwasilisha katika mkutano ujao ili tutekeleze yale ambayo Kamati imeshauri na kupendekeza katika taarifa yao hii.

Pia napenda nitumie nafasi hii nijibu kwa kifupi tu hoja za Waheshimiwa Wabunge wawili, Mheshimiwa Edson Halinga na Mheshimiwa Lekule Laizer.

Kuhusu hoja za Mheshimiwa Edson Halinga, napenda nimhakikishie tu kwamba Miji yetu ni kweli kama alivyosema baadhi ya Miji yetu haipendekezi ni michafu pengine haisimamiwi vizuri. Lakini napenda nitumie nafasi hii kutoa wito kwa watendaji katika miji yetu yote nchini kwa Halmashauri zote kwamba miongozo ipo, sheria zipo sasa tuwaombe wasimamie vizuri uendelezaji wa miji yetu.

Tunaomba Waheshimiwa Wabunge, katika Halmashauri zetu basi wahakikisha kwamba tunatenga angalau fungu kidogo kwa ajili ya uendelezaji wa miji yetu ili iweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Edson Halinga huko Mbozi basi usimamie katika Halmashauri yetu ili mji wetu wa Vwawa na mingine iendelee kupangwa na kuendelezwa vizuri na miji mingine popote nchini basi isimamiwe vizuri.

Pili, Mheshimiwa Lekule Laizer, kwanza namshukuru kwa jinsi anavyofuatilia suala la upimaji na utoaji hati katika vijiji na katika jimbo lake na ningependa tu nimhakikishie kwamba kazi hii ya upimaji na utoaji hatimiliki sasa inafanyika huko huko Wilayani. Sasa hivi tumeanza zoezi la kupima Vijiji vyote nchini na kutoa hatimiliki za kimila vijijini na kazi hii inafanywa na maafisa ardhi huko huko Wilayani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge shirikianeni na maafisa wenu kwenye Halmashauri zenu kufanya kazi na tuhakikishe kwamba tunatenga fungu kwa ajili ya kazi ya upimaji ambayo ni kazi yenye gharama kubwa.

Lakini pale ambapo utalaamu na ushauri wa Wizara unahitajika tuko tayari kushirikiana na vijiji popote nchini ili angalau zoezi hili tuweze kulikamilisha kuwawezesha wananchi wetu kuwa na ardhi wakamilikishwa wakawa na uhakika wa ardhi yao Mijini na Vijijini.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Lekule Laizer, ningekuomba sana ushirikiane na wataalamu wenu kule Wilayani kukamilisha kazi hii. Ile ambayo iko Wizarani tutahakikisha tunaharakisha kuikamilisha ili irudi kwenu muendelee kuishughulikia kwa ngazi ya Wilaya. Tutaendelea kushirikiana. Tunakushukuru sana kwa msukumo wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kutoa wito kwa Watanzania wote, kwamba kwa hali tuliyonayo hivi sasa ni muhimu kwa kila Mtanzania akawa na ardhi yake mahali fulani. Kama umeamua kuishi Mjini basi hakikisha una kiwanja Mjini na umemilikishwa. Kama umeamua kuishi kijijini hakikisha una eneo lako kijijini na utapimiwa utapewa hati miliki huko huko kijijini.

Kwa hiyo, naomba tushirikiane katika hili ili kila mmoja wetu awe na sehemu yake kusiwe na sababu kwamba mimi sina ardhi uanze kuhangaika katika nchi yako kama mkimbizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na naunga mkono hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Joel Bendera, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi. *(Makofi)*

Lakini na mimi nijiunge na wenzangu kutoa rambirambi kwa familia za Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria na Marehemu Paul Bomani waliokuwa waasisi wakubwa sana wa Chama chetu cha mapinduzi na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Eliachim Simpasa na Kamati yake kwa kazi nzuri sana ambao tumefanya nao kipindi chao. Walikuwa ni watu mahiri sana, watu tulioshirikiana vizuri sana na kama alivyosema Mheshimiwa Gideon Cheyo, baadhi ya mambo waliyopendekeza yataonekana kwenye Bajeti yetu mwezi wa sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaenda kwenye hoja nieleze masikitiko yangu kwamba leo asubuhi nimekaa Bungeni humu miaka mingi kidogo sasa, lakini leo asubuhi nimefadhaika sana kwa kitendo kilichotokea humu ndani juu ya Wabunge wenzetu wale ambao Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, imewachukulia hatua. Jambo lile ni aibu kwa Bunge letu, ni aibu kwa nchi yetu. Lakini ni somo kwa Watanzania ya aina ya Wabunge wanaoletwa na baadhi ya Vyama vya Upinzani. Tunawasihi sana jambo hili liwe fundisho, tunaelekea kwenye uchaguzi wasituletee tena, Watanzania wasikubali watu wa aina hii wanaotoka vyama hivi ambavyo wanatuharibia heshima ya Bunge letu na heshima ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia eneo la maji na mifugo ni Mheshimiwa Joel Bendera mwenyewe, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala. Wote naheshimu mawazo yao, nakubaliana sana na baadhi ya hoja zao na nakubaliana na msukumo waliouweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la wafugaji kwamba kuna umaskini mkubwa, nakiri, nakubali sana. Nakubaliana na Mheshimiwa Lekule Laizer, kwamba Morani wengi, walioko Mijini wamekwenda Mijini kukimbia umaskini Vijijini. Lakini umaskini huo kwa kweli umesababishwa na sisi Serikali kwa sehemu kushindwa kuishughulikia vizuri mifugo.

Labda nieleze vizuri, matatizo yaliyotokea katika maeneo ya wafugaji ni kwamba mifugo imekufa mingi sana, mtu alikuwa na ng'ombe 200 wote wamekufa na kwa nini? Huko nyuma Serikali ilikuwa ina-subsidize dawa ya kuogesha mifugo kwa hiyo, nchi nzima mifugo ilikuwa inaogeshwa. *(Makofi)*

Miaka michache iliyopita zikapita sera za kusema kuanzia sasa Serikali haitatoa ruzuku ya kuogesha mifugo, matokeo yake ng'ombe anapozaliwa ana kinga yake ya asili *(natural immunity),* anaweza akaishi nayo au anaweza akafa. Lakini ng'ombe anapokuwa na *natural immunity* ukianza kumuogesha maana yake umemjengea *artificial immunity.* Ile *artificial immunity* lazima iendelee, lazima umuogeshe kila wakati wake. Siku unaacha kumuogesha maana yake umeondoa *immunity* ile na ng'ombe dhahiri atakufa.

Sasa matatizo yalitokea kutokana na Serikali wakati ule kusimamisha mara moja shughuli za kuweka ruzuku kwenye uogeshaji wa mifugo. Ni jambo ambalo tumelitambua na napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kwamba tunalishughulikia kikamilifu sana na kwenye Bajeti ya mwaka huu litazingatiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeunda Taasisi za mifugo alizouliza Mheshimiwa Lekule Laizer, tayari tuna *diary board, beef board* waraka wake uko kwenye Baraza la Mawaziri, nategemea tutaumaliza kabla kipindi hiki hakijaisha Mwenyezi Mungu akibariki. Lakini nitofautiane na Mbunge mmoja aliyesema suala la mifugo halijazingatiwa na Serikali.

Bajeti ya mifugo imeongezeka kutoka shilingi bilioni moja mwaka 2001 mpaka shilingi bilioni 8.3. Sasa dhahiri imeongezeka. Kazi yetu kubwa kwenye sekta ya mifugo kwa kweli ni kuelimisha na kuelimisha. Rafiki yangu Mheshimiwa Danhi Makanga anasema kwa nini tunawaambia wananchi wapunguze mifugo? Mheshimiwa Danhi Makanga tunazungumza juu ya ufugaji bora na wa kisasa. Botswana wana ng'ombe 2,500,000 wanawaletea mapato kwa mwaka dola za Kimarekani milioni 600. Tanzania tuna ng'ombe milioni 17 kwa mwaka tunapata dola za Kimarekani milioni 7. Sasa haziwezi kwenda namna hii.

Kwa hiyo, tunazungumza habari ya ufugaji wa kisasa na wa kibiashara. Tumemaliza kujenga machinjio hapa Dodoma na Mheshimiwa Danhi Makanga utakiri sasa nyama inayoliwa Dodoma sasa ni *first class meat* inayoshindana katika viwango vya Kimataifa. Tunakusudia kuanzisha machinjio nyingine saba ili ikiwezekana tuwashawishi Watanzania kuuza mifugo yao

na ikiwezekana wauze nje ili awe anafuga kibiashara siyo kwa ajili ya umaarufu tu ana ng'ombe 300. Unakuwa na ng'ombe 300 halafu una umaskini haifai, tunataka mtu awe na ng'ombe 20 lakini hali yake ni nzuri. Kwa suala la mifugo ningeishia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kidogo kwenye suala la maji. Nakubaliana na wale waliozungumza juu ya maji, Mheshimiwa Leonard Shango, nakubaliana nawe sana, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu nakubaliana nawe sana na nakupongeza wewe ni mmoja wa Wabunge unayejua kufuatilia mambo sana ya Kimataifa na nakupongeza jinsi ambavyo unapata misaada kwa ajili ya Jimbo lako nakupa hongera sana. Tutazingatia ushauri huo tutakaopata kutoka Israel tutakuwa tayari kujifunza kutoka kwao ili na sisi tufanane nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema tumejibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, ziko humu naomba nimalizie kwa kuwashukuru sana walivyotupongeza, mmetutia nguvu na tutaendelea kusaidiana mpaka tumalize muda wetu ahsanteni sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru kupata nafasi ya kujibu baadhi ya hoja. Lakini na mimi nitangulie kwa kutoa rambirambi kwa wenzetu waliotutoka na kuziombea familia zao kila la heri katika maisha yao kuanzia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa kwanza aliyezungumza ni Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na wengine waliofuatia ni Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na mwisho aliniandikia Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, akinipa hoja zake naye namshukuru. Nawashukuru wote kwa michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote hapa tunahusiana na kilimo zaidi kuliko sekta nyingine yoyote. Kutokana na mchango wa kilimo katika maisha na uchumi wa nchi hii kila mmoja amekizungumzia kilimo kwa njia moja au nyingine. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana sana na mengi mliyosema na hoja nyingi zilizotolewa katika taarifa hii tulishazitoa katika maelezo ambayo tumesambaza kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Lakini niseme naishukuru sana Kamati yetu na Mwenyekiti wake na wajumbe wake wote kwa kazi nzuri sana waliyofanya kutembelea maeneo yote ya kilimo kutusaidia kutoa maelekezo pale ilipobidi kutoa maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati mmoja walikwenda Morogoro wakakuta watu wanalima kwenye misitu wakawa wakali sana. Nawashukuru sana kwa yote hayo waliyofanya. Wametembea siyo humu nchini tu wametembee mpaka nje ya nchi. Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na Mwenyekiti, wamekwenda mpaka nchini Misri walikoona *drip irrigation* anayozungumzia Mheshimiwa Lazaro Nyalandu. Kwa hiyo, wamefanya kazi nzuri sana nawashukuru sana. *(Makofi)*

Nitajaribu kuunganisha majibu kwa sababu muda uliobakia ni kidogo sana ili katika dakika sita/saba niwe nimemaliza kutoa maelezo. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Thomas

Ngawaiya, kwa kutupongeza kwa ruzuku ya mbolea. Sasa hivi tumejaribu kuieneza nchi nzima. Bado kuna matatizo hapa na pale lakini imetupa fundisho kubwa sana.

Ndugu yangu, Mheshimiwa Edward Lowassa, naye amelizungumzia suala kama hili, katika mifugo kwa sababu kwa kweli ni ndiyo njia ya kumrahisishia mwananchi na kumwezesha mwananchi kupata mahitaji yake ili kuboresha uzalishaji wake. Nashukuru sana kwa hilo.

Lakini hakukosa kuzungumza juu ya *STABEX* maana kwa kweli kama kuna Mbunge anayezungumzia *STABEX* hapa Bungeni, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya ni *number one.* Sasa hivi tuko katika hatua ya utekelezaji, uwezekano tena wa kurudi nyuma kufanya *negotiations* kwa kweli haupo. Kwa hiyo, kazi kubwa iliyopo ni kuhimizana ili huu utekelezaji uende kwa kasi kubwa zaidi, hususan ile *component* inayohusu barabara ambayo inashughulikiwa na *TANROADS* kwa sababu wao ndio wataalam wa barabara. Sisi wa kilimo siyo wataalam wa barabara na mkitutaka tutengeneze barabara huenda tukapanda mahinda na kahawa badala ya kuzichonga ili ziimarike zaidi.

Kwa hiyo, naomba tukubaliane kwamba *TANROADS* ndiyo watakaoshughulikia hiyo *component* ya barabara. Wana *capacity* ya kuishughulikia na wameshaishughulikia kwa kiasi kikubwa sana. Ninachotegemea ni kwamba utekelezaji utaanza kabla ya mwisho wa mwaka huu. Naona Mheshimiwa Waziri akitisa kichwa kwa busara pale kwamba hivyo ndiyo itakavyokuwa.

Kwa upande wa utafiti umekuwa ukifanyika na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, anatuambia kwamba hata kule Maruku wanaanza kuzalisha vipando vya kahawa ili ku-*improve* kahawa. Ninachotaka ni vipando hivyo vipatikane kwa wingi zaidi. Mheshimiwa Dr. Kamala nitafuatilia hilo kuhakikisha kwamba linafanyika. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, anazungumzia ugomvi wa siku nyingi sana wa shilingi milioni 580 ulioko kati *KCU* na Bodi ya Kahawa. Tulikwisha kuagiza kwamba pande mbili zikae, wasuluhishe mahesabu yao halafu walipane kadri ambavyo wangekubaliana. Nitafuatilia hili na kuhakikisha kwamba tunalifikisha mwisho. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Edson Halinga, amezungumza vizuri sana. Yule mzee wangu sijui yuko wapi, amezungumza vizuri sana juu ya masuala mbalimbali. Mimi nafikiri nikubaliane naye kwa sababu kwa kweli moja ya matatizo yetu katika nchi hii, siyo katika kilimo peke yake, ni usimamizi hafifu sana wa shughuli zetu.

Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba lazima tuimarishe sana usimamizi na kuhakikisha kwamba kila anayepewa kazi anaifanya kikamilifu na kuitimiza. *(Makofi)*

Aidha, amezungumzia sana hili suala la *irrigation* kwa maana ya kuvuna maji ambalo vile vile amelizungumzia Mheshimiwa Leonard Shango. Tunakubaliana kwa asilimia mia moja. Tatizo ni *resources* na wala siyo nia.

Mheshimiwa Leonard Shango ametaka kujua vile vile kwamba tunaongeza eneo la *irrigation* kwa kiasi gani. Kwa sasa eneo la *'irrigation'* linaongezeka kwa wastani wa hekta 30,000 kila mwaka kama tutakavyotoa taarifa tutakapopata nafasi ya kuzungumzia suala hilo.

Mheshimiwa Edson Halinga amezungumzia vile vile juu ya mbolea kwamba huwa anapendelea *CAN*. Lakini *CAN* haikupewa ruzuku lakini siyo kweli. *CAN* tuliipa asilimia 75 ya ruzuku wakati *TSP, Dap* na *Urea* tulizipa asilimia 100. Sababu ni kwamba *Urea* ina virutubisho mara mbili ya vilivyopo katika *CAN*. *CAN* ina virutubisho 26%, *Urea* ina 46% ya virutubisho. Ndiyo maana ukitumia *Urea* kama unavyotumika *CAN,* mimea yako itarefuka sana kwa sababu ya virutubisho vingi vya katika *Urea.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tu-*encourage* wakulima watumie *Urea* zaidi kuliko *CAN* kwa sababu *CAN* ina virutubisho vichache mno. Ukichukua bei kwa mfuko wa kilo 50 utakuwa kwa kweli ukitumia *CAN* utapata hasara kuliko utakavyotumia *Urea* ambayo utapata faida. Kwa hiyo, tunaendelea kutoa ruzuku kiasi kwenye *CAN*. Lakini tutaendelea kuwavutia wanunuzi kwa kupunguza sana bei ya *Urea* ili watumie *Urea* kwa wingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia suala la usimamizi. Haya mambo mengi yanayolalamikiwa kuhusu usimamizi wa hii mbolea ya ruzuku, yanatokana na usimamizi. Ziliundwa Kamati katika Wilaya, Mkoa na ya Kitaifa. Tulitarajia kwamba kila Kamati ingesimamia eneo lake, ile Kamati ya Wilaya inashirikisha Mkuu wa Wilaya, inashirikisha Mkurugenzi, inashirikisha Maafisa wa pale Wilayani. Kwa hiyo, hatukutegemea kuwepo kwa tatizo hata kidogo. Tutafuatilia hizi Kamati kuhakikisha zinaimarishwa lakini Mkurugenzi tayari yuko katika Kamati hii.

Suala la upungufu wa wataalamu lipo katika Idara zetu zote za kilimo na mifugo. Lakini nafikiri kuna tatizo la usimamizi na kuwapanga vile vile ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi. Kwa sasa wataalamu wa mifugo wanajua pia kilimo cha mazao. Kwa hiyo, ukiwa na mmoja angetusaidia kufanya shughuli zote lakini hata kwa *combination* hiyo bado wataalam ni wachache. Nakubaliana naye. Kuna haja ya kuchukua hatua kujiimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia Kituo cha Mbimba kwamba kimekuwa *neglected.* Tutahakikisha kwamba tunakitazama na kesho najibu swali hapa Bungeni juu ya utafiti. Tumetumia pesa nyingi sana katika utafiti na mwaka kesho tunatarajia kutumia shilingi karibu bilioni tatu katika eneo hili la utafiti. Kwa hiyo, tutawaimarisha hawa. Kuhusu *irrigation* tumeshazungumzia. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Lekule Laizer, alizungumzia juu ya ruzuku kwa mbegu, majembe ya kukokotwa na ng'ombe. Nakubali kwamba wananchi wa jimbo lake wanalima na wanafuga na wao wakulima, wanalima kwa ukubwa sana na nawapongeza sana kwa kazi nzuri.

Kwa bahati mbaya bado hatujafikia kutoa ruzuku kwenye mbegu na majembe ya kukokotwa na ng'ombe. Lakini tuombe Mwenyezi Mungu uchumi ukiendelea vizuri kama unavyokwenda, tutashughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba sasa kutoa hoja kwamba ripoti ya Kamati ya Kilimo na Ardhi ipokelewe na ikubaliwe. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi ya mwaka 2003 yalikubaliwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ukweli ni kwamba taarifa yenyewe wakati wanasoma ndivyo wanavyoomba.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri unafanya kujibu hoja ambazo zinatakiwa zijibiwe na Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01:33 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa Tarehe 29 Aprili, 2005 saa tatu asubuhi)*